ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Pili – Tarehe 29 Machi, 2012

DUA

Mhe.Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzíbar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuwasilisha mezani taarifa ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzíbar pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 29

Ahadi ya Boti Kwa Wanaushirika wa Tundaua

Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Aliuliza:-

Katika jitihada zake za kuwakwamua wananchi kiuchumi, Serikali hutumia mipango na miradi mbali mbali, kama vile miradi ya *MACEMP* na *TASAF*. Katika miradi hiyo Serikali imevipatia vikundi mbali mbali vya ushirika wa uvuvi mashua pamoja na vifaa vya uvuvi. Katika Kitabu cha Bajeti cha iliyokua Ofisi ya Waziri Kiongozi cha mwaka 2009/2010 kimeelezwa kwamba wananchi wa kijiji cha Tundaua Shehia ya Kilindi kupitia kikundi chao cha ushirika nao wamepatiwa boti ya uvuvi yenye thamani ya Tshs. 21, 442,000/=. Lakini kwa bahati mbaya sana boti hiyo hawajakabidhiwa wenyewe, na hadi sasa juhudi za kufatilia boti yao, zimegonga mwamba.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu.

(b) Je Wizara yako ni lini itawakabidhi wananchi boti yao hiyo ili nao waweze kujikwamua katika changamoto zao za kiuchumi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye kifungu (a) na (b) lakini kabla ya kumjibu, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mipango yake ya kuwasaidia wananchi kiuchumi huwashajiisha kuanzisha vikundi vya ushirika ili iwe rahisi kwao kuweza kupatiwa mikopo au misaada mbali mbali kupitia katika miradi mbali mbali ikiwemo miradi ya *MACEMP* na *TASAF*. Lakini tatizo kubwa linalotukabili ni baadhi ya vikundi vya ushirika kutokuelewana wenyewe kwa wenyewe au wengine kuuza vifaa wanavyopewa kwa ajili ya kujisaidia kiuchumi au wengine kuhodhi vitu wanavyopewa kwa ajili ya shughuli za pamoja. Jambo hili huvunja moyo jitihada za Serikali katika kusaidia wananchi kiuchumi.

Serikali kupitia mradi wa *TASAF* imekipatia kikundi cha ushirika wa kijiji cha
Tundauwa – Kilindi, Boti ya uvuvi yenye thamani ya Tshs. 21, 443,110/=.

(Thamani hii ni pamoja na mchango wa wananchi wa gharama za uendeshaji).
Kikundi hiki kimetajwa katika kitabu cha bajeti cha Afisi ya Waziri Kiongozi ya mwaka 2010/2011. Fedha hizo, zimeingizwa katika akaunti yao nam. 041108000853 iliopo Benki ya Watu wa Zanzíbar Pemba. Matumizi yake

yamefanyika kwa kufuata taratibu za Ofisi ya TASAF na kwa msaada wa wataalamu wa Wizara ya Kilimo kwa wakati huo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, napenda kukiri kuwa suala hili, Wizara yangu inalifahamu.

(b) Mhe. Spika, kikundi hiki kilishakabidhiwa rasmi boti na vifaa vyake vyote vya uvuvi, siku ya tarehe 08/01/2010 ikiwa sehemu ya shamra shamra za kuadhimisha Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka huo, zilizofanyika katika Shehia ya Wesha ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. Dadi Faki Dadi, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ukifungua ukurasa wa 72 wa kitabu cha iliyokuwa Afisi ya Waziri Kiongozi cha mwaka 2010/2011, katika Shehia ya Kilindi kuna vijiji viwili vilikabidhiwa mashua. Kijiji cha kwanza kilikuwa kinaitwa Tatugawe, Shehia ya Kilindi na kijiji cha Pili kilikuwa kinaitwa Tundauwa Shehia ya Kilindi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, katika kutafuta kwangu kijiji cha Tatugawe mashua ipo, lakini kijiji cha Tundauwa mashua haipo na ndio suala ambalo wananchi wameniuliza. Sasa namuomba Mhe. Waziri atufafanulie vizuri, ni kijiji kipi kilichopewa mashua na ikiwezekana namuomba sana twende kwenye eneo tukahakikishe kwamba hii mashua anayoisema kuwa imefika, imefika kweli. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kijiji cha Tundauwa Kilindi walipata boti moja na hiyo hasa ndio ilikuwa katika swali mama. Pia katika eneo hilo hilo la Kilindi katika kijiji cha Tatugawe na Kilindi, pia katika bajeti hiyo hiyo ya Waziri Kiongozi kama alivyosema yeye katika ukurasa wa 72, inaeleza kwamba boti hiyo wamekabidhiwa.

Sasa ikiwa kuna utata wowote namuomba Mhe. Mwakilishi yeye na mimi, Mkuu wa Wilaya na Afisa Mdhamini na Mkuu wa *TASAF* Pemba twende kwenye eneo hilo ili tukaone moja kwa moja. Kwa sababu taarifa iliopo ni kuwa boti hizo zimekabidhiwa na zilikabidhiwa katika sherehe za Mapinduzi. Kwa hivyo, itakuwa ni jambo la busara kwenda pamoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri anatoa kauli kwamba Serikali imetoa mashua katika vijiji hivyo vya Tundauwa, lakini wananchi wa kule wanaendelea kusisitiza kwamba mashua hiyo haikufika katika kijiji kimojawapo. Kwa kuwa kuna taarifa kwamba watendaji wa serikali katika ngazi za Wilaya na Mikoa wanakwamisha kwa makusudi juhudi za serikali yetu ya (*GNU*) yaani *Government of National Unity* katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato kwa wananchi.

Je, Mhe. Waziri au Serikali kwa ujumla itakuwa tayari kuchukua hatua kwa wale watendaji wa serikali katika ngazi za Mikoa na Wilaya, pindi tutakapouleta ushahidi wa wazi wazi wa kuweza kukabili juhudi hizo za Serikali?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba watendaji ambao wanafanya uzembe katika kutekeleza kazi zao na wale wanaosema maneno yasiyo sahihi katika kutekeleza kazi zao, basi Serikali itachukua hatua kali dhidi yao. Tunawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tusaidiane na mtueleze watu hao ili tuwachukulie hatua kali dhidi yao. Serikali yetu ya awamu ya Saba ina nia ya kuwahudumia wananchi wetu ili wananchi wetu wapate maendeleo. Wale wote wanaokwamisha nia hiyo basi hawana nafasi katika serikali hii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri sana. Mhe. Naibu Spika, mbali na vijiji vya Tundauwa ambavyo Mhe. Waziri alisema kwamba mashua hizo zimetolewa, lakini *TASAF* kwa kupitia ofisi yake ilifanyakazi kubwa sana kwa Zanzíbar nzima kugawa mashua hizi.

Je, sasa atakua tayari kufanya utafiti kwa Zanzíbar nzima ili kujua mashua zile zipo au tayari zimeshaliwa au zimeshanunuliwa changu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni nia na lengo la serikali kuwasaidia wananchi wake kujikwamua kiuchumi ili kuleta maendeleo zaidi. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kwa wale ambao wanaviuza vifaa mbali mbali wanavyopewa kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao, jambo hilo huvunja moyo jitihada za Serikali. Inabidi sasa tuchukue hatua maalum ili kupambana na watu wa aina hiyo.

Kwa hivyo, pia tutafikiria utaratibu wa kisheria utakaowafanya kwamba licha ya kuwachukulia hatua za kuwajibika na hata hatua za kifungo ziwezekane.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Hija kwamba utafiti ufanywe na wale wote ambao hawakutimiza wajibu wao katika kutekeleza malengo yaliyowekwa katika kujiletea maendeleo yao, basi hatua zichukuliwe.

Nam. 105

Tatizo la Dawa za Kulevya Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua hatua mbali mbali katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya. Hata hivyo idadi kubwa ya watuhumiwa wanaokamatwa na kufikishwa Mahakamani ni watumiaji badala ya wafanyabiashara wakubwa wanaoingiza dawa hizo Zanzibar.

(a) Mhe. Waziri, Je, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 wafanyabiashara wangapi wakubwa wa dawa za kulevya wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani na wangapi wamehukumiwa na Mahakama.

(b) Kwa nini washitakiwa wa dawa za kulevya wengi wanaokamatwa na kufikishwa Mahakamani Zanzibar ni wavutaji wa kete badala ya wafanyabiashara wakubwa wa dawa hizo.

(c) Mhe. Waziri, kutokana na ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya Zanzibar, kwa nini Serikali isiitishe kura ya siri ya kuwafichua waletaji na wauzaji katika mitaa ya Unguja na Pemba.

(d) Kwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Mizengo Pinda aliitisha kura ya siri ya watu waliyokuwa wakiwaua watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino) na kura hiyo imesaidia kupunguza ukubwa wa tatizo. Kwa nini na SMZ isiige mpango huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa kabla ya kujibu swali hilo napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilio chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ina jukumu kubwa la kuratibu na kudhibiti masuala mazima ya dawa za kulevya.

Hata hivyo, kukamilika kwa utekelezaji wa haya, taasisi mbali mbali zinahusika kwa njia moja au nyengine. Hivyo napenda kulifahamisha Baraza lako kwamba miongoni mwa masuala yaliyotolewa na mheshimiwa, utekelezaji wake hauihusishi moja kwa moja Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais peke yake, bali inashirikiana kwa karibu sana na wadau wengine wakiwemo Jeshi la Polisi, Mahakama na wengineo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nichukue fursa hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 jumla ya wafanyabiashara watano (5) wakubwa wa dawa za Kulevya wamekamatwa wanne (4) wamekamatwa *Airport* na mmoja (1) Bandarini katika tarehe tofauti kama ifuatavyo:-

Tarehe 10/7/2011 - *Airport* akiwa na pipi 96

Tarehe 16/7/2011 - *Airport* na pipi 133 na vifurushi 3 *(2kg)*

Tarehe 6/8/2011 - *Airport* akiwa na pipi 93

Tarehe 7/11/2011 - *Airport* akiwa na pipi 54

Tarehe 20/6/2011- Bandarini akiwa na mito 11, mafurushi 277 ya Bangi *(kg 13.87* za bangi)

Watuhumiwa wote hao wamefikishwa mahakamani ambapo kesi zao bado zinaendelea.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa waliokamatwa wengi ni wavutaji wa madawa ya kulevya kuliko wasafirishaji. Hii inatokana na ukweli kwamba mvutaji wa dawa za kulevya anaonekana kwa urahisi kutokana na hali yake na ni rahisi kupata vidhibiti dhidi yake. Vile vile hawa wako wengi zaidi kuliko wasafirishaji. Kwa upande wa wasafirishaji naomba ieleweke kuwa hawa watu wana mtandao mkubwa sana wa kimataifa na kitaifa, na wamejipanga vizuri, hivyo inakuwa vigumu kuweza kuwakamata na ukapata vidhibiti vya kuweza kuwatia hatiani kwa mara moja.

Hata hivyo, kwa kulitambua hilo Sheria Nam. 9/2009 imefanyiwa marekebisho ili kutoa nafasi nzuri zaidi ya kuweza kuwabana na kuwapata wasafirishaji. Pia nyinyi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ni mashuhuda wa hayo kwani tumeshaipitisha Sheria mpya na Mhe. Rais wa Zanzibar ameshaweka saini yake tokea tarehe 5/12/2011. Pia Serikali inaandaa mikakati madhubuti ya kuweza kukabiliana na changamoto katika kusimamia na kutekeleza sheria hii ili kukabiliana na wahalifu hao.

(c + d) Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali c na d kwa pamoja:-
Kura ya siri imesaidia kupunguza ukubwa wa tatizo kwa kuwakamata watuhumiwa waliokuwa wakiwaua watu wenye ulemavu wa ngozi, kama Mhe. Mwakilishi alivyoeleza. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inapokea ushauri huu na kuahidi kuufanyia kazi bila ya kuathiri Sheria zilizopo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na muafaka. Pindi tukipata watu kama nyinyi kwa majibu kama haya basi hatuna matatizo. Changamoto kubwa umetoa katika jibu lako hili la msingi.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa umekubaliana na kura ya kuwatafuta waliokuwa wahujumu wa Albino umesaidia kupunguza tatizo. Je, Serikali ni lini itaitisha kura hiyo kwa vile vijana wa Zanzíbar bado wanaendelea kuteketea na kuteseka na hawa ndio nguvu kazi ya taifa la kesho.

(b) Kati ya waliokamatwa Wazanzibari ni wangapi na Watanzania Bara ni wangapi na Wazanzibari wanaishi katika sheria zipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu mama nilieleza kwamba afisi yangu inauchukua ushauri wa Mhe. Mwakilishi wa kuweza kuona kwamba tunaweza kuitisha kura ya siri kwa ajili ya kuweza kuwabaini wasafirishaji wakubwa, au tunawaita mapapa wa dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Mwakilishi aipe muda afisi yangu ili itafakari kwa kina, kwa sababu pamoja na mafanikio ya kura ya siri kule ambako imefanyika Tanzania Bara, lakini kulikuwa na changamoto ambazo zilijitokeza za baadhi ya wananchi ambao kwa visingizio vyao wenyewe tu waliweza kuwataja watu wengine ambao hawakuwa wamehusika na kufanya zoezi zima lile la kuwatambua hao watu ambao walikuwa wanawakatili maalbino nalo kuwa gumu.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Mwakilishi aiamini afisi yangu kwamba pindipo tukikaa na kutafakari tukaona kwamba tunaweza kulijaribu na kuleta manufaa hapa, basi tutalifanya hivyo. Lakini akae vile vile na kuamini kwamba afisi haiko kimya nayo inajipanga katika mikakati yake ya kupambana kwa njia nyengine ya kuweza kuwabaini na kuwashika wahalifu hao.

Mhe. Naibu Spika, swali lake la Pili, naomba sana kwa kuwa linahusika moja kwa moja na kutaja majina na sehemu ambazo wanatoka watuhumiwa basi anipe muda basi nitamletea kwa maandishi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi kwa majibu mazuri na juhudi ya Wizara inayochukua katika kupambana na dawa za kulevya.

Swali ni kuwa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu udhibiti wa dawa za kulevya ni mkubwa katika bandari na viwanja vya ndege, siku hizi kuna mtindo wa wafanyabiashara hao wakubwa kusafirisha mali hii kwa kupitia bandari ambazo sio rasmi na kwa sababu ya uwezo wao basi wanafanikiwa kupita nazo na kuzisambaza na kuleta ile athari tunayopambana nayo.

Je, Mhe. Waziri umeweka mpango gani ambao ni mahususi wa mawasiliano ili popote suala hili likitokea katika bandari hizi ambazo sio za kawaida basi iweze kujulikana na kudhibitiwa ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kwanza naomba nikubaliane naye kwamba kuwepo kwa bandari zisizo rasmi kwa wingi sana katika visiwa vyetu ni changamoto kubwa inayoikwamisha Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake, hasa katika shughuli nzima za kuzuia magendo ya aina mbali mbali. Lakini pia katika shughuli za kiusalama.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imejipanga ili kuhakikisha kwamba mawasiliano yanawekwa ya kutosha katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, ili kudhibiti usalama katika bandari hizi ambazo zisizo rasmi. Hivi karibuni Serikali ya Marekani ilitoa boti mbili za *fiber* ambazo zitasaidia sana katika kuendesha *patrol* katika maeneo haya ili kuweza kufika kwa haraka ili kuona kwamba tunapata kuzifikia bandari hizi kwa haraka zaidi na usalama wa maeneo haya unalindwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Alipokuwa akijibu swali mama Mhe. Waziri amesema kwamba hivi karibuni wamekamatwa wahalifu wa dawa za kulevya ambao walipatikana katika maeneo ya uwanja wa ndege na bandarini. Kwa kweli uwanja wa ndege na bandarini ni sehemu kubwa ambazo zinapitishwa dawa hizi za kulevya, ukiachana na hizi bandari za panya.

Je, Mhe. Waziri kwa sababu sehemu hizi ndio maarufu umejipangaje kuweka zana za kisasa za kugundua wahalifu pindi wanapopitisha dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba watuhumiwa hawa tuliowataja wamekamatwa katika maeneo ya uwanja wa ndege na bandarini. Hivi sasa kama atakuwa alishuka katika uwanja wa ndege wetu huu wa Zanzíbar basi ataona kuwa tayari kuna vifaa ambavyo tunaviita *scanner* kwa ajili ya shughuli hizo za usalama. Lakini nataka nimueleze kwamba ni vigumu kwa kiasi fulani kuzitambua dawa, kwa sababu jinsi zinavyofichwa na hawa watuhumiwa inakuwa ni tabu sana kuyagundua.

Hata hivyo, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vina utaalamu wa kutosha na vinashirikiana na wataalamu wenzao wa ulinzi na usalama katika Tanzania, lakini pia na duniani ili kuweza kuwashika watuhumiwa hawa. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kamanilivyoanza kueleza mwanzo, suala hili ni la mtandao. Kwa hivyo, wanaanza kumchunguza mtu tokea maeneo ambayo anatoka na wanaweza kumshika kwa ajili hiyo, kuliko kuwa na chombo ambacho kinaweza zaidi kugundua kuwa amepita na dawa.

Hata hivyo, kwenye uwanja wetu wa ndege tutaona kwamba tayari kuna choo ambacho kinaweza kutumika kwa ajili ya kuweza kuwachunguza wale ambao wanashukiwa kuwa wana dawa ndani ya matumbo yao na kuweza kuzitoa na kuweza kupata ushahidi pale pale.

Nam. 18

Uchangiaji Huduma ya Maji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzisha utaratibu wa kupita kwenye maeneo ya Mijini na Vijijini kuchangisha gharama za maji. Kinachosikitisha kuhusiana na utaratibu huo ni kuwa baadhi ya maeneo yanayotakiwa kuchangia hayapati maji kabisa.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa nini ZAWA isidai michango kwa yale tu maeneo ambayo maji yanapatikana.

(b) Kwanini ZAWA isiweke utaratibu wa kutenga eneo la Mjini kuwa ni "*pilot area*" kwa suala la uchangiaji wa huduma za maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 18 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kimsingi napenda kutoa ufafanuzi mbele ya Baraza lako tukufu, kwamba suala la uchangiaji wa huduma ya maji ni la kisheria ambayo inamtaka kila mwananchi anaepata huduma ya maji safi na salama kuichangia huduma hiyo bila ya kujali Mkoa, Wilaya ama Shehia anayoishi, kinachoangaliwa ni kupatikana kwa huduma hiyo ya maji na kama ikithibitika mteja hapati huduma hiyo ya maji basi huwa hachangishwi.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2008 ZAWA, imekuwa ikishighulika na suala la uchangiaji wa huduma ya maji Mjini zaidi, kama ni eneo la mfano kwa kipindi chote hicho, kutokana na kuimarika kwa huduma ya maji safi na salama vijijini

ZAWA imeanzisha utaratibu wa kuwafikia wananchi walio vijijini kwa uchangiaji huduma hiyo kwa kutumia gari za *ZAWA*, kwa ajili ya kuwarahisishia malipo hayo badala ya kuja Afisi Kuu Mablue kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa vile Mhe. Naibu Waziri kwamba amekiri yapo matatizo ya maji na anawapeleka watu kwa gari kwa ajili ya kwenda kukusanya wakati huduma hiyo haipatikani.

(a) Hivi atakubaliana na mimi kuwa hivi sasa wizara imeshindwa majukumu yake na wala hawana usafiri.

(b) Serikali itatumia vigezo gani kwa gari za kwenda kukusanya zinapatikana, lakini wakati wa kwenda kufukua *pump* gari hawana na gari wanayoitegemea ni moja tu kutoka Wizara ya Kilimo, yaani sawa na kauka nikuvae.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, wizara haijashindwa katika kutekeleza majukumu yake au huduma ya maji.

Kuhusu huduma ya usafiri wa gari. Kwa kweli huduma ya usafiri wa gari tunaitumia kwa ajili ya kufuatilia malipo ya wananchi, pia tunatumia usafiri wa gari kwa huduma za kiufundi, ambapo ni tofauti na vile ilivyokadiriwa.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa mfumo uliopo umekuwa na malalamiko makubwa kwa wananchi, kwa sababu si wa uhakika ni wa kukadiria zaidi.

Sasa sijui ni lini Mamlaka imejipanga kuondokana na utaratibu huu na kuja na utaratibu ambao utakuwa na uhakika zaidi wa malipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ahsante wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) imejipanga vizuri katika suala la kushughulikia wananchi hususan katika suala la maji.

Kwa kuthibitisha hilo, ni kwamba kutokana na tamko la Mhe. Rais wa Zanzibar kuwa kutokana na shida iliopo hivi sasa ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi la tatizo la maji, basi Mhe. Rais ameagiza kwamba tuchimbe visima 9 na mpaka hivi sasa tayari tumeshachimba visima 3 ambavyo viko katika maeneo ya Chumbuni. Kwa kweli hiyo ni moja ya kuonesha kwamba Mamlaka imejipanga vizuri katika kulishughulikia suala hili.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini katika Jimbo langu la Rahaleo kwenye Shehia ya Makadara ndio sehemu ya mwanzo ya kufanyiwa majaribio ya kuwekwa mita, lakini baada ya kuwekwa mita zile ndio imekuwa tatizo maji hayapatikani katika maeneo ya Makadara.

Je, ni sababu gani zilizofanya kukosekana kwa maji baada ya kuwekwa mita hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme kuwa nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba katika eneo lake kuna tatizo la maji, lakini masuala hayo yanasababishwa na matatizo ya kiufundi. Kwa hivyo, *Inshaallah* tutajitahidi kulishughulikia suala hilo mpaka huduma ya maji ipatikane katika eneo lake.

Nam. 136

Wakulima Kutolimiwa Mashamba Yao

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kwa kuchukua juhudi za kupunguza bei ya uchimbuaji wa mashamba ya mpunga, bei ya mbolea na mbegu. Hata hivyo, bado kuna tatizo la Maofisa wa Kilimo kuchukua fedha za wakulima bila ya kuwalimia mashamba yao.

(a) Je, kuna sababu zipi zinazopelekea hali hiyo.

(b) Je, serikali haioni kwamba kufanya hivyo ni kuwadhalilisha zaidi wakulima wanyonge wa nchi hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili) – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo kuhusiana na Kilimo cha mpunga mwaka huu 2011/12, kwa ufupi kama kilivyozinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 17/10/2011 katika bonde la Cheju Unguja.
Wakati wa uzinduzi huo, mpango mzima wa kilimo hicho kwa mwaka huu ulielezwa, ambapo Mhe. Rais alikubaliana na mpango huo na ulielezwa utaratibu mzima utakaotumika wa kukusanya fedha za kilimo kutoka kwa wakulima, kupitia maafisa wa kilimo kwa kushirikiana na Viongozi wa Jumuia au Kamati za mabonde kama ilivyozoeleka. Kwa hivyo maafisa hao wa kilimo wanafanya kazi hiyo kwa maelekezo ya wizara.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu umefanywa ili kuwapunguzia gharama wakulima kwa kuwapatia huduma ya matrekta kwa bei ya ruzuku ya shilingi 16,000/- kwa ekari badala ya kulipa zaidi ya shilingi 32,000/- kwa ekari walizokuwa wakitozwa na Kamati za mabonde.

Mara tu baada ya uzinduzi, matrekta 14 yalikuwa tayari kuanza kazi ya uchimbaji lakini siku ya pili tu zilianza mvua kubwa za vuli zilizo dumu kwa miezi miwili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi hicho cha miezi miwili matrekta hayakuweza kufanya kazi na yalibaki vituoni, wakati tayari wakulima wengi walikuwa wameshalipa. Mara tu baada ya mvua kupungua matrekta yalianza kulima huku wakulima wakiendelea kuchangia. Baada ya kumalizika mvua, jua kali lilitoka kwa kipindi kifupi, maeneo mengi ya mabonde yalikauka sana kiasi cha matrekta kushindwa kulima kwa baadhi ya maeneo. Hali hii inatokana

na mabonde haya yanafugwa ng'ombe na kupata shindile katika ardhi ile kwa hivyo inakuwa ngumu ukitia jembe linakatika.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba hali ya hewa ni moja ya chanzo kikubwa kilichochangia wakulima wachelewe kulimiwa na walikuwa wameshalipa.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake yenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Maafisa wa Kilimo katika Vituo vya Kilimo kweli wanakusanya fedha za kulimia kutoka kwa wakulima, na hii kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na wizara na wanaandikiwa risiti baada ya kulipa. Fedha hizo zimewekwa katika Akauni Maalum na zinatumika kwa kununulia mafuta ya kulimia na vilainisho. Wizara inachukua juhudi ya kuhakikisha kuwa wakulima wote waliotoa fedha zao kuwa ziko salama na watalimiwa.

(b) Mhe. Naibu Spika, wakulima hawakudhalilishwa, kinyume chake ni kwamba wamesaidiwa sana kwa kulimiwa kwa bei ya ruzuku, na hivyo kuokoa fedha nyingi ambazo wangelipa katika jumuia.

Nachukua fursa hii kuwafahamisha wakulima wasiwe na wasiwasi kuchelewa kulimiwa, miongo inabadilika kutokana na mabadiliko ya tabia ya hali ya hewa.

Hivyo, na wao lazima wabadilike, waachane na kupanda mbegu za zamani za muda mrefu, badala yake wapande mbegu bora kwa wakati na za muda mfupi ambazo unaweza kupanda kuanzia mwezi wa Februari hadi Aprili. Mbegu hizo zinauzwa kwa bei ya ruzuku ya shilingi 200/- tu kwa kilo na Wizara ya Kilimo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Hivi atakubaliana na mimi kwamba wapo Maafisa wa Vituo ambao wamepokea kweli hizo fedha kama alivyokiri mwenyewe kwenye swali lake. Lakini mpaka hivi sasa katika usimamizi wa matrekta bado wanawadhalilisha wananchi katika upangiliaji mbaya.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Naibu Spika, ninachokifahamu ni kwamba kweli wapo wakulima ambao tayari wameshatoa fedha kwa ajili ya kuchimbiwa na kuburugiwa, lakini kama nilivyosema katika jibu langu la swali la msingi kwamba kazi hii ilichelewa kuanza na kwa sababu hiyo wapo ambao mpaka leo wengine bado hawajachimbiwa wala kuburugiwa, hivi sasa kazi inaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha kati tulipata matatizo ya matrekta kwa sababu ya ugumu, pale tuliharibikiwa na matrekta mengi sana. Kwa hivyo, tulilazimika kuchukua matrekta mengine 10 kutoka Dodoma JKT, ambapo 6 tuliyaweka Unguja na 4 tulipeleka Pemba na kazi inaendelea vizuri.

Kwa kweli, kwa mujibu wa takwimu ambazo ninazo, na jinsi ninavyopita katika mabonde, basi naona kwamba kazi inaendelea vizuri na muda wa mbegu hizi za Serikali upo.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema hivi sasa wakulima wakaacha kupanda zile mbegu za muda mrefu kama vile Ringa, Mpakulie Bwana, na Hali Bibi, waziache na wapande hizi zinazotolewa hivi sasa ambazo zinakwenda kwa muda mfupi sana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kwamba serikali imewarahisishia kupata mbegu na pembejeo za kutosha wananchi, lakini husababisha mbegu hizo kuwapa usumbufu wananchi na hufikia muda wa siku tatu kwa ajili ya kufuatilia mbegu hizo. Je, Mhe. Waziri haoni kama muda umefika kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kuwafuatilia wananchi majumbani kwao, kwa ajili ya kuondosha usumbufu huo.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Naibu Spika, nataka nieleze wazi na Waheshimiwa Wawakilishi wafahamu matatizo ambayo tunayopambana nayo katika mbegu, pia matatizo kama hayo tunapambana nayo kwenye mbolea.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli ipo *control* ya mbegu na *control* hii imeletwa kwa sababu inajulikana katika eka mbegu inahitajika kiasi gani, kwenye nusu eka mbegu inahitajika kiasi gani.

Lakini kwa bahati mbaya tulichokigundua ni kwamba watu wananunua mbegu na halafu wanaitwanga na kuila. Kwa kweli hali hii inatusababisha sisi tufanye *control* ya kutoa hii mbegu. Kwa hivyo, ni kweli anapokuja mtu tayari ameshachukua mbegu jana na leo akaja kusema anataka kuongeza kwa ajili ya kuipiga mchi na kuila, basi kweli tunazuia na tunamchunguza kwa muda wa siku tatu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza azma ya Mapinduzi ya Kilimo kwa nia nzuri, kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kupata chakula katika nchi yetu. Katika kuitikia wito huo serikali ilihimiza kufanya Mapinduzi ya Kilimo na kutumia mbegu bora.

Mhe. Naibu Spika, sasa napenda nimuulize Mhe. Waziri katika azma hiyo.

Je, eka ngapi zimelimwa kwenye nchi yetu katika kufanikisha Mapinduzi hayo ya Kilimo mpaka hivi sasa. e, kwa kuwa wananchi wameitikia wito huo wa kupanda mbegu bora, serikali imeandaa utaratibu gani ambao ni mzuri zaidi, ili wananchi kuwafikia mbegu hizo mpaka vijijini kwa ajili ya kubadilisha hizo mbegu za zamani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Naibu Spika, takwimu ambazo ninazo mimi na hasa Pemba, napenda kuwapongeza sana ndugu zetu wa Pemba. *(Makofi)*

Kwa kweli tulikuwa tumepanga kwa Pemba nzima kulima eka 2,200. Sasa neema ya karafuu iliyoingia Pemba na watu wakapata fedha nyingi, hadi hivi sasa nazungumza hapa basi tayari Pemba tumeshalima kwa asilimia 160 ya mabonde, yaani ni zaidi ya *hundred percentage* ya ile tuliyokusudia kuilima mwanzo na haya ndio Mapinduzi ya Kilimo. *(Makofi)*

Kwa upande wa Unguja pia najua kwamba kazi inaendelea vizuri, kuna mabonde hivi sasa yako kwenye asilimia 95, lakini waliolipa ni wengi zaidi kuliko ile ya asilimia 100. Kwa hivyo, wananchi wameitikia vizuri sana huu wito wa Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, mbegu tunaziweka katika maeneo ya baadhi ya Maduka ya *PADEP* pamoja na sehemu nyengine na watu wanakwenda kununua huko. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 27

Ujenzi wa Chuo cha Uvuvi, Pemba

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Hivi karibuni Balozi Mdogo wa China aliyepo Zanzibar Bibi Chen Qiman, alitembelea Mkoa wa Kaskazini Pemba na kuahidi kuwa nchi yake itajenga kituo kitakachotoa mafunzo mbali mbali yakiwemo mafunzo ya uvuvi, ili kuwapa Wavuvi wa Zanzibar mbinu za kisasa za uvuvi kwa madhumuni ya kusaidia kupunguza ukali wa maisha kwa wavuvi hao.

(a) Je, ni lini ujenzi wa kituo hicho utaanza.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vifaa vya kisasa vya uvuvi, wavuvi wa Kisiwa cha Kojani baada ya kupata mafunzo hayo, ili waweze kuimarisha shughuli za uvuvi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 27 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika ziara ya Balozi Mdogo wa China aliyepo hapa Zanzibar Mama Chen Qiman, alionesha nia ya kuisaidia Zanzibar kwa kujenga Kituo cha Utafiti wa Masuala ya Bahari ikiwemo tafiti mbali mbali zinazohusiana na shughuli za uvuvi na mazao ya baharini.

Nia ya kuendeleza mradi huu tayari zimekwisha anzishwa kwa kuwaalika Viongozi wa Utawala wa Mamlaka ya Taifa ya Bahari ya China (*State Ocianographic Administration*), ambao tayari wamefika nchini kwa ajili ya mazungumzo ya kusaidia ujenzi huo.

(a) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Serikali ya China zinaandaa Hati ya Makubaliano (MOU) kuhusiana na msaada huo wa ujenzi wa kituo hicho, na mara itakapokuwa tayari itatiwa saini.

Ujenzi wa kituo hiki unategemea kufuata taratibu za kikawaida za kiserikali zikiwemo:-

(i) Kuainisha eneo la ardhi na kupata Hati Miliki ya eneo hilo;

(ii) Kuandaa michoro halisi ya ujenzi wenyewe, ambao utapelekea kuandaliwa kwa bajeti halisi ya ujenzi wa kituo hicho;

(iii) Kupatikana kwa fedha hizo;

(iv) Kutangaza zabuni ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi huo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kukamilika taratibu hizo, ujenzi wa kituo hicho utaanza.

(b) Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Miradi ya *TASAF* na *MACEMP* tayari imekwishatoa vifaa vya kisasa vya uvuvi, ikiwemo boti, mashine pamoja na mitego kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo.

Hivyo, serikali itaendeleza juhudi za kuwaandaa wavuvi wadogo wadogo, kutoka kwenye maeneo yao ya ndani na kuwapeleka katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.

Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika naomba nitahadharishe kwamba juhudi hizi ni za muda mrefu, na kwa kuwa tunahitaji kujipanga pamoja na kuwa na bajeti ya kutosha, kwa ajili ya kuweza kupata mitaji ya kuwafikisha Bahari Kuu. Kwa hivyo, mpango huu hautakuwa kwa Kojani tu, isipokuwa ni kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kuwaboreshea wavuvi uvuvi wa kisasa na wenye tija.

Lakini kumekuwa na malalamiko makubwa dhidi ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2010, kwamba imekuwa ni kikwazo kwa wavuvi na wala hawapati fursa ya kufanyakazi vizuri kama ilivyotarajiwa.

Je, Mhe. Waziri ni lini sheria hiyo italetwa hapa Barazani kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho, ili wavuvi waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako tukufu likumbuke kwamba sheria hii ambayo aliyoitaja Mhe. Mwakilishi Sheria Nam. 7 ya 2010 ni ya karibuni sana, ambayo ni sheria mpya ya uvuvi na tuliipitisha karibuni sana ndani ya Baraza letu.

Kwa kweli nia ya Serikali Mhe. Naibu Spika kama alivyoeleza Mhe. Mjumbe, ni kuwaendeleza wavuvi na kuwapa fursa, ili waweze kuendelea na kwenda kwenye uvuvi wa kisasa, na wala sio kuwabana wavuvi wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimshauri Mhe. Mwakilishi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kama wameona kuna mapungufu ndani ya Sheria hii Nam. 7 ya mwaka 2010, ambayo yanawanyima fursa wavuvi wetu kuweza kuendelea na shughuli zao, naomba sana wawasiliane na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kueleza yale maeneo ambayo wanaona ndio hasa yanayokuwa ni kikwazo kwa wavuvi wetu, ili kwa pamoja tuweze kuyajadili.

Sasa ikiwa Serikali itaona ni kweli maeneo hayo ambayo Waheshimiwa watayaeleza kwamba yanawabana wavuvi wetu, basi serikali haitasita kuileta sheria hiyo ndani ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kufanya marekebisho, ili wavuvi wetu wawe na fursa ya kuendeleza kazi zao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri, wizara yake iliwachukua Wafugaji wa Samaki wa Unguja na Pemba na kuwapeleka nchini China, kwa ajili ya kupata mafunzo bora ya ufugaji wa samaki akiwemo mfugaji mmoja wa Jimbo la Kiwani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa eneo la Mwambe ni eneo moja ambalo limejaaliwa na mabwawa ya asili ya bahari ambayo hayakauki. Vile vile wananchi wa Mwambe wamekuwa wakifuga samaki kabla ya mafunzo ya China. *(Makofi)*

(a) Je, sasa Mhe. Waziri atakuwa tayari kuwachukua wafugaji wengine kuwaleta Mwambe kwa ajili ya kujifunza badala ya kwenda China.

(b) Kwa nini Kituo cha Mafunzo ya Ufugaji wa Samaki na Wavuvi hakijengwi Mwambe, ambapo kuna eneo la kisasa ambalo ni kubwa tena lenye mabwawa ya asili ya samaki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba arudie tena swali la pili sikulifahamu vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kama serikali ya China kupitia Balozi imekubali kujenga kituo cha Mafunzo ya Wavuvi, na kwa kuwa eneo la Mwambe lina mabwawa ya asili mengi yenye samaki wengi. Kwa kuwa eneo hilo liko huru halina shughuli nyengine za kilimo au ujenzi.

Kwa nini kituo hicho hakijengwi eneo la Mwambe na badala yake kinajengwa katika sehemu nyengine ya Zanzibar.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli hivi karibuni baadhi ya wafugaji wetu wa samaki waliweza kupatiwa fursa ya kwenda China kwa ajili ya kujifunza, na kupata utaalamu zaidi kwa lengo la kuendeleza shughuli zao.

Mhe.Naibu Spika, naomba nieleze kwamba hao ambao tayari tuliwapeleka kupata mafunzo yale, tunategemea kuwa watakaporudi hapa wawe ni chachu ya kuweza kuwasaidia wenzao waliomo ndani ya nchi, ambao hawakupata fursa hiyo ya kwenda kujifunza. Lakini hata hivyo jitihada hizi za kuweza kuwatoa zaidi wavuvi wetu, na wafugaji wetu wa samaki kwenda kujifunza zitaendelea kadri fursa zitavyopatikana.

Kuhusu swali lake la pili linalohusiana na ujenzi wa kituo hiki cha Utafiti wa Mambo ya Bahari yanayohusiana na Shughuli za Uvuvi. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba aipe nafasi Wizara ya Mifugo na Uvuvi itafakari kwa kina hasa ni eneo gani, ambalo litakuwa sahihi katika kujenga kituo hiki pamoja na sababu ambazo amezitoa, ambapo wizara inazichukua kwa ajili ya kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina azma ya kuondosha umasikini kwa wananchi wake, na kuleta kipato zaidi katika nchi. Sasa kwa sababu Zanzibar ni visiwa, tena tumejaaliwa na bahari iliyo nzuri, kubwa tena yenye mapato ndani yake.

Kwa hivyo, ni lini hasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kwa makusudi kuona kwamba sasa wakati umefika wa kuitumia Bahari Kuu, ili kuwapata wale samaki kwa ajili ya kuongeza kipato katika nchi yetu.

Je, kwa kuwa hivi sasa kumeanzishwa Wafugaji wa Samaki Wadogo Wadogo katika nchi yetu, ni lini serikali itawaongezea kipato, ili wananchi wale wasiwe wanafuga samaki wa kufanyia kitoweo tu na iwe samaki wa biashara.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, naomba kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba serikali inayo nia na kama ataangalia kwenye mipango ya serikali ya muda mrefu na mfupi, ya kuwatoa wavuvi wetu kwenda katika Uvuvi wa Bahari Kuu, kwa kuona

kwamba huko hasa ndiko kwenye manufaa na ndipo pale wananchi au wavuvi wetu watakapokuwa wamefaidika zaidi.

Kwa hivyo, naomba nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba, shughuli nzima ya Uvuvi wa Bahari Kuu haipo kirahisi kama uvuvi wa ndani, ambapo wavuvi wetu wadogo wadogo wamezoea kuvua. Kwa kweli uvuvi huu wa Bahari Kuu ni uvuvi ambao unahitaji kwanza vifaa vya thamani, yaani unahitaji mtaji mkubwa, ili kuweza kupata vifaa vya kuweza kufika huko, lakini pia utaalamu pamoja na uzoefu.

Mhe. Naibu Spika, kinachofanywa hivi sasa, ni kuandaa matayarisho hayo, kwa kuweza kuona kwamba serikali inaweza kupata wawekezaji, ambao wataweza kuekeza katika uvuvi huo wa Bahari Kuu, ili waweze kushirikiana na wavuvi wetu wadogo, kwa ajili ya kuweza kufaidika na wao. Kuhusu swali lake la pili, kweli kuwa serikali inayo nia ya kuwasaidia sana sio tu wavuvi, lakini hata wananchi wote kwa ajili ya kuondokana na umasikini.

Mhe. Naibu Spika, kuna Wizara Maalum ambayo imeundwa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, na nia ya serikali ni kwamba wavuvi hawa nao, watajikusanya katika vikundi, ili waweze kupatiwa mikopo ambayo itawasaidia katika kuendeleza shughuli zao.

Nam. 91

Uzalishaji Samaki na Nyama

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza :-

Zanzibar inao utajiri mkubwa wa bahari lakini pia inao umaskini wa ardhi. Mhe. Waziri Zanzibar ina utajiri mkubwa wa bahari ambayo bado haijatumiwa ipasavyo, huku wananchi wake wakinunua samaki na nyama kwa bei ya juu sana kutokana na upungufu wa samaki na nyama.

(a) Mhe. Waziri, kwanini Wizara yako haijazipa umuhimu Sekta za Uvuvi na Mifugo ili kuondoa matatizo yanayotukabili ya ughali wa kitoweo na umaskini.

(b) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuna haja ya kutafuta wataalamu wa uvuvi kutoka nje ya nchi ili kutoa taaluma ya uvuvi wa kisasa, ili wavuvi wetu waweze kuvuna mazao ya baharini kwa kiwango kizuri zaidi.

(c) Mhe. Waziri haoni kuwa kuna haja ya kuwapeleka wataalamu wetu wa uvuvi na mifugo kwenda kujifunza jinsi gani wenzetu wanaendelea katika sekta hizi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mh: Waziri wa Mifugo na Uvuvi) – Alijibu :-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Serikali yetu inatoa umuhimu mkubwa sana kwa sekta za mifugo na Uvuvi, na ndio maana kwa makusudi katika serikali ya awamu hii, imeundwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa madhumuni ya uendelezaji wa sekta mbili hizi maalum. Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaa na kutekeleza miradi tofauti ukiwemo mradi wa MACEMP na TASAF kwa lengo la kuondoa matatizo yanayotukabili, kutokana na kukosekana kwa kitoweo cha kutosha. Wazalishaji wetu wanapatiwa taaluma na misaada ya nyenzo za uzalishaji kutoka katika taasisi za nchini na kuombewa misaada kutoka nje ya nchi ili waweze kuzalisha kwa wingi lakini kwa uzalishaji endelevu ambao hautochafua mazingira na kusababisha matatizo hapo baadae.

b) Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu inawasiliana na wadau wa maendeleo mbali mbali wa ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kuwaendeleza wavuvi wetu kuweza kupata taaluma itakayowawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi. Lengo letu ni kuwapatia wavuvi wazalendo vyombo na taaluma itakayowawezesha kuvua kisasa na kuvuna kwa kiwango kizuri zaidi.

c) Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi ya kwamba, ipo haja ya kuwapatia wataalamu wetu elimu zaidi, ili waweze kuwashauri wazalishaji wetu juu ya mbinu za uzalishaji kwa ufanisi. Hivi sasa jumla ya wataalamu wetu 43 wapo masomoni kwa kujiendeleza katika taaluma zao. Aidha, jumla ya wafanyakazi 29 wamepatiwa masomo ya kujiendeleza nje ya nchi ndani ya mwaka huu wa fedha 2011/2012. Wafanyakazi hawa wanasomea fani za sekta ya mifugo na uvuvi.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri haoni kwamba wakati sasa umefika kwa Zanzibar kuweza kujenga Chuo kwa masuala ya uvuvi badala ya kukaa na kutegemea vyuo viwili ambavyo viko upande wa Bara tu na Zanzibar yetu yote imezungukwa na bahari.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Ni kweli na muda mrefu sana serikali inaona kwamba ipo haja ya kuwa na vyuo vya uvuvi hapa ndani ya Zanzibar, kama atakumbuka katika miaka ya nyuma tayari tulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa wanasoma michepuo ya uvuvi ndani ya Zanzibar. Mhe, Spika, serikali inalitafakari hili kwa njia ya kulipatia ufumbuzi na kuona kwamba tunapata vyuo vya uvuvi ndani ya Zanzibar.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa huko nyuma kulikuwepo na wanafunzi waliopelekwa China kwa mradi huo wa *MACEMP* na kwa taarifa tu, sasa hivi wanafunzi hao wako hapa Zanzibar. Je, ni sababu zipi zilizosababisha wanafunzi hao kurejeshwa?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mh: Waziri wa Mifugo na Uvuvi) Naomba nilichukue swali lake kwa ajili ya kulifanyia kazi na nitamletea majibu kwa maandishi.

Nam. 7

Huduma Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza :-

Upatikanaji wa huduma za Afya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja bado si za kutumainiwa sana.Kuna baadhi ya wakati wa mchana ambapo wagonjwa wanakwenda au kupelekwa Hospitali huwa hakuna kabisa Daktari wa kuwahudumia, na hivyo kulazimika kwenda kwenye hospitali binafsi au kurudi tena Mnazi Mmoja siku ya pili yake.

(a) Je, Mhe. Waziri anaelewa kuwepo kwa hali hiyo.

(b) Ni mikakati gani Wizara yako itachukua katika kupambana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu :-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Taarifa ya hali hiyo si ya kweli, na kwa kipindi kirefu sasa daktari dhamana wa Idara ya wagonjwa wa nje hajapata malalamiko hayo lakini kwa kuwa huduma hazitoshi, hilo linaweza kuwa kweli kwa sababu tunazidiwa sana na mzigo.

b) Mikakati ipo na inatekelezwa, kwani kuna ratiba ya kila mwezi ambapo madaktari 4 wanaingia asubuhi, 2 mchana na 2 usiku. Kwa utaratibu unaotakiwa kufuatwa ni kwamba, daktari hapaswi kutoka kabla anaeingia baada yake hajafika kazini, lakini napenda kukiri kwamba tuna upungufu wa

wafanyakazi wa kada mbali mbali katika hospitali yetu na hilo ndilo linalopelekea kwamba huduma zisiwe nzuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Katika majibu yako ulikuwa unasema sio kweli. Je, upo tayari kupokea majina ya watu waliokutana na mkasa huo au dharuba hiyo, na hatua gani utachukua pamoja na kuwa na upungufu wa madaktari.

b) Je, ni utaratibu gani ambao ulichukua Wizara yako kuelimisha wananchi juu ya haki zao za msingi za matibabu kwa kuelimisha kwa kupitia vipindi vya TV.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Inategemea mtu kaenda wapi utaratibu wa kwenda Mnazi Mmoja hospitali unatakiwa upitie kitengo cha wagonjwa wa nje, pale ndipo ambapo madaktari saa zote wapo utakapopaswa kulazwa au kwenda sehemu nyengine za wodini, kule madaktari wanakuwepo asubuhi tu kwa sababu ni wachache na wanafanya kazi zote zile za asubuhi pamoja na upasuaji na shughuli nyenginezo. Ikifika saa nane au wanapomaliza shughuli zao madaktari wale wanarudi majumbani mwao wanabakia madaktari wa *Intern* wawili ambao ndio wanaozunguka hospitali ile. Kwa hivyo inategemea mgonjwa anapokwenda, pengine wodi moja akamkuta daktari hayupo ama yupo kwenye wodi nyengine kwa hivyo utaratibu unafanyika kuita na kumhudumia mgonjwa katika wodi ile, pale ambapo daktari yule ameshindwa basi kwa lile ambalo analihudumia ndipo anapompigia sasa daktari ambaye yuko zamu anapokuja hapo kuja kumhudumia mgonjwa.

Dhana za wananchi ni kwamba kila utakapokwenda hospitali katika wodi umkute daktari, lakini madaktari tuliokuwa nao ni wachache wanakuwepo asubuhi na jioni wanaitwa pale inapokuwepo haja, vile vile nimesema kwamba tuna upungufu mkubwa wa madaktari kama tungelikuwa nao masaa 24 hospitali wangekuwepo madaktari.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi nilichouliza Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri yupo tayari kupokea majina kwa wananchi waliokutana na mkasa huo na Wizara yake itachukua hatua, jawabu lake sivyo alivyolieleza.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili bado hajajibu una haraka Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kama ni *out patient* naomba niletewe kama ni wodini si sahihi.

Mhe. Naibu Spika: Je, ni wodini au *out patient* Mheshimiwa Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pale pa kupokelea wagonjwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kama ni *out patient* naomba niletee.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa unaombwa umpelekee majina ili achukue hatua.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake, moja alisema si kweli, na madaktari wanakuwepo muda wote, lakini sasa hivi amesawazisha akasema kunako mapokezi na wodini. Lakini mimi nakwenda kunako mapokezi. Hivi karibuni Makamo wa Pili wa Rais alifanya ziara ya ghafla wakati wa usiku na alipokwenda kutembea kule hakumkuta daktari sehemu ya mapokezi, Je, Mhe. Naibu Waziri kauli hiyo anayotwambia hapa kwamba si kweli, je hili suala ambalo Makamo wa Pili alisema hakukuta madaktari haoni kama baraza kalidanganya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kunapokuwa na taarifa yoyote huwa tunaelezwa mimi hilo sijawahi kulisikia, kwamba Makamo wa Pili kenda *out patient* hakukuta madaktari, taarifa ya mwisho ambayo Makamo wa Pili alikwenda na wakati alipokwenda akakuta lifti haifanyi kazi umeme umezimika. Hicho ndicho ninachokijua mimi.

Kwa hivyo siwezi nikakubali au nikakataa hilo kwa sababu sina uhakika nalo.

Nam. 36

Ujenzi wa Jengo la Wizara ya Fedha Tibirinzi Pemba

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:

Muda mrefu umepita tokea kusimamishwa kwa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Tibirinzi, Pemba.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani juu ya jengo hilo.

(b) Kwa kuwa inaonekana ujenzi umefeli, ni nani atawajibika kulipa gharama za kufeli kwa ujenzi huo.

(c) Serikali iligharimika kiasi gani kwa ujenzi huo mpaka ilipofikia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu naona tena nichukue nafasi ya kumpongeza Mhe. Mohammedraza kwa kuwa nasi katika baraza hili tukufu, pia nawaomba waheshimiwa wajumbe tumuunge mkono kwa vitendo kama nilivyofanya mimi leo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli muda mrefu umepita tokea kusimamishwa kwa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo liliopo Tibirinzi Pemba. Hata hivyo, wakati ujenzi unasimamishwa mwanzoni mwaka 2011. Ofisi yangu ilikuwa haijakabidhiwa jengo hilo. Katika kulipatia ufumbuzi tatizo hili, mazungumzo ya muda mrefu yalifanyika kati ya Mshauri wa Ujenzi (*Consultant*), Mjenzi (*Contractor*) na Muajiri (*Client*) ambapo mazungumzo hayo hayakuweza kutoa ufumbuzi.

Kwa vile suluhu haikuweza kupatikana kiutaratibu, ilibidi tarehe 9/2/2012 suala hili lipelekwe kwenye Bodi ya Wakandarasi na ile ya wasanifu Majengo zote za hapa Zanzibar, kwa lengo la kufanyiwa uchunguzi wa kina, utakaopelekea kuchukua hatua ya usuluhisho (Arbitration). Hata hivyo kwa sasa, serikali haina mpango wowote hadi itakapopata ripoti ya uchunguzi.

(b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika kifungu (a), Serikali inasubiri matokeo ya uchunguzi unaofanywa na Bodi hizo kwa nia ya kupata ufumbuzi wa tatizo hili. Uchunguzi huo ambao huendana na ushauri ndio utakaotupa fursa ya kujua nani baina ya Mjenzi, Mshauri au wote wawili watakaowajibika kurejesha gharama zilizotumika.

(c) Mhe. Naibu Spika, mpaka ujenzi huo ulipositishwa, gharama zilizotumika ni Shilingi Mia saba na thalathini na sita milioni, laki nane na ishirini na sita elfu, mia tisa na thalathini na sita (TZS.736,826,936/=).

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu *a* na *b* kwa pamoja.

Kwa kuwa amekiri kwamba ujenzi ule umesita na bado wanatafuta ushauri.

a) Je, Mhe. Waziri anaweza akakiri kwamba ubovu wa mkataba uliofanywa ni moja wapo uliochangia kushindwa kupata ushauri kwa muda mfupi.

b) Kwa kuwa pale ni kiwanja cha ujenzi, na ujenzi wenyewe umefeli, Je, haoni kwamba wao ndio wanaozuia kiwanja kile kisitumike bila ya kuamua moja wapo.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Kwanza nataka niseme tu kwamba ningefurahi sana Mhe. Rashid Seif angenipatia kifungu kilichomo ndani ya mkataba ambacho hicho yeye anakiona ni kibovu na tukaweza kukifikisha kwa mwanasheria tukakubaliana kama kweli ni kibovu au sio kibovu. Lakini kusema mkataba mzima sidhani kuwa itakuwa sahihi na mimi kukiri kwa mkataba mzima sidhani kama itakuwa ni sahihi.

Ningelimuomba anipatie kifungu ambacho yeye anakihisi hiki ndio kifungu kibovu na hatimae tuweze kukubaliana kwa hilo.
Lakini la pili kwa sasa Mhe. Naibu Spika, utakubaliana na mimi kwamba kuliondoa lile jengo tutapoteza ushahidi, ni dhahiri kwamba lile jengo liendelee kuwepo pale mpaka kesi ya msingi itakapomalizika ili tusije kupoteza ushahidi, kesi ya msingi itakapomalizika basi ni dhahiri kwamba lile jengo tutalazimika kuliondoa kulingana na maelekezo tutakayoyapata hapo baadae.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, wakati jengo hili lilipokuwa likijengwa mimi, nilikuwa katika kamati ya *PAC* na baada ya kuona ubovu wake tukafuatilia sana na mwisho wake tukapata wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa jina la siku hizi na wakatueleza kwamba walitoa ushauri wao wa kina kabla ya jengo kuanza kujengwa, lakini ushauri ule haukukubaliwa.

a) Je, Mhe. Waziri analijua hilo.
b) Mheshimiwa ametwambia kuwa mpaka hivi sasa kama rekodi zangu sahihi jengo limetumia jumla ya TZS 736,826,936/= na kama hivyo ndivyo kwa thalasini na sita, thalasini na sita hizo naweza nikapata ufafanuzi hasa wa kifungu kwa kifungu mpaka hesabu ikawa hii.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, mimi ni Waziri ambae nimeteuliwa mwaka Jana sijapata taarifa kwamba kulitolewa ushauri na Wizara ya Ardhi, kama ushauri ulitolewa na Wizara ya Ardhi, itakuwa amepatiwa mshauri ambae alikuwepo kwenye *site*, na kama ushauri huo alipatiwa na Wizara ya Ardhi hakuutekeleza hili itakuwa ni kosa moja la mshauri na sisi kwa upande wetu tutalifanyia kazi, namshukuru Mheshimiwa na mimi nitafuatilia ushauri niweze kuona kama umetolewa kwa maandishi, na mimi niweze kusoma na kuufahamu.

Kifungu cha (b) cha suala lake ametaka nimtolee mchanganuo, naomba nimtolee mchanganuo kama ifuatavyo.

Shs. 645,590,505 Ameshalipwa mkandarasi
Shs. 81,176,432 Amelipwa Mshauri *(Consultant).*
Shs. 2,100,000 Zimetolewa kwa matayarisho ya kazi nyengine.
Shs. 6,844,000 Zimetolewa kwa ajili ya uzabuni na
Shs. 1,116,000 Zilikuwa zimetumika kwa ajili ya uzabuni na tulipositisha ujenzi kulikuwa kuna gharama hizo tulilazimika kulipa shs. 1,116,000 zote zimekuja milioni TZS 736,826,936/=

Naomba Mhe. Muwakilishi kama hajanipata vizuri nitampatia kopi ya hizo fedha ambazo tumeshazitoa kwa kila mtu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa tokea kusimamishwa kwa ujenzi huo ni muda mrefu, na kwa kuwa kadiri siku zinavyopita ndio gharama za ujenzi zinavyopanda juu kila siku, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katwambia hapa kwamba Bodi ya Mkurugenzi.

Sasa anaweza kutwambia ni lini taarifa ya bodi hii itakuwa tayari ili gharama za ujenzi zisije zikaongezeka zaidi na zaidi.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Ninachoweza kusema ni kwamba bodi hizi mbili hiyo kazi wameshaanza, na nina imani kubwa watamaliza katika kipindi kifupi kijacho, siwezi kutoa ahadi ni lini watamaliza, lakini kwa sababu ya unyeti wa suala lenyewe, nina imani kwamba mwezi ujao hautomalizika watakuwa wameshatupatia ripoti.

Nam. 118

Wafungwa Kucheleweshwa Nakala za Hukumu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mwaka 2007/2008 ukurasa 137 imezungumzia malalamiko ya wafungwa kucheleweshewa nyaraka za hukumu na kusindwa kukata rufaa jambo ambalo ni kinyume na misingi ya Haki za Binadamu.

a) Je, Mhe. Waziri ni kwa sababu gani nakala za hukumu na mwenendo wa kesi hucheleweshwa kwa wafungwa.

b) Serikali itachukua muda gani kuondoa tatizo hilo pamoja na tatizo la msongamano wa mahabusu na wafungwa katika Vyuo vya Mafunzo Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu inaelezea katika ukurasa wa 137 mambo mengi yakiwemo:

i) Kucheleweshwa kwa nakala za hukumu
ii) Kutojuilishwa dhamana zao
iii) Kutorejeshewa mali zao zinazowekwa dhamana na
iv) Kutopewa vielelezo vyao wanapohamishwa kutoka chuo kimoja kwenda chuo chengine.

Mhe. Naibu Spika, ripoti hii kwa bahati nzuri na mimi nimeisoma kikamilifu. Baada ya kusema hayo napenda niseme tu kwamba, maelezo yote yaliyoelezwa na ripoti hiyo katika ukurasa huo ambao nimeutaja inahusiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Na hapa Mhe. Naibu Spika, napenda nieleze tu kwamba, wizara yangu inahusika na wafungwa au wanafunzi pale ambapo wanapelekwa Mahakamani mpaka kesi zao zinapomalizika. Wanafunzi hao wakishapelekwa Chuo cha Mafunzo, wizara yangu haina dhamana tena ya wanafunzi hao, dhamana ile inabakia katika Ofisi ya Rais Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Hata hivyo, baadhi ya mambo ambayo yanakwamisha utekelezaji mzuri tumeshazunguma na uongozi wa Mahakama na yameshaanza kuchukuliwa hatua, ingawa naamini kutakuwa na kasoro ndogo ndogo za hapa na pale. Lakini naomba pia niliahidi Baraza lako tukufu kwamba bado tutazidi kuyatatua ili wenzetu hawa wasitiwe katika dhiki za makusudi. Lakini zaidi nimeshazungumza na Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili tuweze kuyatatua baadhi ya mambo ambayo yameelezwa katika ripoti hii.

Matatizo mengine kama vile upungufu wa makarani na mashine ya kupigia hukumu, mambo ya wino nayo pia tumeyaona. Na haya kwa upande wangu tumeyachukulia hatua kidogo, tumejaribu kutafuta mashine hizi za kupigia type, tumeongeza makarani na hayo tunafanya ili wenzetu hawa wasipate matatizo.

Mhe. Naibu Spika, suala la msongamano wa wafungwa yaani wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo, kama nilivyosema mwanzo ni suala ambalo linahusiana na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lakini Serikali kwa ujumla kwa sababu ya kukerwa na tatizo hili, wameshaanza kulichukulia hatua ya kupunguza msongamano huo. Hivi sasa kutokana na maelezo haya tuna hakika kwamba ule msongamano hasa kwa mfano wa watoto kuwa pamoja na watu wazima tumeshauondoa moja kwa moja.

Hivi sasa Serikali imeshapata eneo kubwa la ujenzi wa chuo Kikubwa cha mahabusu katika eneo la Hanyegwa Mchana. Chuo hicho kitakapokamilika kitakuwa na sehemu tofauti zinazowatenganisha watoto na watu wazima.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Saydina Abubakar kwa kuwa haki ya kukata rufaa kwa wafungwa ni haki za Kikatiba.

(a) Je, Serikali inalinda vipi haki hiyo hasa ukizingatia Tanzania imesaini mkataba wa Haki za Binaadamu za Umoja wa kimataifa.

(b) Kwa vile tukio kubwa la vitendea kazi ni tatizo, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mfuko wa fedha wa Mahakama ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, wafungwa hapa wana haki mbili. Kwanza anapokuwa Mahakamani kwa mfano Hakimu akasema anamtia hatiyani na kumfunga miezi sita kwa mfano. Pale pale hakimu kwa mujibu wa sheria lazima atamke kwamba una haki ya kukata rufaa katika kipindi cha mwezi mmoja. Lakini anapofika Gerezani au Chuo cha Mafunzo, kama nilivyosema sasa utawala wa kule upo chini ya Afisi ya Rais, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lakini na wao kule wanawajibika kuwaelimisha wanafunzi hawa kwamba na wao wana haki ya kukata rufaa. Walimu wa kule yaani askari na wao wanawajibika pia kuchukua hatua za kushughulikia mafaili yao ili waweze kukata rufaa.

La pili Mhe. Naibu Spika, ni suala la kuhakikisha kwamba haya yote yanalindwa kwa mujibu wa Katiba na haya tumeyazingatia katika Bajeti zetu na katika shughuli nyengine ambazo mara kwa mara tunawasaidia wanafunzi ili kuhakikisha haki zao zinakwenda kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa mikataba ya ulimwengu.

TANGAZO

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri kipindi cha maswali kimekwisha kwa hivyo nina tangazo moja naomba Waheshimiwa mlisikilize kwa makini.
Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais amesema kwamba wale waliokamilisha kujaza zile fomu za miradi ya majimbo tuwakabidhi vijana wetu hawa wazikusanye ili zipelekwe Wizarani kwa hatua iliyobakia. Kwa hivyo mtu kama hakupeleka atajicheleweshea mwenyewe.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya
Jimbo Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya na kutuwezesha kufika hapa kwa ajili ya kufanikisha majukumu yetu tuliyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba kwa ruhusa yako uniruhusu nitoe mkono wa pole kwa wafiwa, wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mhe. Mtondoo. Hiyo ni kazi ya Mwenyezi Mungu na tumuombee dua amlaze mahala pema Peponi. Amin.

Aidha Mhe. Naibu Spika, nakuomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati kabisa ndugu yangu Mhe. MohammedRaza kwa ushindi mkubwa alioupata katika jimbo lake la Uzini. Tunamuhakikishia kwamba Serikali tupo pamoja naye katika kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia uniruhusu nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu leo ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Aidha Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Baraza lako Tukufu ya kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa michango yao muhimu sana katika kufanya Mswada wetu huu uwe mzuri kama unavyoonekana. Naomba nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Hamza Hassan Juma. Waheshimiwa wajumbe wote wa Makatibu wa Kamati hiyo kwa michango, ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia ambao umeonesha nia zao njema katika harakati za kuongeza kasi ya maendeleo katika majimbo yetu.

Aidha niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa wanayoipa Serikali katika kutekeleza majukumu yetu.
Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani hizo sasa naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu uliwasilishwa katika Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza lako tukufu na ukachangiwa na kutolewa maoni ya kuufanya uwe bora zaidi ambapo marekebisho yaliyofanywa yamezingatiwa ipasavyo na Serikali. Michango hiyo hasa ililenga zaidi katika marekebisho ya lugha na kupendekeza baadhi ya vijifungu vya baadhi ya vifungu ama viandikwe tena au vifutwe na ni mambo ambayo yalitekelezwa kwa juhudi kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba hapo baadaye umruhusu Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yako tukufu ya viongozi wakuu wa serikali aviainishe vifungu vyote vilivyofanyiwa marekebisho na kamati yake ya kukubaliwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, dhamira kubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuwapelekea huduma mbali mbali zikiwemo za maji safi, barabara, elimu, afya, pamoja na rasilimali nyengine zitakazowezesha wananchi hao kujikwamua kiuchumi. Ingawa huduma hizo zinaendelea kutolewa na Serikali pamoja na sekta binafsi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kuna haja ya kuona utaratibu utakaoratibiwa vizuri zaidi katika utoaji wa huduma hizo katika ngazi za Majimbo chini ya misingi madhubuti ya kisheria. Aidha kuna umuhimu mkubwa wa maendeleo hayo kusimamiwa na viongozi ambao wananchi wamewachagua hususan wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huu kunapendekezwa kuanzishwa kwa sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar ambao utatarajiwa kuharakisha maendeleo. Mfuko huu utawashirikisha kwa ukaribu zaidi wananchi wenyewe hasa katika uteuzi na utekelezaji wa miradi mbali mbali katika majimbo yao kulingana na vipau umbele vyao.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu uliokuwa ukitumika zamani katika kugharimia miradi ya wananchi katika majimbo ulikuwa unaratibiwa na Wizara ya Fedha ambayo ilikuwa inatoa fedha kwa miradi midogo midogo ya maendeleo iliyobuniwa na wananchi kwa kuzingatia maombi yaliyowasilishwa.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huo umekuwa ukileta malalamiko kutoka kwa wananchi pamoja na viongozi wao. Aidha utoaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi mara nyengine ulikuwa hauzingatii usawa wa majimbo. Pia utaratibu huu ulikuwa hauongozwi na sheria maalum na hivyo kuufanya kutokufahamika vyema miongoni mwa wananchi.

Madhumuni makuu ya Mswada huo ni kuanzisha Mfuko wa maendeleo ya Jimbo Zanzibar, utakaoweka mazingira bora na endelevu ya kusaidia nguvu za wananchi katika kujiletea maendeleo na kupunguza umasikini katika majimbo yao. Utekelezaji wa mfuko huu utahamasisha maendeleo katika majimbo yote ya Unguja na Pemba, vile vile kutaweka uwiano wa maendeleo miongoni mwa majimbo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Majimbo umeanza kutekelezwa na nchi nyingi duniani zikiwemo nchi ambazo mabunge yake ni wanachama wa Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA), ambapo Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni miongoni mwa wanachama wa chi zilizoanza kutekeleza Mifuko ya Majimbo na ambazo zimekuwa ni mfano wa kuigwa kwa maendeleo yaliyopatikana katika majimbo kupitia mifuko hiyo ni pamoja na Kenya, India na Jamaica.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huo wa kuwapelekea wananchi maendeleo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo utawapunguzia viongozi wa majimbo mzigo mkubwa wa uchangiaji binafsi katika maendeleo ya majimbo yao.
Mhe. Naibu Spika, Mswada huu umegawika katika Sehemu Nane nazo ni kama hivi ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza	Inahusu utangulizi, inajumuisha jina fupi la Mswada, tafsiri na kutumika kwa sheria hii.
Sehemu ya Pili	Inahusu uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Usimamizi wa Fedha kwa ajili ya mfuko huo, vyanzo vyake vya fedha pamoja na utaratibu wa upelekaji fedha katika Majimbo. Vile vile sehemu hii inampa mamlaka katibu Mkuu anayeshughulikia mfuko kusimia utekelezaji pamoja na kupokea malalamiko mbali mbali yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa kazi za Mfuko.
Sehemu ya Tatu	Inaelezea kuhusu uwanzishwaji wa Kamati za Maendeleo za majimbo, miundo, pamoja na kazi za kamati za maendeleo ya Jimbo.
Sehemu ya Nne	Inahusu uwasilishwaji na upitishwaji wa mapendekezo ya miradi ya wananchi na namna yatakavyotathminiwa kabla ya kupitishwa na Kamati za Maendeleo ya Jimbo. Sehemu hii pia inaelezea kuwasilishwa na kupitishwa kwa miradi ya majimbo inayopendekezwa.
Sehemu ya Tano	Inahusu aina ya miradi inayoweza kupatiwa fedha kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.
Sehemu ya Sita	Inahusu utekelezaji wa miradi na ushiriki wa Kamati za Maendeleo za Majimbo na Wananchi ndani ya Majimbo katika utekelezaji wa miradi hiyo.
Sehemu ya Saba	Inahusu masharti ya fedha na namna ya kufanya matumizi, utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka muhimu pamoja na ukaguzi wa fedha zilizoingizwa kwa ajili ya miradi hiyo.
Sehemu ya Nane	Inahusiana na Mambo mengineyo yakiwemo kumpa uwezo Waziri anayehusika na Masuala ya Baraza la Wawakilishi kwa kutunga kanuni. Aidha sehemu hii inaelezea makosa yanayoweza kufanyika chini ya sheria hii na kuweka adhabu kwa makosa hayo.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu unapendekeza mambo mawili yatuatayo:-

(1) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar *(Zanzibar Constituency Development Fund)* ili kuwa na utaratibu mzuri zaidi ya kuharakisha maendeleo kwa wananchi wake.

(2) Mfuko huu uingiziwe fedha kutoka mfuko Mkuu wa Serikali ili kuzigawa majimboni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wamepata muda kuusoma kwa makini Mswada huu pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Hivyo Mhe. Naibu Spika, nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili Mswada huu kwa kina, watoe mapendekezo na hatimaye waupitishe.
Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja iamuliwe)

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru kunipa nafasi hii nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa taarifa ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kwa mara nyengine kukutana mbele ya Baraza lako tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema ili kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo ya Nchi yetu pamoja na mustakabali mzima wa wananchi wetu, likiwemo suala la kujadili na kupitisha miswada mbali mbali ukiwemo mswada uliopo mbele yetu. Mswada wa Sheri ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hapa Zanzibar na Mambo Mengine yanahusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya kamati kutoa mkono wa pole kwako wewe binafsi kwa ofisi yako, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wananchi wa Jimbo la Bubu na Familia ya marehemu aliyekuwa Mheshimiwa mwenzetu marehemu Salum Mtondoo aliyekuwa mjumbe wa Baraza la

Wawakilishi wa jimbo la Bububu, ambaye alifariki tarehe 15/3/2012 na kuzikwa tarehe 15/3/2012, katika kijiji chao Bumbwini Misufini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu Peponi. Amin.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Kamati kutoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuwasilishia mbele ya Kamati Mswada huu na kuweza kuujadili kwa kina na uwazi na baadaye kutoa mapendekezo yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda uniruhusu niwashukuru kwa dhati, Wajumbe wa Kamati yetu kwa mashirikiano na michango yao muhimu waliyoitoa katika kuujadili kwa kina Mswada huu siku ya Jumatano ya tarehe 21/03/2012. Naomba uniruhusu niwataje Wajumbe wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohammed Ali - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai - Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg. Ramadhan Kh. Masoud - Katibu

Mhe. Naibu Spika, utakumbuka kwamba chimbuko la Mswada huu lilianza mwaka 2002 wakati katika vikao mbali mbali vya bajet suala hili lilijitokeza mara kwa mara.

Mhe Naibu Spika, hili halikuja bure bure tu, sababu kubwa ya Wajumbe wako kudai Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ilikuwa ni hamu kubwa ya wananchi wetu wa Zanzibar kutaka kujiletea maendeleo katika majimbo yetu, lakini uwezo wao unakuwa mdogo na wananchi wetu wao kimbilio lao ni kwa Wawakilishi wao. Wao mara nyingi hawajui kama hali za Wawakilishi wao zinakuwa dhaifu kwani wanabeba majukumu makubwa majimboni yaliokuwa ya maendeleo na ya watu binafsi ambayo ndio mengi zaidi. Kwani kutokana na hali ngumu za maisha kwa wananchi wetu kimbilio lao kubwa linakuwa ni kwa Wawakilishi wao. Wanapokujia na shida zao wao hawajui unacho au huna.

Mhe Naibu Spika, ukiangalia Wajumbe wako kila mmoja anaongoza watu zaidi ya elfu ishirini katika jimbo lake na kila anaekwama wakatimwengine hata chejio basi kimbilio lao huwa kwa Mwakilishi wao.

Mhe Spika hii sio kama tunawasimbulia wananchi wetu bali ndio hali halisi ilivyo. Tunawahakikishia wananchi wetu waliotuchagua kuwa hatununi wala hatukasiriki tunafurahi sana kila wakija kutueleza shida zao kwani tunaamini kila anaekuja kukueleza shida yake basi amekukinai na anakuthamini. Lakini mara nyingi uwezo wa kuwasaidia watu wote wanaotujia tunakuwa hatuna. Lakini kila tunapokuwa nacho tunajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu Mwenyezi Mungu aliotujaalia kuwasaidia.

Mhe Naibu Spika, kutokana na mapenzi tunayowapenda watu wetu waliotuchagua, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi yeyote akiwa amekaa siku tatu mfululizo hajaendewa na wananchi wake kumuelezea shida zao, basi huwa hapati usingizi kwani anahisi labda wameshaanza kumchoka.

Na yeye mwenyewe utaona anajipeleka mwenyewe au kujipitisha pitisha mitaani alau apate kuelezwa japo shida mbili tatu nahiyo ndio maumbile ya kazi yetu. Kwa hiyo tunawaomba wananchi wetu msichoke kutujia na shida zenu pale tutakapokuwa nacho tutawasaidia na pale tutakapokuwa hatuna basi wala msikasirike kwani hakuna alie kamilika.

Mhe Naibu Spika, kazi yetu Wawakilishi ni ngumu sana kwani aliyeko nje humlaumu alieko huku ndani lakini miezi miwili tu akiingia humu ndani utamkuta anaanza kulalamika kwa kuwa ana maombi mengi ya wananchi lakini uwezo wa kuyahudumia anakua uwezo wake ni mdogo. Kwa hiyo waheshimiwa wenzangu tujitahidi kufanya kazi zetu kwa bidii ili kuiondoa hali hii na njia pekee ya kuliondoa tatizo hili ni kuibua miradi mikubwa ya kiuchumi hapa Zanzibar. Tuendelee kushikamana kutafuta vianzio vipya vya mapato ikiwemo utafutaji na uchimbaji wa

mafuta hapa Zanzibar, ili rasilimali hiyo ije kuwasaidia Wazanzibari wote kwa ujumla. Inshaallah kwa uwezo wa Allah atatuwezesha kwa uwezo wake.

Pia tujitahidi kisimamia ukusanyaji wa mapato hapa Zanzibar ili yasivuje ili Mfuko wetu Mkuu wa Fedha za Serikali upate fedha za kutosha ili Serikali yetu iwe na uwezo wa kuwahudumia wananchi wetu kwa ujumla.
Mhe Naibu Spika, nimeamua kuyaeleza hayo kwa makusudi ili serikali iweze kujua ni kiasi gani waheshimiwa tunavyosaidia Program ya kuondoa umasikini huko majimboni kwetu.

Mhe Naibu Spika, hayo yote tunayakabili majimboni mwetu lakini kwa uwezo mdogo tuliokuwa nao inakuwa ni vigumu kuyamudu hayo yote, ndio maana Waheshimiwa wako wakawa wanahitaji alau kuwe na Mfuko wa jimbo ambao utaweza kutusaidia kwa yale mahitaji muhimu ya kijamii na maendeleo katika majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu kwa muda mwingi ilikuwa haijaweka utaratibu maalum wa kumuwezesha Mwakilishi kupata fedha za uhakika za kuondoa kero kwa wananchi majimboni mwetu. Ingawa kulikuwa na fungu la miradi midogo midogo kupitia Wizara ya Fedha, lakini halikuwa na utaratibu mzuri na wa uhakika kuzipata fedha hizo. Kama huu utaratibu ambao Serikali yetu kwa hivi sasa, imeleta sheria hii ambayo baada ya kuipitisha tunaamini utaweza kusaidia wananchi wataweza kufaidika na fedha hizo, napengine hata utaratibu wa kusimamia fedha hizo wakati mwengine kwa hapo nyuma ulikuwa sio mzuri, lakini kupitia Sheria hii tutakayoipitisha tunaamini utaweza kutusaidia kuondoa baadhi ya kero ndogo ndogo majimboni mwetu. Baada ya maelezo hayo machache sasa naomba kutoa maelezo mafupi ya mswaada huu.

Mhe Naibu Spika, tunaishukuru Ofisi yako ya Baraza la Wawakilishi mnamo mwaka 2008/2009 ilifanya ziara nchini Kenya kwenda kujifunza ni namna gani Mfuko huu umeweza kusaidia vipi wananchi wa Kenya. Nashukuru Mhe Naibu Spika, ofisi yako ilinishirikisha na mimi kwenda kujifunza katika nchi ya Kenya kwa kweli nimeona tumechelewa sana kuanzisha Mfuko huu. Tulipata nafasi ya kuongozana na Mbunge mmoja wa kule Kenya wa Jimbo la Naivasha kwenda kujionea kwa macho yetu maendeleo aliyoyapata kupitia Mfuko huu wa jimbo.

Mhe. Naibu Spika, mfuko huu kwa kweli yapo mengi sana ambayo waliyofanya lakini nitayataja machache kutokana na muda tulikuwa nao. Kwa mfano katika jimbo tulilolitembelea la Naivasha kule Kenya ametueleza kwamba tangu kupata Uhuru wa Kenya miaka 30 iliyopita, katika jimbo lake kulikuwa na Shule za Sekondari tano tu. Lakini baada ya kuanzisha Mfuko wa Jimbo ndani ya miaka sita waliweza kujenga Shule za Sekondari kiasi 15, kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo. Wameweza kujenga barabara za ndani nyigi sana katika maeneo mbali mbali, amediriki hata kujenga Gereza la watoto ndani ya jimbo lake. Baada ya kutembelea Gerezani la watoto ndani ya jimbo lake baada ya kutembelea gerezani na kuona watoto wadogo wamefungwa pamoja na watu wazima ambao wanaweza kuwaazaa.

Pia sheria yao inawaruhusu kusadia malipo ya ada ya shule kwa wale watoto ambao wamefaulu lakini wazazi wao hawakuwa na uwezo wa kuwalipia ada, pia wameweza kuwapatia fedha na kuwaanzisha miradi midogo midogo vijana ambao walikuwa wakikaa vijiweni (maskani) bila ya kazi yoyote. Pia waliweza kuwapatia *tender* kupitia Baraza la Mji ya kutengeneza Makalbi, *Calvart* na kujenga vikuta pembezoni mwa barabara. Kwa hiyo, fedha zile zimewasadia sana wananchi wa Kenya kuondoa matatizo mbali mbali katika majimbo yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa fedha za Kenya wenzetu wao hupatiwa kiasi cha Kenya Shs 20 milioni kwa mwezi kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwani wao wameweka asilimia 2 ya mapato yote ya Kenya, ndio moja kwa moja huingia kwenye mfuko wa Jimbo kutoka mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Kenya. Lakini kwa kwa kuwa sisi ndio kwanza tunaanza kutokana na makusanyo yetu kuwa madogo tunashukuru japo kwa kuanzia hizo fedha zilizotengwa na serikali yetu shilingi milioni 10 kwa mwaka zitaweza kutusaidia japo kidogo. Lakini Mhe. Naibu Spika, tunaiomba Serikali yetu kutokana na mfumko wa bei hasa vifaa vya ujenzi kwa hivi sasa pesa hizi bado ni ndogo sana kwa hiyo tunaomba bajeti ya mwakani ziongezwe alau kufikia milioni 20 kwa mwaka. Tunajua hali ya Serikali yetu bado ni changa lakini waswahili wanasema safari ni hatua, tunaamini kwa mashirikiano ya pamoja tutafikia mbali zaidi huko siku za mbele.

Mhe. Naibu Spika, sasa napenda kutoa maoni ya Kamati kwa kufanya marekebisho mbali mbali katika mswada huu muhimu katika Maendeleo ya Majimbo yetu na Taifa kwa ujumla. Mhe. Naibu Spika, marekebisho hayo yaliyofanywa katika mswada huu yamegawika kama hivi ifuatavyo:-

1. Marekebisho ya mswada kwa kubadilisha maneno ili yaendane na maana halisi ya mswada. Kwa mfano, katika Sehemu ya Kwanza ya mswada, Kifungu cha 2 katika tafsiri ya maneno, maneno "Katibu Mkuu" na "Mkurugenzi" tafsiri zao zimebadilishwa na kuandikwa upya.

2. Marekebisho ya mswada kwa kuongeza vifungu kwa lengo la kuviweka vizuri vifungu hivyo pamoja na mswada kwa ujumla. Kwa mfano, Sehemu ya Pili, Ukurasa wa 29 wa mswada kimeongezwa kifungu cha 3(3) ambacho kinaeleza dhamana ya Mkurugenzi katika utekelezaji wa shughuli za mfuko.

3. Marekebisho ya mswada kwa kurekebisha maneno ili yalete maana halisi iliyokusudiwa. Kwa mfano, Sehemu ya Pili, ukurasa wa 29, kifungu cha 7(1) neno "Risiti" lisomeke " Mapato yote"
4. Marekebisho ya mswada kwa kufuta baadhi ya vifungu vya mswada kwa kuonekena kutokuwa na umuhimu na pia kutoathiri kwa kutolewa kwake. Mfano, Sehemu ya Saba, ukurasa wa 37, kifungu 30(3) kimefutwa.

5. Marekebisho ya irabu kwa baadhi ya maneno ili yaende sawa na mpangilio wa maneno mengine. Kwa mfano, Sehemu ya Kwanza, neno "Ola" limebadilishwa na kuwa "la**"**

Mhe Naibu Spika, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kujaribu kuyapitia sana yale marekebisho tuliyoyasambaza kwa sababu haya ndio yaliyotoa hasa ni namna gani tuliweza kufanya marekebisho katika mswada ule. Lakini zaidi katika kile kifungu cha 9 kuna suala zima la uteuzi wa Wajumbe wa Kamati tumempa mamlaka moja kwa moja Mhe. Mwakilishi kwamba yeye ndio aweze kuwateuwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo katika jimbo lake, ili kuhakikisha kwamba wanasimamia maendeleo na ile ahadi ambayo aliyoiweka Mhe. Mwakilishi katika jimbo lake.

Mhe Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niwashukuru sana, sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Waziri katika Ofisi yake kwa kutuletea mswaada huu muhimu kwa maendeleo yetu. Pia kwa heshima zote tunaomba utupelekee shukrani zetu za dhati kwa Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi kwa kusikia kilio chetu cha kutaka kuleta maendeleo katika majimbo yetu na kutukubalia kuanzisha mfuko huu wa maendeleo wa jimbo.

Mhe. Naibu Spika, tunamuahidi kwamba tutajitahidi kuwasimamia watu wetu tutakaowakabidhi fedha hizo ili wazitumie vizuri na pia tunaahidi kumbukumbu zote za matumizi tutaziwasilisha Serikalini. Pia nawaomba waheshimiwa wenzangu kujitahidi kusimamia vizuri matumizi ya fedha hizi kwani tukifanya vizuri basi naamini Serikali itaongeza fungu hilo kila mwaka, pia tunawatahadharisha wajumbe wenzangu kwamba kuna kifungu katika sheria hii kwamba jimbo lolote litakaloshindwa kufanya marejesho ya matumizi ya fedha hizi basi hazitoweza kupatiwa fedha nyengine hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura kwa kunituma kuwawakilisha katika chombo hiki kwa maslahi ya Wazanzibari wote. Baada ya maelezo hayo, naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza kwa makini na kwa niaba ya Kamati yangu naomba kuunga mkono mswada huu kwa kuupitisha ili iwe sheria itakayowaletea maendeleo wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kama kawaida kwa kuwa na mimi nimefanya mambo mawili kwa pamoja, kwa vile ni Mwenyekiti wa Kamati pia nilikuwa naomba uniruhusu nitoe maelezo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa umeonesha bashasha inaonesha umenikubalia.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nataka niwaombe sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mswada huu tuuchangie sana, tuishauri serikali kwa sababu waheshimiwa kwa kweli mswada huu tukiupitisha basi kile kilio chetu cha muda mrefu kitakuwa kimeanza kutatuka.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu mimi mwenzetu nilipata kwenda kuwaona wenzetu walivyofaidika na fedha hizi. Kwa kweli washirika wa maendeleo walikasirika sana wenzetu wa Bunge la Kenya walipoanzisha huu mfuko wakasema kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wao kazi yao kusimamia matumizi ya fedha za serikali. Lakini leo inakuwaje kwamba wawakilishi hao hao waje kuwa ndio watumizi wa fedha za serikali. Je, wao watasimamiwa na nani?

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwathibitishie kwamba fedha hizo Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuja majimboni kuja kuzisimamia na matumizi yake yatakuwa hayana matatizo. Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikajaribu kuwaasa waheshimiwa wenzangu kwamba fedha hizi tuzitumie vizuri, kwani fedha hizi hatutozitumia sisi kama wawakilishi. Lakini fedha hizi tutawakabidhi kamati zetu za maendeleo kwa ajili ya kuleta maendeleo katika majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, naamini tukiweza kufanya vizuri waheshimiwa basi ile asilimia 2 ya mapato yote ya nchi kwamba wanapewa Wabunge kwa ajili ya kuleta maendeleo katika majimbo yao, basi naamini kuna siku serikali itasema hebu tujipunguzie mzigo wa kuweza kupelekewa malalamiko kwa wananchi kwamba huduma za maendeleo majimboni mwao zinadhoofika. Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo majukumu yale watatukabidhi sisi Waheshimiwa Wawakilishi ili kuweza kuhakikisha kwamba serikali kuu inafanya majukumu yake makubwa, kwa kushirikiana na halmashauri zetu pamoja na Baraza la Manispaa tunaweza kusimamia maendeleo katika majimbo yetu madogo madogo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema sisi leo kwa kuanzia serikali yetu itatupa shilingi milioni 10 kwa mwaka mzima, ukifanya mahesabu ya haraka haraka milioni 10 ni sawa sawa na shilingi 900,000/= kwa kila mwenzi. Lakini Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema wenzetu wa Kenya wanapewa shilingi milioni 20 kwa mwezi kwa ajili ya maendeleo ya majimbo yao. Na sisi tukiweza kuzitumia vizuri naamini itafika siku serikali yetu itatukabidhi shilingi milioni 20 vile vile kwa mwezi, sio kwa mwaka ili tuweze kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naamini wananchi watatuunga mkono katika mswada huu na sasa hivi kila jimbo ambalo hajaunda kamati zao za maendeleo, basi tunawaomba wakaanzishe kamati za maendeleo kwa sababu fedha hizi zinakuja na sheria, kama hujaanzisha kamati ya maendeleo, basi fedha hizi huwezi kuzitumia. Mhe. Naibu Spika, naamini Mhe. Waziri kwa kweli yuko makini sana kuipitisha hii sheria yeye yuko tayari kuweza kutoa hizi fedha kwa ajili ya kuleta maendeleo katika jimbo letu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naendeleo tena kumshukuru Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri katika ofisi yake. Na pia namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuweza kutukubalia kutupa fedha hizi kwa ajili ya maendeleo ya majimbo yetu. Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kuwa ni kiranja wa kuchangia mswada huu wa maendeleo ya jimbo. Kwanza nianze kwa kuipongeza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuleta mswada huu ambao kwa kima fulani utatusaidia utendaji wa shughuli zetu katika majimbo yetu.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kila mwakilishi hususan sisi *backbenchers* ni mawaziri wa wizara zote za serikali katika majimbo yetu. Mimi ni Waziri wa Afya, kigari changu ni chakuchukulia wagonjwa, mimi ni Waziri wa Elimu, mimi ni Waziri wa Biashara, mimi ni Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mimi ni Waziri katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, mimi ni Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na wizara zote kwa ujumla. Mhe. Naibu Spika, katika wizara hizo zaidi ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi humu sisi ni mawaziri ambao tunatoa huduma kwa wingi. Na kile kidogo tunachotoa sisi wenyewe ukilegea basi hupati kijio kwako. (*Makofi*).

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mswada huu utaweza kidogo kujisukuma katika utendaji wetu. Hivyo basi, ningewaomba wawakilishi wenzangu mfuko huu pengine kesho tupewe kabisa tuutumie kwa sababu ile iliyokusudiwa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hapa tumezingatiwa sisi peke yetu watu wa majimbo 50, lakini serikali katika utendaji wake kwa mfumo wa siku hizi basi kila pahala wanawake wanaingizwa katika hesabu. Humu kwenye Baraza wanawake wana asilimia maalum wanaingia katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, mfuko huu wanawake hawajahisabiwa kwa hivyo ningeiomba serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 na wao wapewe asilimia fulani ili kile watakachopata wao na tutakachokipata sisi tuungane kuendeleza majimbo yetu. Ingawaje hao wenzetu hawana majimbo, lakini tuna mifumo miwili tofauti kwa mfumo wa chama kimoja wao ni wawakilishi wa wilaya zao, na wengine ni wawakilishi pengine wa mikoa yao. Kwa hivyo, pengine wao kama watafanya kazi wana jukumu kubwa zaidi kuliko sisi pindipo kama watafanya kazi vizuri. Kwa hivyo, ningeiomba serikali kama wanavyofikiriwa katika mambo mengine na hapa na wao wafikiriwe.

Mhe. Naibu Spika, mfuko huu leo uko uwanjani unajadiliwa na Waheshimiwa Wawakilishi tunaonekana moja kwa moja nini tunachokizungumza. Kwa hivyo, mtu aliyekuwepo katika kijiji changu leo anajua tunajadili nini, mtu aliyekuwepo Vitongoji anajua leo kunasemwa nini, mtu aliyekuwepo Mgogoni, Mkanyageni, Muyuni na kwengineko wanajua kwamba leo tunajadili nini. Kwa hivyo, tuone kwamba hili jambo linawagusa wananchi moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya mfuko huu ilikuwa hatulali kwa wananchi, je leo wanasikia kwamba tunajadili mfuko ambao ni kwa ajili yao. Kwa hivyo, mfuko huu ni lazima tuutumie vizuri ili kuondoa matatizo kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mimi ni mmoja ambaye tumeujadili mfuko huu hapo awali hivyo sina mchango mkubwa isipokuwa hayo machache niliyosema, hivyo tutatayarisha kamati zetu ambazo zitaweza kutuunga mkono katika kuendeleza haya ambayo serikali imekusudia. Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, mimi siungi mkono asilimia 102 kama watu wanavyounga, lakini naunga mkono mswada asilimia 100, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi sina budi kwa kukushukuru kuweza kunipatia nafasi nikaweza kutoa mchango wangu katika suala zima linalotukabili mbele yetu la kuanzisha kwa mfuko wa maendeleo wa jimbo. Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulifikiria suala hili muhimu ambalo tulilokuwa tukiliomba kwa muda mrefu. Leo ni furaha yetu wawakilishi wote tuliopo hapa ndani, na hatuna budi suala hili kuliunga mkono mia juu ya mia ili kuona jitihada za serikali baada ya maombi ya muda mrefu. Kwa hivyo, na mimi kwa upande wangu nasema naunga mkono suala hili la mfuko wa maendeleo wa jimbo mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli leo tuko katika furaha kubwa sana kusikia kwamba serikali imeitikia wito wetu wa maombi ya muda mrefu. Suala hili ni muhimu sana katika jimbo letu kwa sababu na sisi wananchi wetu wana matatizo mengi hivyo na wao wanahitaji kuona kiasi gani uwakilishi wanasimamia matatizo katika jimbo ambazo hizi ni kero za muda mrefu katika majimbo yetu. Mhe. Naibu Spika, katika majimbo yetu tuna kero ambazo wananchi wetu na wao wanataka kero hizo ziweze kuondoka mara moja.

Kwa hivyo, baada ya kupata kero hizi na sisi kupeleka maombi yetu kwamba tunahitaji mfuko wa maendeleo ili uweze kusaidia jimbo, leo alhamdulilah tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba serikali imeitikia maombi yetu na sisi tunasema, serikali itakapotukabidhi fedha hizi tutafanya kila bidii kuweza kufuatana na sheria ya mfuko huu. Kwa sababu huu mfuko una sheria zake, una kanuni zake na chini ya Mkurugenzi wa mfuko huu ni lazima taarifa zote za maendeleo ni lazima fedha hizi zijuulikane nini kinafanywa. Mimi naamini katika kila jimbo na kila mwakilishi katika majimbo yetu yote 50 matatizo yapo ya kutosha. Hii ni kwa kuanzia kwa kuiomba serikali hicho kidogo, lakini naamini serikali baadae inajua itakapoona faida inapatikana katika kila jimbo, basi serikali itaweza kuongeza mfuko huu uwe mkubwa zaidi. Kwa sababu ili kupunguza kero na manung'uniko ya wananchi wetu katika majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwaambie wenzetu fedha tutapewa, lakini tuna wajibu wa kuisimamia fedha hii, hivyo ni lazima tuunde kamati za maendeleo ya jimbo. Kamati hizi ndizo zitakazoweza kusimamia pamoja na yeye mwenyewe mwakilishi akiwa ndiye mwenyekiti wa suala hilo, yeye ndiye atakayechagua katibu na wajumbe ambao watasimamia kamati ya maendeleo. Mwakilishi hana haja yeye kutaka kutumia pesa ile, yeye anaomba pesa hiyo kila ikipatikana aipeleke katika jimbo lake ili kamati ya maendeleo iweze kupunguza kero ambazo tunazo katika majimbo yetu. Kwa hivyo, tuna wajibu wa kusimamia fedha hii itumike vizuri na ripoti tuweze kupeleka ya fedha hii kuona kwamba aina gani ya miradi tuliyoichagua.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwaombe wawakilishi wenzangu tuangalie ni aina gani ya miradi ambayo tunataka kufanya katika majimbo yetu. *Priority* tutoe haidhuru tutachagua watu mbali mbali wakiwemo wajumbe mbali mbali tunahitaji kuwa na mashekha katika suala hili, tutawashirikisha watu mbali mbali katika kamati zetu za maendeleo, kuna jamii, taasisi mbali mbali, walemavu kama sheria ilivyozungumza humu ndani na sisi watu hawa ambao wamezungumzwa katika sheria hii ni lazima tuwashirikishe wote. Kwa hivyo, naomba tuhakikishe kwamba hili suala ni muhimu na tukilipata tuliendeleze tuchague miradi iliyokuwa muhimu ya mwanzo ili tuweze kufanikisha kama ni mradi mmoja au miradi miwili tuliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri mfuko huu utatupa chanzo na kwa sababu ya Serikali yetu tuliyonayo ya Umoja wa Kitaifa tutaweza kuwapunguzia mzigo, kwani mzigo mkubwa wa serikali hii ni matatizo ya wananchi. Mhe. Naibu

Spika, matatizo ya nyuma tunajua kwamba serikali itajitahidi kupunguza mfumko wa bei, lakini pamoja na mfumko wa bei wananchi wanataka kuona maendeleo katika majimbo yao. Kwa hivyo, serikali inapiga huku na huku, sisi tutasaidia upande wetu katika kupunguza kero kwenye majimbo yetu. Na upande wa pili serikali ijaribu kufikiria suala zima la mfumko wa bei ambao hali ngumu za kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri kwa upande wetu wawakilishi tutaweza kusimamia vizuri haki hii iweze kutolewa na kila mmoja kati yetu ni lazima watu wetu tuwaarifu nini serikali imekusudia kwenye suala hili, tuwajuilishe, tuweke vikao, tuweke mikutano tuwaarifu watu wetu hii ni kwa wote hakuna siri katika suala hili. Mhe. Naibu Spika, nawaomba waheshimiwa kila mmoja katika jimbo lake ajitahidi kuita watu wake awaeleze nini madhumuni ya mfuko huu wa maendeleo katika jimbo, ni katika kutatua matatizo ambayo ni kero za wananchi za muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza serikali kwa mara ya mwanzo kuweza kulifikiria suala hili na kuweza kutusaidia sisi wawakilishi kwa sababu kama si mfuko huu ingelitubidi sisi kile ambacho serikali inatupa tutoe katika mfuko wetu ili kuwasaidia wananchi. Na sisi kama ni wawakilishi wananchi wetu wanatuona kama sisi wawakilishi ndio kama serikali, yaani sisi tuna kila kitu kwa shughuli zote ikiwa kwa furaha au kwa mazishi, mwakilishi yeye ndiye nambari moja katika kuchangia. Kwa hivyo, tunahitaji kuweka maendeleo mazuri ya maji, maendeleo mazuri ya barabara zetu na maendeleo yote ambayo kila mwananchi anastahiki apate inakuwa mwakilishi yeye ndio kigezo kikubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, na wao wanaelewa kwamba japokuwa hatuna kitu lakini mtu wa mwanzo wa kuambiwa ni mwakilishi. Kwa hivyo, tulichonacho tunajaribu kusaidia katika kuendeleza, lakini pia tunaunga mkono serikali kutusaidia sisi wawakilishi ili kuweza kufanikisha maendeleo ya jimbo letu. Kwa hivyo, mimi naipongeza sana serikali kwa kuweza kulifikiria suala hili na kuliona umuhimu wake na kuangalia wananchi kwa sababu serikali inatoa inatupa sisi, na sisi tufanye uaminifu kwenye fedha hii ambayo serikali inatupa kwa ajili ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache yanatosha kuyapa nguvu maelezo haya, ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana mimi sitakuwa na mchango mkubwa, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai na uzima na kuweza kufika katika kikao hiki. Huu mswada ni mzuri napenda kutoa mchango wangu kwamba mwanzo ilitajwa Kamati ya Maendeleo ya Jimbo, mimi sina tatizo na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo. Lakini sehemu ya tano utekelezaji wa miradi hapa ndio penye masuala yangu, kutakuwa na Kamati ya Utekelezaji wa Miradi kwa utekelezaji wa miradi chini ya sheria hii. Kwa hivyo, mimi namuuliza Mhe. Waziri kwamba kamati hii inayoitwa Kamati ya Utekelezaji Miradi ni ile ile Kamati ya Maendeleo ya Jimbo au ni kamati nyengine. Kama ni kamati nyengine basi mimi naona ni *duplication* na italeta matatizo makubwa.

Kwa sababu fedha zinazozungumzwa na haja iliyoko majimboni ni kidogo sana, sasa kuziundia kamati nyingi zote zitamalizwa na hizi kamati tu kabla hata hazijenda huko jimboni. Kwa hivyo, kama Kamati hii ya Utekelezaji wa Miradi ni nyingine kuliko ile kamati ya Maendeleo ya Jimbo nahisi kuwepo kwake ni kikwazo katika utekelezaji wa hii miradi kutokana na hali halisi ilivyo katika majimbo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri wakati wa majumuisho aje anitolee ufafanuzi. Mimi nahisi kwamba ile ile Kamati ya Maendeleo ya Jimbo, ikateua kamati ndogo ndani yake ya ufuatiliaji wa miradi, lakini kufanya kamati mpya na fedha zenyewe ni hizi zinazotolewa, kwa kweli kutakuwa na matatizo. Huo ndio mchango wangu mkuu.

Halafu kifungu cha 21 kuna kamati nyengine inayoitwa Kamati ya Manunuzi. Sasa naona kamati zinakuwa nyingi, kwa hivyo, hebu Mhe. Waziri aje atueleze. Kwa sababu hili jambo sio kuwa sana hata hivyo, kwanza fedha zenyewe zinatolewa mwaka hadi mwaka halafu zinaanzia na shilingi milioni 10, sasa kuziundia kamati nyingi na watu wetu tunawajua kila akiitwa katika kamati inawezekana yeye apate posho na pesa zenyewe ni hizi. Kwa hivyo, mimi nafikiri kamati ile ile ya maendeleo ingelitawala mambo yote hayo, mpaka hapo baadae itapoonekana kwamba sasa Mfuko umeshafikia kiwango cha kutosheleza na miradi hii inakua, lakini kwa kuunda kamati hizi kwa kweli kuna matatizo.

Mhe.Naibu Spika, baada ya hayo, mimi naunga mkono hoja na nadhani ni mswada mzuri wa kupitishwa, lakini hayo niliyoyasema mawili ya kamati nyingi yaweze kuzingatiwa. Kwa sababu hii ni ile wataalamu wanaoita urasimu. Kwa mfano Mfuko wa Wabunge uko katika halmashauri, ikishaamua kamati iliyofanywa ndani ya Halmashauri,

ndio fainali, unakwenda moja kwa moja utekelezaji, hakuna kamati nyengine ya utekelezaji, hakuna kamati nyengine ya nini. Sasa tungeangalia uzoefu uliopo kwa Mfuko wa Wabunge ambao tayari umeshaanza kazi.

Kwa hivyo, mimi nahisi kuwa na Kamati nyengine ya Utekelezaji na Kamati ya Manunuzi kwa kweli zitakuwa ni kikwazo cha utekelezaji wa hii miradi, au itakuwa fedha zenyewe zinatumika kwa kamati tu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru mchana huu, kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwa mswada ambao ni mzuri kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe.Naibu Spika, na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kusikiliza matakwa ya wananchi, pale alipoamua kuandaa mswada huu na kutuletea kwa ajili ya kuujadili na hatimae kuupitisha kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe.Naibu Spika, kimsingi mswada huu wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ni mzuri, na mimi naunga mkono mswada huu. Ni mzuri kwa sababu dhana nzima ya mswada huu utashirikisha wananchi moja moja katika majimbo yetu. Sasa mtazamo wangu mswada huu Mhe. Naibu Spika, ungekwenda sambamba na uanzishwaji wa Ofisi za Wawakilishi, Mfuko wa Jimbo mwenyekiti atakuwa Mhe. Mwakilishi, lakini hadi hii leo hatujawa na utaratibu wa kuanzishwa kwa Ofisi za Wawakilishi.

Sasa tukiangalia Mhe. Naibu Spika, Baraza hili zamani tunagaiwa bendera, bendera ambazo lengo lake ni kuwekwa kwenye ofisi za wawakilishi. Lakini vile vile kama tungekuwa na ofisi za wawakilishi mbali ya kupewa bendera ambazo tumepewa na serikali hii, lakini uratibu wa shughuli hizi za Mfuko zingekuwa zinajulikana wapi zinafanyika, na hivyo Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wangekuwa ni rahisi zaidi kwao kuwapata wawakilishi badala ya kuwatafuta majimboni siku hadi siku.

Kwa hivyo, mimi ushauri wangu nimuombe Mhe. Waziri pamoja na nia safi ya kuanzisha Mfuko huu, lakini kwa kuanzia angalau angewataka Waheshimiwa Wawakilishi basi wakatafuta sehemu japo za kuanzia, hata kama za kuazima wakaweza kuweka bendera na ofisi za wawakilishi ili wananchi wajue wapi pa kupeleka mahitajio yao chini ya Mfuko huu.

Wasi wasi wangu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tunaweza tukawa na Mfuko, lakini uratibu wa Mfuko huu ukawa haujulikani, kwa sababu ya ukosefu wa ofisi ambayo Waheshimiwa Wawakilishi, na kamati zao wangefanyia kazi.

Mhe.Naibu Spika, lakini uzuri wa Mfuko huu nitoe tahadhari kwa Waheshimiwa wenzangu, kwamba hii ni ndoana, ndoana unaweza ukaimeza ukapata salama, na unaweza kuimeza ukapata majeraha. Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba, tuwe makini sana na Mfuko huu, kwa sababu serikali muda mrefu tumekuwa tukiilaumu sasa isije ikawa na sisi tunalaumiwa na serikali kwamba tumepewa fedha kwa ajili ya wananchi lakini hatimae Wawakilishi wanafuja.

Jambo hili kwa sababu litasimamiwa na kamati na Ofisi ya *CAG*, basi *CAG* atapokagua fedha hizi, si vyema kabisa Mhe. Naibu Spika, kuonekana Mwakilishi na kamati yake amechangia katika kupoteza fedha za umma, na itakuwa ni doa kubwa. Sasa ile dhana nzima ya usimamizi wa serikali itakuwa haifanyi kazi, kwa sababu wawakilishi watakuwa wamechangia katika kufuja fedha za umma. Kwa hivyo, Mhe.Naibu Spika, mimi nitoe tahadhari na nasaha kwa wawakilishi wenzangu kwamba, kama kuna jambo la umakini basi hapa umakini uongezeke zaidi, ili iondoshwe aibu ya dhana nzima ya upotevu wa fedha za umma chini ya mikono ya Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe.Naibu Spika, jambo jengine ambalo ningesema kwa ufupi, ni suala zima la uteuzi wa kamati. Mfuko huu Kamati ya Maendeleo itakuwa chini ya mwakilishi kama mwenyekiti, lakini imezingatia suala zima la kuwatambua madiwani, kwamba madiwani pia itakuwa ni sehemu ya wajumbe wa Kamati ya Maendeleo pamoja na mlemavu.

Mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwamba ametambua kuwepo umuhimu wa walemavu na amewatia kwenye kamati hii, jambo ambalo limetoa ushirikiano na litatoa picha nzuri kwa jamii.

Sambamba na hilo Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri pia amependekeza kuwa, Wajumbe wa Kamati hii wawe na elimu angalau isiyopungua sekondari kwa maana ya *Form IV*. Pia Mhe. Naibu Spika, nipongeze kwamba ni jambo zuri kwa sababu hapa tunazungumza fedha na miradi, kwa hivyo kuwachagua wajumbe ambao wana ufahamu kidogo wa kitaaluma ni jambo zuri ambalo la ujasiri, na Mhe. Waziri nampongeza na naomba Waheshimiwa

Wajumbe hili pia tuzingatie, kwamba kuna umuhimu sasa kwa suala hili la maendeleo, ambalo linahusisha fedha na mipango ya jimbo, lazima tuwapate watu wenye uwezo ambao watatusaidia sisi wawakilishi kutushauri, ili fedha hizi zifikie malengo yaliyotarajiwa.

Mhe.Naibu Spika, kifungu cha 16(3) Mhe. Waziri amesema kwamba miradi yote itakuwa ya maendeleo, na inaweza kuhusisha gharama za upembuzi yakinifu, upangaji na michoro.

Mhe.Naibu Spika, mimi nina wasi wasi, kwamba fedha hii pengine shilingi milioni kumi, gharama za upembuzi yakinifu, michoro na upangaji zitoke humo humo, nadhani hii sasa itakuwa ni fedha za uchambuzi wa miradi tu. Fedha hizi ningemshauri Mhe. Waziri kwamba gharama zote za upembuzi yakinifu, upangaji na michoro zingetafutiwa namna ya kupatikana fedha nyengine, vyenginevyo fedha hiyo wasi wasi wangu wataalamu wa majimbo watatumia kwa ajili ya vikao na kisingizio cha upembuzi yakinifu.

Kwa msingi huo, mimi ningemshauri Mhe. Waziri hapa, angalau akaweka asilimia fulani, kwamba asilimia fulani ya fedha hizi isikiukwe isizidi hapo iwe ndio fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya upembuzi yakinifu, upangaji na michoro, vyenginevyo tukiacha wazi hivi hivi, basi wataalamu hawa wa jimbo wanaweza kutumia fedha hizi kwa ajili ya michoro ambayo malengo ya mradi huu yatakuwa hayakufikiwa.

Mhe.Naibu Spika, jambo jengine ambalo ningelisema ni kifungu cha 27. Mhe.Waziri amependekeza hapa kwamba gharama za uendeshaji wa Mfuko, matumizi ya kuonesha shughuli za Mfuko, zinatokana na fungu la bajeti ya Wizara. Swali langu, nani atakayeratibu uhalali wa matumizi haya? Kwa sababu fedha za Mfuko zinakwenda jimboni, lakini uendeshaji wake uko chini ya wizara, nani atakayedhibiti matumizi ya fedha hizi? Je, Kamati ya Jimbo itashirikishwa kujua kwamba fedha zilizotolewa na wizara kwa ajili ya uendeshaji ni ngapi na uhalali wake.

Nasema hivyo kwa sababu wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali, anaweza akapata mgongano hapa, kwamba fedha nyengine zimetumika wizarani na nyengine zimetumika jimboni jambo ambalo lingekuwa sio zuri. Mhe. Waziri nimshauri kwamba, katika utungaji wa kanuni hii ungewekwa utaratibu wa wazi ili watu wa jimbo nao wakajua kwamba uendeshaji wa fedha hizi ukoje.

Lakini kifungu cha 30(2) kuna makosa na adhabu. Mhe. Naibu Spika, ni vyema makosa na adhabu yakawepo kwa matumizi ambayo yatafuja fedha hizi za maendeleo ya jimbo. Lakini nimeshtuka kidogo kwamba fedha zenyewe zinaweza kuwa shilingi milioni kumi lakini adhabu yake miaka kumi jela, maana yake hii sheria mkazo wake kwa kweli ni wa hali ya juu. Kuna sheria tulipitisha hapa Mhe.Naibu Spika, ni fedha nyingi angalau shilingi milioni mbili au tatu, lakini hapa fedha ndogo shilingi milioni kumi sasa hizo shilingi milioni kumi na jela miaka kumi. Sasa naomba tuangalie, ni vyema kwa sababu wawakilishi watalindwa hapa, lakini fedha hii itasimamiwa sio na mwakilishi tu, itasimamiwa na watendaji wetu ambao taaluma yao, uwezo wao ni mdogo. Sasa kuweka adhabu ya miaka kumi jela kwa shilingi milioni kumi kidogo Mhe. Waziri naomba tuzingatie, kwa sababu watendaji wetu uwezo wao mdogo tunaweza kuwafunga watu wengi kwa sababu taaluma yetu ni ndogo ya jimbo na fedha ndogo, lakini adhabu kubwa sana. Ningekuomba Mhe. Waziri kwa busara zako sheria ya adhabu kidogo tuipunguze.

Sisemi hivyo kwa sababu labda keshokutwa atakuwa mkosa mwakilishi asifungwe, mimi nasema afungwe akiharibu, lakini tuangalie hii adhabu kwa sababu naona ni kubwa sana hasa kwa watendaji wetu walioko chini.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi mimi mswada huu naunga mkono, lakini niwakumbushe wenzangu kwamba hiki ni chambo, na tukikitumia vibaya kitatumaliza. Ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi niseme chochote kuhusiana na mswada huu muhimu uliopo mbele yetu.

Pili naomba niitumie fursa hii nitoe mkono wa pole kutokana na kifo cha Marehemu Salum Amour Mtondoo, swahibu wangu na jirani yangu katika Baraza kwa safari aliyokwenda ya haki, naomba Mwenyezi Mungu aijaalie familia yake iwe na subira na wananchi wote wa Jimbo la Bububu wawe na subira kwa kuondokewa na kipenzi chao.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niseme kwamba msingi na chimbuko la kuwepo kwa mswada huu wa *CDF* umetokana na uzeofu wa wenzetu ambao katika mabunge mengine wameanzisha Mifuko kama hii. Na msingi wa

Mfuko kama huu ni kutokana na hoja ya mgawanyo wa rasilimali za nchi katika bajeti. Hoja ilikuja kwamba, kila mwaka serikali inapitisha bajeti lakini bajeti hiyo ukiacha mbali matumizi ya serikali katika matumizi ya maendeleo yanajikita katika maeneo fulani ya nchi na maeneo mengine ya nchi hayafaidiki na keki ya taifa. Sasa baada ya utafiti, wenzetu wakaona basi njia nzuri ambayo inaweza ikapelekea keki ya taifa ikaenea nchi nzima ni kupitia Mfuko wa *CDF*.

Tafiti zinaonesha kwa wenzetu walioanzisha Mfuko huu kama Kenya, kwamba ni kweli kuwa kabla ya kuwepo kwa Mfuko huu hali ya maendeleo ya kijamii ilivyokuwa, na baada ya kuanzisha Mfuko huu namna ambavyo majimbo mbali mbali bila ya kujali ukubwa wake, bila ya kujali utajiri wake, na bila ya kujali mambo mengine, kwamba baada ya kuanzishwa Mfuko huu mambo mbali mbali ya kijamii yamegusa wananchi, na kila mwaka wananchi kwa njia moja au nyengine wanafaidika na bajeti ya nchi yao.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio hoja ya msingi, na sisi tukafika pahala tukaona kwamba ni wakati sasa tuanzishe Mfuko huu, hasa kutokana na hoja ya mfumo wa uandaaji wa bajeti. Kwa sababu lengo la serikali kila mwaka kuandaa bajeti ni namna inavyoweza kutumia fedha za umma katika kufanya mambo yake ya kimaendeleo. Sasa ni bahati mbaya kwamba, namna inavyowashirikisha wananchi au namna wananchi wanavyoguswa au wanavyofaidika, au wanavyoshiriki katika kuandaa bajeti hapa ndio Mhe. Naibu Spika, penye matatizo.

Kwa hivyo, hoja nyengine ya msingi ni kwamba, namna wananchi wanavyoweza kushiriki katika uandaaji wa Bajeti ya Serikali. Sasa wanaounga mkono Mifuko kama hii, wanaunga mkono kwa hoja ya mafanikio yanayopatikana baada ya kuanzishwa Mfuko huu. Lakini wako wengine wanapinga katika mabunge yetu, hasa sheria hizi zinapopitishwa huwa kuna makundi ya wanajamii, au makundi hata ya wabunge wenyewe hupinga.

Msingi wao mkubwa Mhe.Naibu Spika wa kupinga, ni kutokana na hoja ya kikatiba na hoja ya kisheria. Wao hujielekeza kwamba Mifuko kama hii inakwenda kinyume na katiba, kwa sababu majukumu ya serikali yameelezwa wazi katika katiba, majukumu ya mabunge, ama majukumu ya mbunge au mwakilishi nayo pia yameelezwa wazi katika katiba, kwamba bunge kazi yake ni kutekeleza shughuli, lakini vile vile Mabunge haya ama Mabaraza ya Wawakilishi kazi yake ni kusimamia serikali. Sasa inapofika pahala na Baraza la Wawakilishi, Bunge au Mwakilishi anapotaka kufanya kazi za kiserikali, hapa ndio tatizo hutokea kwamba nani anafanya nini na nani anamsimamia nani. Kwa hivyo, hiyo ndio hoja Mhe.Naibu Spika, ya msingi.

Sasa mimi naomba nikumbushe tu, kwamba kadiri tutakavyokubaliana, kitu kimoja ni cha msingi sana tukumbuke. Kwamba fedha itakayotolewa hii Mhe. Naibu Spika, ni fedha ya umma, ni muhimu tukalikumbuka hilo, ni fedha ile ile ya umma inayokusanywa na serikali, ni fedha ile ile inayopitia katika mfumo wa kawaida wa kibajeti. Kwa msingi huo, kwa sababu ni fedha ya umma, na hata usimamizi wake basi utapaswa usimamiwe na sheria zinazoongoza matumizi ya fedha za umma.

Kuna sheria ile ya mwaka 2005, kuna sheria ya manunuzi pamoja na kanuni zake, hizi ndio sheria ambazo kwa sasa tunazo na ndizo ambazo zinazoongoza na zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Kwa hivyo, tukumbuke kwamba fedha hizi zitakapotoka, tukumbuke kwamba hatimae taratibu zetu zinatueleza kuwa serikali inapotoa fedha kitendo kinachofuatia ni kitendo cha ukaguzi. Tukumbuke kwamba tutakapopewa fedha hizi katika majimbo yetu baadae mkaguzi atalazimika kupita majimboni, na kufanya ukaguzi wa namna fedha zilivyotumika.

Baada ya kufanya ukaguzi huo ataandaa ripoti, kwa hiyo kama kuna jimbo A na B na C limekiuka taratibu itaandikwa katika Ripoti ya Mdhibiti, na ripoti hiyo hatimae itarudi katika Baraza hili kuja kuangalia namna gani Mwakilishi A, B na C walivyokiuka sheria ya matumizi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba nikumbushe hilo kwamba kuna sheria zile zinazoongoza tusisahau. Ingawa kwa kiwango hiki vile vile kuna utaratibu kwamba, katika kiwango ambacho kitaanzia kwa shilingi milioni kumi, basi vile vile kuna taratibu zake naomba niwakumbushe wenzangu kuwa tusisahau hilo. Mhe.Naibu Spika, vile vile na mimi niungane na wenzangu hapa kwamba uwepo wa kamati nyingi kwa kweli utapelekea matatizo. Ni ukweli Mhe. Naibu Spika, watu watakaoteuliwa kuingia katika kamati hizi, basi kwa namna moja au nyengine watajenga matumaini. Kwa hivyo, hofu yangu ni kwamba watakaodai chejio, watakaodai nauli na vitu vyengine, hizo pesa zote zitaishia katika utaratibu huo au vyenginevyo, kama ikiwa si pesa hizo basi Mwakilishi atalazimika sasa atafute nyengine za kuwalipa posho za vikao pamoja na usafiri.

Mhe.Naibu Spika, mimi niunge mkono kwamba, tujaribu kuangalia, ikiwezekana tuangalie aina moja tu ya kamati, kwa sababu fedha zenyewe ni kidogo sana. Sasa hofu yangu ni kwamba pengine huenda ikaishia huko na hili Mhe. Naibu Spika, nasema tayari lishaanza kutokea katika majimbo. Sitaki niseme wapi na wapi, lakini tayari ishatokea kwamba wengine nusu na robo ya fedha ikaishia kwenye mambo ya kugharamia safari na vitu vyengine.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi naamini kwamba fedha hizi zitakuwa ni sehemu ya ukombozi na zitatupunguzia mzigo mzito wawakilishi katika majimbo yetu, na kwa kweli ni kama alivyosema Mhe. Mohammed Haji Khalid kwamba sisi wawakilishi katika majimbo, kwa kweli ni mawaziri tusiokuwa na wizara maalum katika majimbo yetu. Kwa kiasi kikubwa sana tutapunguziwa mzigo, naomba niipongeze serikali kwa kuleta sheria hii na naomba pamoja na yote, lakini tuangalie ili badala ya kuwa ni faida, na badala ya kutupa faida, suala hili lisije likageuka, tukajikuta wawakilishi tuko katika hatari na kupoteza imani kwa jamii.

Mhe.Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kutujaalia asubuhi hii ya leo kuwepo hapa tukiwa katika hali ya salama na tukiwa wazima wa afya.

Lakini la pili, nachukua nafasi ya kuwapa pole wenzetu wa Bububu kwa kifo cha ndugu yetu Mwakilishi mwenzetu, Mhe. Salum Amour Mussa (Mtondoo) Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema **AMIN.**

Pia nachukua nafasi hii, kumpongeza Mhe. Mohammedraza kuwa nae katika Baraza letu hili, tunaamini kwamba tutashirikiana nae vyema na kumpa mashirikiano ya hali ya juu kabisa. Nasema kwamba ahsante sana.

Baada ya hapo, napenda kuuchangia mswada huu kwa ujumla wake. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba naipongeza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuletea mswada huu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Ofisi hii imewashusha pumzi kiasi fulani wawakilishi wa Zanzibar, niseme kwamba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imewaletea Waheshimiwa Wawakilishi *ICU*. Kwa kweli hali ya wawakilishi wa Zanzibar ilikuwa ni ngumu sana majimboni, kutokana na mahitaji mbali mbali ambayo walikuwa wanahitajiwa na wananchi wao, huku wananchi wakiamini kwa asilimia mia moja kwamba wawakilishi wana posho maalumu kwa ajili ya jimbo lakini wanatumia kivyao.

Kwa hivyo, Mhe.Naibu Spika, nashukuru kwamba Mfuko huu utatoa elimu leo kwa wananchi wetu katika majimbo, kwamba wawakilishi walichokuwa wakikitumia katika majimbo ni imani zao pamoja na huruma kama wao walivyoonewa huruma na wananchi wao kuwachagua kuwa katika Baraza la Wawakilishi, lakini hawakuwa na Mfuko wowote wa maendeleo kama baadhi ya wananchi ambavyo walikuwa wakiamini hivyo.

Mhe.Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo naiomba serikali isije ikajisahau katika masuala mbali mbali ya maendeleo ya jimbo ikakosa kuendeleza huduma za majimbo kwa kuwa mwakilishi leo anapatiwa Mfuko huu wa Jimbo. Kwa sababu serikali ndio chombo kikuu cha nchi, kuna mambo makubwa makubwa ya maendeleo ambayo bila ya wao kwa Mfuko huu wa jimbo tu basi tutakuwa hatufiki pahala pakubwa.

Jengine nizungumze kwamba, niwaombe wananchi wetu katika majimbo, pamoja na kupitisha mswada huu baada ya kukubalika na kuwa sheria, basi mswada huu ni kwa ajili ya maendeleo ya jimbo si kwa ajili ya maendeleo ya mtu mmoja mmoja. Nasema haya kwa sababu nahofia kwamba labda inaweza kueleweka kuwa leo labda wawakilishi wanaupitisha mswada huu kwa ajili ya kutatua matatizo ya kila mtu katika jimbo. Ndio nasema hivi kwamba kila mwakilishi ana haki ya kusimamia masuala ya maendeleo ya jimbo.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba niunge mkono hoja hii kwa niaba ya wananchi wangu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa fursa hii, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia mara nyengine kukutana hapa kujadili masuala yanayohusu nchi yetu.

Mhe.Naibu Spika, mimi naomba nianze kuuchangia Mswada huu kwanza kueleza *reservation* zangu. Mhe.Naibu Spika, wakati Bunge wanapitisha mswada kama huu mimi niliwahi kushiriki katika mjadala mmoja na vyombo vya habari nikipinga dhana nzima ya kuwepo kwa mswada wa aina kama hii.

Mhe.Naibu Spika, nilifanya hivyo na mpaka leo naziamini sababu zile kwa sababu moja kubwa sana ambayo Mhe. Omar Ali Shehe ameigusia hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika uendeshaji wa nchi kuna mamlaka tatu hizi ambazo zimegaiwa majukumu yake. Mamlaka hii inaitwa Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utendaji wa Shughuli za Serikali. Sasa kwa mtazamo wangu mimi unapowaingiza wawakilishi katika shughuli za utendaji katika majimbo yao ikiwa ni dhamana yao ya kisheria maana kufanya tunafanya sote. Mimi natumia takriban asilimia 70 ya mapato ninayopata kila mwezi kwa shughuli za jimbo lakini sina dhamana ya kuwajibika kwa mtu yeyote, nafanya kama ni wajibu wangu kwa wapiga kura wa jimbo langu.

Lakini unapoweka utaratibu kama huu hii inaweza kufika pahala ikaleta mgongano wa kimaslahi. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, likitokezea lolote ambalo likapelekea kukiukwa kwa sheria hii kama sheria inavyosema inaweza ikamfanya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi sasa asiwe tena na nguvu ya kuhoji utendaji wa serikali kwa kuhofia kwamba akiihoji serikali na yeye ataelekezewa kidole. Ndio maana nikasema pale mwanzo kwamba mamlaka hizi tatu Mamlaka ya Utendaji ambayo ni Serikali, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Shughuli za Serikali ambayo ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Utoaji Haki ambayo ni Mahakama kila moja ikapangiwa majukumu yake. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, *in principle* hasa mimi *concept* hii inanipa shida sana.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba wenzetu wametaja mifano ya nchi nyengine ambazo zimeanzisha mifuko kama hii na pengine tunataja mafanikio yake kwa sababu ya uzoefu uliokuwepo wakati ule tunaanzisha. Lakini nafikiri Mhe. Naibu Spika, kama tutafuatilia tutajua kama Kenya kulikuwa na *scandal* kubwa sana miaka ya karibuni kutokana na mifuko kama hii kwa wabunge wake.

Zambia ambao hawakutajwa hapa pia wameanzisha mfuko kama huu nako kumekuwa na *scandal* kubwa sana kwa wabunge wake kwa sababu ya suala kama hili hata walikuwa wanafikiria kuondosha kitu kama hichi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema kuna matatizo sana lakini najua nawaelewa kabisa wenzangu ambao wanaunga mkono kwa sababu ya kuona kwamba katika hali ya umaskini ambayo inazikabili nchi zetu na maombi mengi ambayo yanakuja kutoka kwa wananchi tunaamini kwamba kuwepo kwa kitu kama hiki kinasaidia namna fulani kupunguza matatizo ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naelewa kwa nini wajumbe wenzangu wanaunga mkono lakini nasema pia upande mwengine huwa napata wasi wasi sana. Mhe. Naibu Spika, niseme nilianza kwa kusema kwamba nilishiriki katika mjadala kama ule nakumbuka hata baadhi ya wabunge ambao walishiriki mjadala ule wakaupinga. Kwa hivyo, walipata matatizo makubwa sana ya kupingwa na wabunge wenzao kule katika Bunge la Muungano. Lakini baadaye ikaonekana ni wachache mno kwa hivyo hawana uwezo wa kuuzuia mswada ule usipite na matokeo yake hata wao kwa sababu sheria imetaka kuwa nalo na inabidi wasimamie matumizi yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo huo siamini kwamba hata nikiupinga kama mswada huu hautopita. Kwa sababu kama nilivyosema naamini *majority* ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaunga mkono. Kwa msingi huo huo nimeona nitoe maoni pamoja na kwamba *in principle* siikubali hii *concept* lakini kama nilivyosema najua utapitishwa tu. Kwa hivyo, nikiuacha ukipitishwa tu bila ya kuutolea maoni katika maeneo ambayo pia yana matatizo naona nitakuwa siutendei haki. Sasa nimeona kwamba na mimi niuchangie katika baadhi ya vifungu ambavyo naona kwamba vinahitaji kutazamwa upya.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kifungu cha 6. Mhe. Naibu Spika, kwa maoni yangu kazi alizopewa Mkurugenzi hizi kwanza naziona ni nyingi lakini nyengine naona kama zitamshinda kwa hivyo tunaweza tukaingiza kazi hapa baadaye zikawa ngumu kutekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano katika jumla ya mambo yaliyotajwa hapa kifungu © kinazungumzia kupokea ripoti za robo mwaka na mwaka mzima pamoja na marejesho kutoka katika kamati na hili limejirejea katika sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa mtazamo wangu mimi nakubali katika misingi ya utawala bora kuwe na ripoti ya robo mwaka, lakini kwa kiwango cha fedha ambacho kimewekwa kuwa na ripoti za robo mwaka mimi naona kwa kamati hii kutakuwa na maripoti mengi ambayo idara hii itakuwa nayo ya kuyafanyia kazi majimbo 50 ambayo kila miezi mitatu yatakuwa yanaingia pengine hata zisiweze kufanyiwa kazi yake ambayo inakusudiwa. Kwa hivyo, nadhani kwa kiwango hichi ambacho kinazungumzwa pengine kungekuwa na ripoti angalau ya miezi sita halafu ripoti ya mwaka mmoja. Hayo ni maoni yangu.

Lakini la pili hichi kifungu cha (d) katika kifungu hichi cha 6 kupokea na kutatua migogoro inayohusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jimbo na kuchukua hatua zinazofaa. Maana tukianza kumfikisha pahala Mkurugenzi tukampa kazi ya kutatua migogoro ya miradi midogo midogo kama hii katika majimbo tutambebesha mzigo mkubwa sana kwa majimbo 50 ya Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba na hili Mhe. Waziri alitazame tena na aone kama kweli kuna haja ya kubebeshwa mzigo kama huu Mkurugenzi.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia niende katika kifungu cha 8, hichi nilikuwa naomba kutoa maoni ya jumla tu kwamba mbali ya yale ambayo yameelezwa hapa kuhusiana na mgawanyo wa fedha, mimi nilikuwa nadhani katika kuhakikisha kwamba baadae tutakuwa na uwajibikaji mzuri, basi kungekuwa na ripoti ya kila mwaka ambayo inaonesha fedha hizi ambazo zimetolewa serikalini kuwapa wawakilishi sasa hivi. Baada ya kupata yale marejesho yalivyotumika kungekuwa na ripoti ambayo inaonesha ili kuweka uwazi. Kwa sababu siudai uwazi kama mwakilishi kwa serikali katika matumizi, sisi kama tutakwenda kupewa jukumu hili sasa ionekane mfano hapa.

Kwa hivyo, nilikuwa nasema kungekuwa na haja ya kuweka ripoti za kila mwaka ambazo zinaonesha fedha ambazo zimeidhinishwa, zimetumikaje kwa kila jimbo hususan kama kuna matumizi mabaya au kuna kuvunja sheria basi itajwe katika ripoti hiyo katika muhtasari ambao utakuwa unatolewa kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kifungu cha 9 ambacho kinazungumzia kuanzishwa kwa kamati yenyewe na muundo wake. Mhe. Naibu Spika, kwa maoni yangu kwanza kamati hii ikilinganishwa kwa mfano na ile kamati iliyoundwa ya wabunge hii imekuwa ni kubwa mno. Kwa wenzetu katika wajumbe wale kuna diwani mmoja na kuna sheha mmoja, huku kumewekwa madiwani wawili na masheha wawili. Ukitazama hii kamati nadhani itakuwa na wajumbe kama 9. Sasa nasema tena Mhe. Naibu Spika, ukitazama kile kiwango chenyewe cha fedha kinachowekwa nadhani kamati hii ni kubwa sana.

Lakini pili nadhani waliofanya rasimu ya mswada huu hawakutazama vizuri. Kuna majimbo Mhe. Naibu Spika, sijui kama mnajua hapa kwamba yana diwani mmoja tu jimbo zima ni wadi moja. Yapo hapa katika taratibu za zamani za kukata kata majimbo na mambo yaliyokuwepo huko miaka ya nyuma sina haja ya kurejea ilifanyika namna kama hiyo. Sasa katika hali kama hiyo ukiweka sharti la kisheria kwamba kuwe na madiwani wawili jimbo moja litakuwa limejiondoa halina sifa ya kuwemo katika mfuko ule. Kwa hivyo, nadhani hili tulitazame tena.

Mhe. Naibu Spika, naomba niondoke hapo niende ukurasa wa 31 katika kifungu hicho hicho cha 9 (6) naomba kunukuu hapa inasema: “Bila kuathiri masharti ya kijifungu cha (5) cha kifungu hiki, inapotokea nafasi kuwa wazi katika kamati kwa sababu ya kujiuzulu, kutokuwa au kufa kwa mjumbe, kamati itajaza nafasi hiyo kutokana na asili ya nafasi hiyo ilipotokea.”

Sasa kwanza hii kutokuwa haifahamiki kutokuwa na nini, nimeangalia marekebisho ya kamati sikuona kama hili waliliona. Kwa hivyo, naomba hii kidogo Mhe. Waziri akija atuweke sawa hapa.
Lakini jengine napinga hata hiyo *concept* yenyewe kwa sababu inasema kukitokezea nafasi iko wazi kamati itajaza. Lakini kifungu cha 9 (2) ambacho kinazungumzia namna ya kuipata ile kamati utaona mteuzi wa kamati ile ni mwakilishi ndio anayewateua wajumbe kwa kushauriana na diwani na sheha. Sasa huku anayeteua ni mwakilishi ambaye ni mwenyekiti kwa kushauriana na hawa, lakini ikitokea huku tunaambiwa kamati nzima ndio ijaze. Hapa naona Mhe. Naibu Spika, kuna kugongana mimi nadhani utaratibu ule ule uliotumika katika kumpata mjumbe akiondoka ufuatwe kumpata mjumbe mwengine ndio tutakuwa tuna-*consistency* katika hii sheria.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba tufanye marekebisho ya uchapaji ambayo kamati haikuyaona. Ukurasa wa 31 kijifungu cha 9 (11) naomba kunukuu: “Mikutano ya Kamati itasitishwa na Katibu wa Kamati kwa maelekezo ya

Mwenyekiti au kwa maombi ya robo ya wajumbe wa Kamati yaliyowasilishwa kwa Katibu." Nadhani kilichokusudiwa ni itaitishwa hiyo imeachwa naomba tufanye marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika kifungu cha 10 Kazi za Kamati. Kwanza *concern* ipo pale pale kijifungu cha 2 (b) naomba kunukuu: "Kukusanya ripoti za robo mwaka na mwaka mzima, marudisho na ripoti zinazohusiana na miradi ya maendeleo yaliyotekelezwa katika jimbo hilo."

Mhe. Naibu Spika, bado mimi naona kwamba ripoti za robo mwaka kwa kiwango hichi kidogo cha fedha ni kuongeza kazi kubwa ambayo pengine haina sababu.

Lakini kijifungu (d) imeandikwa "kutekeleza kazi nyengine yoyote" imeishia hapo hapo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naogopa hii kamati isije ikajitwisha kazi nyengine yoyote tu kwa sababu sheria imeorodheshwa, ingefafanua nadhani madhumuni ya sheria hii ni kuhamasisha maendeleo ya jimbo. Kwa hivyo, nadhani tungefafanua kutekeleza kazi nyengine yoyote inayohusiana na maendeleo ya jimbo, isije ikawa tena inafanya kila shughuli huko tukasema sheria imewapa mamlaka hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kifungu cha 11 (2) sehemu ya nne Kukamilisha Mapendekezo ya Miradi ya Jimbo. Kifungu hiki kinasema "Kamati itaifanyia uhakiki miradi iliyowasilishwa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha (2) cha sheria hii."

Sasa kifungu cha (2) cha sheria hii kidogo kimenikwaza, kifungu hichi kinahusu ufafanuzi wa maneno yaliyotumika tafsiri za maneno. Sasa nikajiuliza miradi gani iliyoelezwa katika kifungu cha (2).

Lakini kama imekusudiwa kijifungu pia kijifungu cha kifungu hichi kitakuwa ndio hichi chenyewe cha (2). Kwa hivyo, haiwezi ikafanya *reference* kwa kijifungu cha (2) ilikuwa waseme tu kwa mujibu wa kijifungu hichi. Nadhani hii kidogo inaweza kuwa na matatizo ningeomba pia hili litazamwe.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha 14 (2) naomba hichi Mhe. Waziri akija anipe maelezo kidogo kinazungumzia zile fomu za maelezo ya miradi. Kifungu cha (2) naomba kunukuu kinasema: "Waziri kwa mashauriano na Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufanya masahihisho ya fomu hizi katika sheria hii."

Nilikuwa najiuliza masahihisho yepi ya lugha au hata ya kumrekebishia mradi mwakilishi na kamati yake ambayo kaleta. Hili kidogo liko *too general* nilikuwa naomba liwekwe vizuri zaidi hivi lilivyo kidogo linatutia mashaka.

Halafu naomba Mhe. Naibu Spika, twende kifungu cha 15 hiki kinasema Sifa za maelezo ya mradi naomba kunukuu: "Aina ya miradi itakayowasilishwa kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kupatiwa fedha kwa mujibu wa sheria hii itapashwa (nadhani imekusudiwa itapaswa) kutimiza masharti ya sheria hii pamoja na vigezo ambavyo vitatayarishwa na Mkurugenzi kwa mujibu wa sheria hii."

Sasa hivi vigezo kidogo Mhe. Naibu Spika, mimi vinanipa mashaka vile vile. Sheria kule mwisho inazungumzia Waziri anaweza kutunga kanuni nilikuwa nadhani bado majukumu haya kama ilivyokuwa kawaida kwa sheria nyengine ya kuweka sifa kama hizi yawemo katika kanuni kuliko kumpa madaraka Mkurugenzi tu kwamba anaweza kuweka vigezo vya kufuatwa na kamati nje ya vile ambavyo vimeshatajwa ndani ya sheria hii. Nilikuwa naomba pia hili tulirekebishe. Mhe. Naibu Spika, mimi pia niungane na Mhe. Hija Hassan Hija kuhusu kifungu cha 16 (3) aliposema "Miradi yote itakuwa ya maendeleo na inaweza kuhusisha gharama za upembuzi yakinifu, upangaji na michoro pamoja na mambo mengine ya kitaalam bila ya kuhusisha maendeleo ya kila siku ya miradi."

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema fedha yenyewe ukiiangalia si fedha kubwa kiasi hicho ni tofauti anavyotuambia Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba Kenya walipangiwa milioni 20 za Kenya kwa kila mwezi. Hapa tunazungumza kwa mfano kwa wastani tunaouzungumza sasa hivi ni bilioni 10 kwa mwaka mzima. Sasa ukisharuhusu zitumike kwa upembuzi yakinifu, upangaji na michoro zinaweza hizi zikatumika vibaya sana.

Haya Mhe. Naibu Spika, yanafanyika hata katika nchi za wenzetu zilizoendelea seuze katika nchi zetu. Mwaka jana palikuwa na *scandal* kubwa sana katika Bunge la Uingereza, kuna fedha ambazo zinaruhusiwa kuajiri kwa mfano Makatibu watu wakenda wakaajiri watoto wao zikawa zile fedha kumbe hakuna Katibu lakini zinatumika kuhalalisha kuomba viwanja anaambiwa ndio Katibu wa Bunge. Au wengine wakaajiri waume zao, wengine

wakaajiri wake zao, ilikuwa *scandal* kubwa sana mwaka jana mpaka ikasababisha kuwa ni *issue* kubwa katika kampeni za uchaguzi wa Uingereza kwamba wale waliochaguliwa na wananchi kuwa wasimamie mambo yao wao wenyewe wanatumia kujinufaisha wao binafsi.

Kwa hivyo, nasema na hapa kuna upenyo ambao unaweza ukatumika vibaya. Mhe. Hija Hassan Hija kapendekeza ingetajwa asilimia maalum mimi hata hiyo asilimia naogopa. Kwa sababu nasema fedha milioni 10 kwa mfano Mhe. Naibu Spika, ni mradi gani, hakuna mradi wa ujenzi kwa milioni 10, unajenga nini kwa milioni 10. Ni miradi hii midogo midogo *community problems.* Kwa hivyo nilikuwa nadhani haya mambo ya upembuzi yakinifu na upangaji wa michoro tungeliondoa hili kuja kuepuka fedha hizi kutumika vibaya dhidi ya serikali tukanuka Baraza zima kwa sababu ya mtu mmoja au wawili kuitumia vibaya nafasi kama hii.

Lakini hapo hapo Mhe. Naibu Spika, mimi sikubaliani na restriction iliyokuwepo katika kijifungu cha (4) cha kifungu hichi cha 16 katika sehemu moja. Kimesema "Fedha zitakazotolewa kwa mujibu wa sheria hii hazitatumika kabisa kwa shughuli za kisiasa na kidini."

Mhe. Naibu Spika, shughuli za kisiasa sina matatizo naunga mkono zisitumike kwa shughuli za kisiasa. Lakini kwa maumbile ya nchi yetu yalivyo kutu-*restrict* kwamba zisitumike kwa shughuli za kidini mimi sikubali Mhe. Naibu Spika. Ujenzi wa misikiti au ujenzi wa madrasa ni sehemu muhimu ya shughuli ambazo tunafanya kila siku. Nitakubali ukinambia tusitumie katika kuchangia maulidi kwa sababu huko kama unazo unataka kutoa ni fedha watu wakapige mpunga utatoa zako, lakini katika hizi za maendeleo ya jimbo ujenzi wa msikiti au ujenzi wa madrasa ni sehemu za maendeleo katika majimbo yetu. Madrasa zinatoa elimu na zinawalea watoto kimaadili pengine katika mambo ambayo skuli hazifanyi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba katika hali ya nchi yetu na hili tusilikwepe, tusitake kujifanya nchi yetu sisi hata kama tunasema ni *circular,* lakini katika katiba yetu sisi Kadhi Mkuu anachaguliwa na Rais, wala tusilionee aibu hili.

Mhe. Naibu Spika, nchi kama Uingereza inaambiwa ni nchi ya kidemokrasi na inaambiwa ni *circular* lakini kanisa la *Anglican* lina *role* maalum katika nchi ya Kiingereza kwa sababu ndio msingi ulivyonyanyukia nchi ile. Sasa na sisi tusikwepe mambo haya kwa kuogopa tutakuja kuambiwa kwamba tunadhamini shughuli fulani. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema hili tulitazame vizuri sana, mimi nadhani kwamba maadam shughuli hizi zitakuwa zinasaidia maendeleo katika jimbo ziruhusiwe kabisa na ni sehemu ya shughuli za maendeleo katika maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, humu katika mafungu ya wakubwa wetu Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais wanapotembelea miradi mingine wanaahidi kusaidia ujenzi wa misikiti kwa mfano, sijawahi kusikia kwa Zanzibar kusaidia ujenzi wa kanisa.

Mhe. Naibu Spika, fedha ile ni fedha ya walipa kodi kwa sababu ni katika fedha ambazo wanapewa katika kusaidia miradi ya maendeleo. Sasa kwa nini iwe inawezekana kule ijekuwa mwakilishi katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo isiwezekane. Mhe. Naibu Spika, mimi hili silioni mantiki yake na siliungi mkono. Mara nyingi ithibitishwe sana kwa vitu kama hivi kwa fedha ambayo inatoka ndani ya walipa kodi wa Zanzibar ambao wenyewe ndio watakaofaidika na miradi kama hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kifungu cha 20 na mimi nikubaliane na wenzangu sina haja ya kutoa maneno mengi. Hapa Mhe. Naibu Spika, pana mfumko wa kamati, maana tumetoka mfumko wa bei, mfumko wa sheria, sasa humu katika sheria kuna mfumko wa kamati. Maana kuna Kamati ya Maendeleo ya Jimbo, halafu kunaundwa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi, halafu kijifungu cha (6) cha kifungu cha 20 kinazungumzia Kamati ambayo kwa mujibu wa taratibu itakuwa ni ile Kamati ya Maendeleo ya Jimbo. Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu kifungu cha 20 (6): "Kamati itakuwa na wajibu wa kufanya ufuatiliaji katika utekelezaji wa miradi iliyoidhinishwa na kamati hiyo inaweza kuteua kamati ndogo kati ya wajumbe wa kamati hiyo kuwa na jukumu la ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa."

Sasa hizi kamati zimekuwa nyingi. Kama nilivyosema Mhe. Naibu Spika, sheria yenyewe tunaiona sisi wenyewe, mimi nilikuwa nadhani tungekuwa na kamati moja tu Kamati ya Maendeleo ya Jimbo. Sasa kama wenyewe watagawana majukumu kwamba miongoni mwao wanasimamia mradi fulani itakuwa ni jukumu lao mradi yale masharti mengine yaliyotajwa katika sheria kuhakikisha kwamba sheria zinafuatwa, kumbukumbu zinawekwa,

stakabadhi zinarejeshwa zinafuatwa itoshe. Lakini haya mambo ya kuwa na mfumko mkubwa wa makamati mimi siungi mkono.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kifungu cha 23 sehemu ya sita Fedha na Uendeshaji. Kifungu cha (2) hii *drafting* tu naona si sahihi. Kinasema "Angalau watu wawili watahitajika kutia saini kila hundi au hati nyengine kwa ajili ya malipo au utoaji wa fedha kutoka katika Akaunti Mfuko. Ikizingatiwa kwamba kwa utekelezaji mzuri wa kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, kila hundi ni sharti itiwe saini na Mwenyekiti au Katibu, pamoja na mjumbe mwengine aliyeteuliwa na Kamati kwa ajili hiyo."

Mhe. Naibu Spika, kijifungu cha (2) ndio kijifungu hichi sasa hatuwezi tena tukafanya *reference* kwa utekelezaji mzuri wa kijifungu cha (2) cha kifungu hiki. Nilikuwa nadhani tungesema tu kwa utekelezaji mzuri wa kijifungu hiki imetosha kabisa. Nadhani katika *drafting* wanajua wenyewe kwamba hii si *drafting* nzuri kukitaja kijifungu hicho hicho ambacho kinatajwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia Mhe. Waziri akija anisaidie katika sehemu hiyo hiyo kile kifungu cha 24 (1) naomba kunukuu, inasema:
"Kumbukumbu sahihi za malipo yote yaliyofanywa kwa kamati kwa ajili ya mradi katika kila jimbo na Katibu wa Kamati atazitunza na kuzirekebisha kila mwezi na kuziwasilisha kwa Mkurugenzi."

Sasa hii kila mwezi sikufahamu kwamba je, ni katika kuzitunza na kuzirekebisha tu, au pia kila mwezi zinatakiwa ziwasilishwe kwa Mkurugenzi. Maana yake kama kila mwezi anatakiwa aziwasilishe kwa Mkurugenzi ninajiuliza kule tumezungumzia miezi mitatu lakini sasa tunazungumza kila mwezi. Kwa sababu huwezi ukapeleka risiti tu bila ya kuwa na maelezo yake. Kwa hivyo nahisi kidogo hii inaongeza kazi kubwa kwa fedha ambayo si kubwa. Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri akija anisaidie ufafanuzi ili tupunguze urasimu uliomo humu.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kifungu cha 26 (1) naomba kunukuu kinasema: "Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu cha 24 cha sheria hii, Katibu wa Kamati atasimamia uendeshaji wa miradi iliyo chini ya sheria hii."

Sasa nasimama hapo kwa sababu huku ndani kabla tumezungumzia kamati zinasimamia hapa tunasema Katibu atasimamia. Halafu kuna Kamati ya Kusimamia Miradi, halafu kuna Kamati Ndogo. Hebu nataka hii sheria iwe *clear* anayesimamia nani, kama Katibu ndiye mtendaji kwa hivyo ndio dhamana isemwe hivyo. Lakini huku tusizungumzie miradi halafu tunazungumza Katibu ndio msimamizi wa uendeshaji wa miradi. Nataka hii tuweke *clear* hasa tukifanya *reference* na kile kifungu cha 20 ambacho nilikitaja tulipozungumza yale makamati mengi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa sehemu ya saba Masharti Mengineyo kifungu cha 30 kinachozungumzia Makosa na Adhabu. Mhe. Naibu Spika, nikubaliane na Mhe. Hija Hassan Hija kwamba adhabu zilizowekwa hapa hazilingani kabisa na uzito wa hii sheria yenyewe. Mhe. Naibu Spika, ikiwa fedha zinasimamiwa na kamati ni milioni 10 – 15 halafu unasema faini ya kosa hapo ni shilingi milioni 10 na kifungo kisichopungua miaka mitano.

Mhe. Naibu Spika, hatuna *consistency*, tuliwahi kuambiwa na Waziri mara moja katika kutunga miswada mingine huko kwamba tatizo letu hatuna fedha kuhusu adhabu kwa hiyo kila mmoja anaitunga sheria anavurumisha tu anasema miaka 15, miaka mitano, milioni 10.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nasema tumepitisha sheria hapa ya Madawa ya Kulevya karibuni tukaifanyia marekebisho vifungo ndio hivi hivi. Sasa nauliza hii Sheria ya Madawa ya Kulevya adhabu yake ikalingane na sheria ya mtu anaye-*handle* milioni 10 haiingii akilini. Kwa hivyo, naomba hili Mhe. Waziri alitazame tena katika sheria na adhabu.

Lakini zaidi siko hapo Mhe. Naibu Spika, hiki kijifungu cha 3 kwenye adhabu ni zaidi kinanitia mashaka. Hichi kinasema: "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na sheria hii kwa jambo ambalo si kosa chini ya kijifungu (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalazimika kulipa faini ambayo si chini ya shilingi laki tano na si zaidi ya shilingi milioni mbili, au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote mbili."

Mhe. Naibu Spika, hichi kifungu kimetoa mamlaka makubwa mno ya kufanya kila kitu kiwe kosa katika sheria hii. Kwa sababu kinasema kila mtu anayekwenda kinyume na sheria hii sasa maana yake nini. Atakayekuwa hakuwasilisha fomu kwa sababu kuwasilisha fomu iseme sheria hii, kwa hivyo kama hujawasilisha fomu kwa

Mkurugenzi pia utakuwa umetenda kosa wewe mbali ya ile kuwasilisha stakabadhi. Kama umetakiwa uunde kamati hujaunda itakuwa pia umetenda kosa kwa sababu hichi kifungu kilichowekwa ni kwamba ukikiuka sehemu yoyote ya sheria hii ni kosa.

Hiki nadhani ni *too wide* namuomba Mhe. Waziri akae na Mwanasheria Mkuu na wanasheria wake wakitazame tena, hichi kifungu hakikubaliki kabisa nilikuwa nadhani tukiondoe. Tungeweka wazi kwamba kuna makosa ambayo yanahusiana na kile kifungu cha 30 (1) kwa mtazamo wangu mimi kilikuwa kinatosheleza. Kwa sababu kinasema "Mtu yeyote atakayetumia vibaya, atakayesaidia au atakayesababisha mtu mwengine kutumia vibaya au atakayetumia fedha au mali za mfuko kinyume cha matakwa ya sheria hii, atakuwa ametenda kosa."

Nilikuwa nadhani kile kwa maana ya kulinda dhidi ya wizi, rushwa, matumizi mabaya kishatosheleza ku-*cover* maeneo yale. Mimi nilikuwa nadhani hichi kijifungu cha (3) kiondoke kabisa ili kutokuja kutumika vibaya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema napata vigumu sana kusema nauunga mkono mswada huu kwa sababu ile niliyosema mwanzo. Lakini nausaidia kuurekebisha kama nilivyosema mimi ninaamini utapitishwa tu, kwa hivyo nataka hata ukipitishwa tulisaidie Baraza kutunga sheria ambayo itakuwa nzuri. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

Mhe. Abdulla Juma Abdulla: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi angalau kuubariki mswada ambao ni muhimu. Mimi pamoja na yote lakini nataka niipongeze serikali kwa kutuletea mswada huu wa sheria ambao tukiangalia kwenye madhumuni yake ni kuharakisha maendeleo katika majimbo yetu. Suala la maendeleo ndio *concern* ya nchi kwa hivyo madhumuni haya yananishawishi niipongeze serikali kwa kuleta mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada ni muhimu kwa sababu una Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDF)* ambao utasaidia sana kupunguza changamoto za wananchi hasa kule kwenye *grass roots*. Kwa sababu miradi ya serikali mara nyingi inalenga katika maeneo haya yaliyo karibu karibu, maeneo ya mijini, labda maeneo ya njia za kuendea bandarini, uwanja wa ndege, huko utakuta maendeleo serikali inaangalia humo ambamo mko machoni kwa watu.

Mhe. Naibu Spika, kule kuna vijiji ndani ya mapori serikali si rahisi kuviona lakini wakifanya hivi kwa mfuko huu sasa hasa kwa sababu uko chini ya uangalizi wa mwakilishi ambaye yuko karibu na hao wananchi huko chini basi maendeleo yatakuwa yametawanyika kila kona ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine muhimu zaidi katika mfuko huu mimi mara nyingi nimekuwa nikieleza masikitiko yangu katika namna ya kupembua vipaumbele vya maendeleo. Wataalamu wa mipango wana hadidu rejea zao. Lakini mimi kama ni Mwakilishi ninayesimamia watu na watu nao wana vipaumbele vyao kwa mujibu wa mazingira yao wanayoishi, ambavyo mara nyengine vinatofautiana na vile vipaumbele walivyo viona wataalamu.

Kwa hivyo, nasema ni muhimu kwa sababu mfuko huu sasa utasaidia angalau wataalamu wao na waone vipaumbele vyao wafanye, lakini na mfuko huu utasaidia kuna vipaumbele vile walivyonavyo wananchi wenyewe kwa mazingira yao, hivyo ni mfuko muhimu.

Mhe. Naibu Spika, tumeelezwa humu kwamba fedha hizi zitasaidia maendeleo na ndivyo ilivyo, lakini kwa kuwa nia ni maendeleo, naamini Serikali kuu nia yake ni maendeleo. Lakini pia na hii kamati ya jimbo itakayoundwa chini ya uwenyekiti wa Mwakilishi nia yake itakua hiyo hiyo ya maendeleo.

Sasa mimi nilikua nadhani ikiwa lengo ni maendeleo basi hizi fedha Serikali iangalie zaidi kuziongeza ni kidogo mno. Ni kidogo mno Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna vijiji labda nivitaje vichache tu katika jimbo langu ambavyo toka siku vilivyoumbwa na toka siku Serikali hii ilipoingia madarakani basi havijapata huduma yoyote ya kijamii. Huko hakuna barabara, hakuna maji, hakuna hospitali. Kama ni skuli basi waifuate mbali kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mimi nina kijiji cha Kilindi hawana chochote hao, kuna kijiji cha Mwachawa, kuna kijiji kinaitwa Chanoni, kuna kijiji kinaitwa Ngomeni na ni vijiji muhimu kweli kweli, kwa sababu maeneo haya ni maeneo ya rutuba sana na ni maeneo ambayo wananchi wanajitahidi kulima sana, lakini wamekosa miundombinu ya maji, umeme, barabara na kila kitu.

Sasa Serikali ikinipa milioni 10 nitajiuliza, hivi nakwenda kutatua au nakwenda kusababisha ugomvi. Kwa sababu milioni 10 nikizipeleka Kilindi basi watu wa Mwachawa watakuja juu, aah bwana vipi mbona unafanya huko tu, kwa sababu na wao wana hamu, wana njaa na wana kiu ya maendeleo. Kwa hivyo, nilikuwa naiomba sana Serikali iwafikirie tena hizi pesa waziongeze angalau hamna hamna basi zifike milioni 50, zitasaidia angalau kwa miradi miliwi au mitatu midogo midogo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine muhimu sana ukisoma kifungu cha 8 katika sehemu ya 4, kile kifungu ni muhimu sana, naomba ninukuu kidogo pahala padogo tu. Kopi zote za kumbukumbu ya fedha zilizopokelewa na kamati, imekusudiwa kamati ya maendeleo na matumizi yaliyofanyika yatapelekwa kwa Mkurugenzi ndani ya siku 30 kabla ya kufungwa kwa mwaka wa fedha. Hapa maana yake nini. Maana yake kamati itakapotumia, kwanza itumie kwa mujibu wa sheria ya fedha, sasa ndani ya sheria ya fedha kuna *procurement, procurement* ni utaratibu mrefu mtu wa kamati ya jimbo aliyekuwa hajui hata a, b, c huyo hatoweza kufanya chochote katika masuala haya.

Kwa hivyo, inawezekana hata miaka mitatu ikafika lakini kamati hii ikashindwa kupeleka ripoti kwa Mkurugenzi jambo ambalo, maelezo yanayofuata yanasema hakutafanywa mgao mwengine wowote wa mwaka mpya wa fedha hadi hapo marudisho hayo yatakapotolewa kwa Mkurugenzi. Kwa maana hiyo jimbo mwaka wa pili linaweza likakosa.

Sasa nilikua naomba sana Serikali iandae utaratibu wa mafunzo, hizi kamati za maendeleo za jimbo zipatiwe mafunzo angalau zijue a, b, c namna ya kutumia, namna ya kutunza kumbukumbu na namna ya kudai risiti na mambo mengine ili zisije zikapata kikwazo kwamba jimbo lile mwaka wa pili unaofuata likakosa mgao.

Halafu jambo jengine Mhe. Naibu Spika, hili nataka nitoe tahadhari kidogo, nataka nitoe tahadhari kwa sababu pesa hizi za *CDF* ni pesa za Serikali na ukisoma kifungu cha 8 cha sehemu ya 7 kinasema kwamba fedha zote zilizopokelewa kwa mujibu wa sheria hii zinapokelewa na kutolewa taarifa kwa Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali kama ilivyo kwa fedha nyengine za Serikali katika Wizara. Yaani hizi fedha zitakaguliwa matumizi yake yote na ionekane kama zimetumika kihalali kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa. Sasa hatari iliopo ni kuja mtu kuona kapata pesa ama yeye Mheshimiwa mwenyewe akawa ana matitizo yake binafsi akanyoboa nyoboa. Ukinyoboa maana yake utashindwa maelezo.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni miongoni mwa kile kikundi ambacho tulifuatana na kina Mhe. Hamza Hassan Juma tukenda Kenya kusoma uzoefu wa wenzetu wa *CDF*. Kuna wabunge kule walipoteza nafasi zao za ubunge kwa sababu hii ya kunyoboa nyoboa fedha za *CDF*. Kwa hivyo, nilikua nawaomba sana wenzangu wajitahidi sana kufuata hii sheria na sio wenzangu tu. Najua mimi waheshimiwa watapata vikwazo vikubwa, kwa sababu utakapoitisha kikao cha kamati ya maendeleo ya jimbo, kwa kuwa pale ajenda ni fedha basi nina hakika utadaiwa *allowance*. Kwa hivyo, ni lazima uwe makini kweli.

Kuna mjumbe mmoja kasema humu labda utoe pesa mfukoni mwako utoe *allowance*, lakini ukinyoboa humu, basi labda uwe na sababu nzito sana, vyenginevyo Mkaguzi akija atakutia kwiri, akikutia kwiri mwenzangu umepoteza kiti. Pengine kifungu cha 30 kule kinaweza kikakukamata ukalipa fidia ya milioni 10 ingawa waheshimiwa wanasema ni nyingi sana, lakini kwa vyovyote vile ni lazima tuwe waangalifu sana.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo haya niliyotoa hivi punde, lakini ukisoma kifungu cha 27 pale pana gharama za uendeshaji wa mfuko. Sasa matumizi ya kuendesha shughuli za mfuko zitatokana na fungu la bajeti ya Wizara. Mimi sijafahamu uendeshaji upi, maana hii Kamati ndio itakayokua inasimamia pesa hizi, ndio itakuwa inapanga na kufanya upembuzi wa miradi, pengine itahitaji kuandaa maandishi kidogo ya mradi na yote ni mambo ya gharama, itakaa vikao na yote ni mambo ya gharama.

Je, kifungu hiki kinakusudia gharama kama hizo zitaingizwa kwenye bajeti ya Wizara. Naomba hapa Waziri atakapokuja atupe maelezo kidogo ili tufahamu vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi niseme tu kwamba mswada huu kama nilivyotangulia kusema kwamba naukubali mia juu ya mia na ninauunga mkono. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya Mhe. Waziri ya Kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niipongeze Serikali kwa wazo zuri kabisa hili la kuanzisha mfuko huu. Mfuko huu kwa kweli ni muhimu sana katika kusaidia kuleta maendeleo ya wananchi wetu kwenye majimbo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina tatizo sana na huu mfuko, lakini kuna mambo mawili au matatu nimeyaona nahisi kidogo yanahitaji marekebisho, ingawa wenzangu wachangiaji waliopita wameyazungumza kwa kuyachanganua sana, basi na mimi nitachukua mawili matatu na mimi niliyoyaona hapa ili Mhe. Waziri atakapokuja hapa na yeye atusaidie katika kuyafanyia marekebisho ili mfuko wetu huu uweze kufanyakazi vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikianza niende moja kwa moja katika sehemu ya nne ya kukamilisha mapendekezo ya miradi ya jimbo, kwenye kifungu cha 12 aya ya 3, ambacho kinasema Mkurugenzi ataweza kuirudisha miradi kwa Kamati, pale ambapo itabainika vigezo havikuzingatiwa, ili Kamati ifanyie kazi kabla ya kuiwasilisha tena kwa Mkurugenzi. Sasa kidogo hapa ninapata shaka, kwa sababu kamati iliyokaa kupitisha ile miradi kule, ndio kamati kubwa kabisa ile, lakini maamuzi ukimpa Mkurugenzi ya kubana hii, akasema hapana haikukamilia hii rudini, nahisi kama ile kamati utakua umeipunguzia ule uwezo wake au zile nguvu zake ilizonazo pale, kwamba mtu mmoja anaweza kupinga maamuzi ya Kamati ya mradi ule.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, inawezekana kwa utashi tu, maana sisi tunaishi hapa tunajuana, kwa utashi tu, inawezekana Mkurugenzi ana nia na yeye ya kuja jimboni mwakani na mimi Mwakilishi ndio nipo kwa sasa, basi tumeandaa miradi yetu, tunapeleka kwake, basi kwa kuonesha tu kwamba Mwakilishi aah! Hana lolote huyu, basi anakurejesheni rejesheni ili ionekane huu mradi haufai. Lakini kile kikao ambacho kimekaa kule kuna Mwakilishi, kuna Madiwani na kuna Masheha na wale Wananchi wenyewe wa kwenye jimbo lile, wenye ile miradi yenyewe wanaona umuhimu wa miradi ile, basi wameshapendekeza kwamba hivi ndio vipaumbele vyetu vya miradi hii.

Sasa atakapokua yeye anaikataa na kusema haikukamilia au haikukidhi vigezo basi anaweza akawapa sababu za uongo na kweli, ilimradi mimi nahisi kama kutakua kuna usumbufu. Ni vyema miradi ile mimi nahisi ikishaamuliwa kule na ile kamati basi miradi hii iletwe huku kwa kuendelezwa, sio kuwa ianze tena kurejeshwa kule, itaonekana kama hiki kikao hakikutimia vizuri ninavyohisi. Mhe. Naibu Spika, hilo lilikuwa moja katika fungu hili.

Mhe. Naibu Spika, nisogee mbele kwenye kifungu cha 16 kwenye aya hiyo ya sehemu ya nne ambayo inazungumzia fedha zitakazotolewa kwa mujibu wa sheria hii hazitotumika kabisa katika shughuli za kisiasa na kidini. Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumzia hili na mimi nataka nikazie hapo hapo. Kwa sisi huku kwetu unaposema shughuli za kidini, maana yake kasema Mhe. Ismail Jussa hapa. Kwa mfano kujenga Misikiti na kujenga Madrasa. Ukiangalia kwa mazingira ya kwetu kama mimi kwenye jimbo langu, kwa asilimia 100 pale katika jimbo langu sisi sote ni waislamu.

Sasa wakati mwengine kipaumbele kwetu sisi yaani kwa wananchi wangu pale ni ujenzi wa msikiti au ujenzi wa madrasa, sasa ikiwa wameamua wananchi kuwa kipaumbele chetu sisi, kwa mfano Skuli tumejenga na sasa tunataka tujenge madrasa, kwa sababu madrasa nayo inatoa elimu, inatoa elimu ile ile kama inayofanana na ile ya skuli. Kwa hivyo, wanaamua sasa kutaka kujenga ile, sasa hapa katika sheria hii inaonekana kwamba kitu kile kitakuwa hakiwezekani.

Sasa mimi ningemshauri Mhe. Waziri kwamba kifungu hiki tukakiondosha ili tuweze kupata nafasi kwa wale wananchi wetu hasa kwa mazingira ya hapa Zanzibar. Kujenga madrasa ni sehemu ya wananchi. Kwa sababu wenyewe madrasa ndio wameshaamini kuwa hiki ndio kitu chao kama ni sehemu ya kutoa elimu, sasa tutakuwa tunajenga skuli tu au chekechea, lakini unapojenga madrasa nayo inatoa elimu ile ile. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba kifungu hiki tukiondoshe ili tuwape nafasi kwa wale wananchi ambao wataamua wenyewe kujenga msikiti katika eneo lao kwamba ndio sehemu ya maendeleo katika jimbo lao, basi iwe inapatikana ruhusa hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele kwenye sehemu ya fedha na uendeshaji. Hapa kidogo nina mashaka, kwa sababu hii sheria ina mambo kidogo, usimamizi wa fedha, niko hasa kwenye usimamizi wa matumizi ya fedha kwa sababu fedha hizi ni za Serikali. Nikianza kwenye aya ya pili 23, inasema angalau watu wawili watahitajika kutia saini kila hundi au hati nyengine kwa ajili ya malipo au utoaji wa fedha kutoka katika *account* ya mfuko, ikizingatiwa kwamba kwa utekelezaji wa mradi wa kijifungu cha 2 cha kifungu hiki kila hundi ni sharti itiwe saini na Mwenyekiti au Katibu, pamoja na Mjumbe mwengine aliyeteuliwa na Kamati kwa ajili hiyo.

Mimi ninavyojua Mhe. Naibu Spika, haya mambo ya fedha ni lazima yasimamiwe na mtu mwenye taaluma hii ya mambo ya fedha. Unaposema Katibu mjumbe mwengine yeyote tu asaini, kwanza huyu Mwenyekiti hapa mimi ningeshauri asiwe anasaini, huyu Mwenyekiti wa hii kamati asiwe ana saini, kwa sababu yeye ni Mwenyekiti ana mamlaka ya kutoa maamuzi kwenye kikao, lakini suala la kusaini hizi lingepewa mshika fedha ambaye ana taaluma ya ile fedha, kwa sababu hizi fedha zinatakiwa zitumike kwa mujibu wa sheria ya matumizi ya fedha. Sasa ni lazima huyu mtu ambaye atakuwa anazishika hizi fedha awe ana taaluma ya fedha. Sasa sijui huyu Mhe. Waziri hapa anatuambiaje juu ya mtu wa namna hii.

Kwa mfano unaweza kwenda kwenye baadhi ya majimbo, ukakuta unachagua hii Kamati hakuna mtu mwenye taaluma ya fedha, mkampachika jukumu la kusaini hapa, Katibu inawezekana akawa na uwezo tu wa kuratibu yale mambo, lakini sio mtaalamu wa mambo ya fedha na ukasema mtu mwengine umchague miongoni mwa wale wajumbe wa kamati ambao wamependekezwa basi hana taaluma ya fedha, Mwenyekiti naye hana taaluma ya fedha, sasa sijui usimamizi wake utakuwaje hapa na hii sheria unamuambia aende kutokana na sheria ya fedha na matumizi ya fedha za Serikali, sasa sijui watayajuaje haya. Mimi naona hii sheria hapa tukienda hivi baada ya mwaka mmoja basi hawa wajumbe wote wanaohusika na fedha tutawafunga.

Mimi nipo kwenye kamati ya PAC ni mjumbe, kwa hivyo nazijua hizi sheria za fedha nimejifunza kule. Sasa nahisi huu mzigo tukiwapa tu hawa au Mhe. Waziri atuambie kila jimbo atatuletea mtu anayeshughulika na masuala ya fedha juu ya kamati hizi, basi mimi nitakubaliana naye kwamba kwenye kamati hizi nitawapeni mtu mwenye taaluma ya fedha ambaye huyo atakua anashughulikia hizo fedha. Anachukua maagizo ya kamati, lakini yeye atakuwa anazisimamia kwa kuziwekea utaratibu ule wa matumizi ya Kiserikali. Lakini kwa kuwapa hawa watu wetu.

Kwa mfano katika jimbo langu basi utanifungia bure watu wangu, kila siku nitakuwekea watu utawafunga. Kwa kufuata hivyo wakakuwekea kumbukumbu hizi vizuri ni pagumu kidogo, vyenginevyo basi watu hawa wapate taaluma kwanza. Suala hili Mhe. Waziri nilikuwa naliangalia hivyo.

Lakini nikisogea kwenye kifungu cha 23 aya ya 7 kwenye nyongeza yoyote ya mapato, riba na madai kutoka kila mfuko yatatolewa taarifa kwa Mkurugenzi pamoja na nakala za marejesho ya mwaka. Ndio ninakuja kwenye hoja yangu ile ile, huyu mtu atayatayarisha vipi haya kumpelekea Mkurugenzi kama hana taaluma ya fedha, maana aweke mahesabu na aweke ule mpangilio.

Hawa watu tuliowachukua jamani tusijione kama majimbo ya mjini, mjini huku utayapata maana yake ndio watu wote wanakaa mjini. Sisi kule kwetu hasa majimbo ya kwetu vijijini ni tatizo hili, kuwapata watu wenye taaluma hii wakaweza kuweka huu mpangilio na hii ni sheria, tukishaipitisha hapa inatakiwa utekelezaji wake uanze. Hakufanya haya, nimeangalia kwenye kifungu cha mwisho kuna adhabu huku.

Kwa hivyo, kama hakuweka haya vizuri basi Mhe. Waziri utanifungia wengi, itakuwa mwisho hizi fedha niziogope hata nisizichukue. Jambo ambalo litakuwa linarejesha sana nyuma maendeleo ya wananchi wangu.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo kwenye kifungu cha 23 aya ya 8 inasema, hakuna fedha zitakazoingizwa kwenye *account* ya kamati nje ya fedha za mfuko. Sasa hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi, huu mfuko una fedha zake ambazo zinakua zinapatikana kutoka Serikalini, lakini inawezekana kuna wafadhili ambao wameamua kutusaidia, maana yake fedha zile zisiingizwe katika *account* ile. Suala hili nilikuwa nataka kidogo nije nipate ufafanuzi. Nafikiri Mhe. Waziri umenielewa hapa juu ya hili suala la fedha, fedha nyengine yaani kutoka nje ya zile za mfuko ambazo zimetoka katika Wizara yako. Mfadhili ametoa fedha tusiziingize kwenye mfuko ule hata kama unaendelea kuendelezwa ule mradi ambao tumeuomba.

Kwa mfano ule mradi tulioombea ni wa ujenzi wa skuli, lakini wewe umetupa milioni 5 tu za ujenzi ule, kuna Mfadhili katupa milioni 20, ina maana tusiziingize hapa. Je, ule mradi ambao tunauombea usije ukaingiziwa fedha nyengine zozote isipokuwa zile ambazo utakuwa unazitoa wewe tu. Kwa hivyo, ukitoa milioni 5 basi tujengee hizo 5 halafu mpaka tusubiri mwakani, hapa kidogo nilikua nahitaji nipate ufafanuzi katika uingizaji wa fedha hizi.

Nikiendelea mbele Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 24 kwenye kumbukumbu sahihi za malipo yote yaliyofanywa kwa kamati kwa ajili ya mradi katika kila jimbo na Katibu wa Kamati, atazitunza na kuzirekebisha kila mwezi na kuziwasilisha kwa Mkurugenzi. Hapa napo napaona kwamba kila mwezi Katibu awe anatayarisha,

anaziandikia na anazipeleka kwa Mkurugenzi. Lakini tukumbuke Katibu huyu sio mwajiriwa huyu, inawezekana ana kazi zake nyengine, hizi kazi za kuwasilisha kila siku kwa Mkurugenzi na Wakurugenzi wetu tunawajua hapa. Unaweza kwenda karibu mara tatu hujamkuta, na pengine amkute ili aziangalie waweze kuzungumza na kumfahamisha mawili au matatu. Tunaona kuwa tutakuwa tunamuongezea shughuli ambayo na huyu hana malipo, huyu ni mtu wa kujitolea tu kwa nilivyofahamu mimi. Sasa kama mtu wa kujitolea atakua anahangaika pasi na kitu chochote basi hii kazi itafeli, kwa sababu atafika pahala atachoka na kusema huu ukatibu siutaki na kila utakayemchagua atakuwa hivyo hivyo, kwa sababu kwa kazi ya kuihangaikia hivi na hakuna tija yoyote anayoipata basi hatoweza kwenda kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, naona tuangalie mazingira mengine. Aidha, utuletee watendaji kutoka afisini kwako ambao utakua unawalipa, halafu sisi wanatufanyia kazi au tuangalie utaratibu mwengine juu ya hili, lakini kila mwezi kumlipa Mkurugenzi huyu, shughuli hii itakua kubwa kidogo. Kwa sababu sisi majimbo yetu yako vijijini na yeye atahitaji kutumia nauli, akija leo akimkosa akirudi, kesho aje tena arudi, utakuta siku tatu au nne kaja kumtafuta Mkurugenzi atakua anatupa gharama zake kutoka mfukoni na hali ya wananchi wetu tunaijua kule ni maskini mno. Usiifikirie ile Shilingi 1,500/- kuja na Shilingi 1,500/- ni Shilingi 3,000/- hizo, kwa wiki hizo akija mara tatu ni Shilingi 9,000/- ni kubwa sana kwa mtu wa kijijini. Vinginevyo mzigo huo utakusimamia Mwakilishi utoe nauli, sasa na mimi ikiwa nitoe nauli tu kwa kushughulikia jambo hili basi itakuwa na hayo mengine hayaendi, badala ya faida tunapata hasara sasa. Mimi nafikiri jambo hili Mhe. Waziri nalo ulitizame kidogo.

Nisogee mbele Mhe. Naibu Spika, kwenye kifungu cha 25 katika ukaguzi na uhasibu. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakua na mamlaka kamili ya kuzikagua hesabu za kamati na mfuko kwa kutayarisha ripoti kwa ajili hiyo. Aya ya pili inasema, kwa kuzingatia sheria ya fedha za umma, kamati zitawasilisha ripoti zao za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa ajili ya uchunguzi kama inavyoelekeza kwenye sheria hii. Hapa ndio swali langu linakuja, nimeshalizungumza kule nyuma. Kamati ndio inatakiwa ifanye, sasa nani ndio atakua ana wajibu wa kuzisimamia zile hesabu, ndio tatizo langu, nani. Maana yake hesabu zote zinasimamiwa na Mhasibu au mtu mwenye taaluma ya hesabu. Sasa hapa unasema kamati, unakusudia Mwenyekiti, au Kamati unakusudia Katibu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ingekuwa kuna mtu wa fedha hapa, ukishasema Kamati itasimamia basi inajulikana moja kwa moja Mhasibu ndiye atakayelisimamia hili, maana anajua Mhasibu kazi yake yeye kwenye Kamati nzima kuratibu mambo ya fedha, hata kama mtatoa miongozo Kamati, lakini Mhasibu ndio anayesimamia hili. Sasa fedha hizi zinatakiwa hesabu zake zipelekwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, nani anazipeleka kule na nani atakuwa ndiye anawajibika katika hili. Sasa hapa kidogo Mhe. Waziri mimi naona pana tatizo, hebu uje utusaidie ufafanuzi kidogo katika hili, maana yake hapa kuzipeleka pesa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hazipelekwi tu kama ninavyofanya mimi moja na moja ni mbili, najua kuna utaratibu mzima hapa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ukitutizama Kamati ile ambayo ndio inaitwa Kamati sote kama Mtando hatuna kitu, mimi ndio Mwenyekiti mfano, ndio nitakuwa Mwenyekiti maana ndio Mwakilishi wa jimbo, sina mimi taakuma ya hesabu. Haya na hao wanaonifuata hawana taaluma ya hesabu. Mimi naona hapa Mhe. Waziri umetuwekea mtego, naona kama unataka kutufunga. Ndio maana nikasema mapema kwamba huyu Mwenyekiti usimshirikishe kwenye mambo ya hesabu, akae pembeni asisaini kabisa ili yeye abakie kuwa Mwenyekiti aweze angalau kuwashughulikia hao wengine. Lakini hapa ni lazima tuwe na mtu wa hesabu, kama hatukuwa naye basi Mhe. Waziri mtego huu bwana mimi sikubaliani nao, huu mimi nahisi ni mtego. Kwa sababu ukishamtaja Mdhibiti basi huyu ana sheria yake kabisa, hata haoni hasikii kama hukupita kwenye ule utaratibu wake, utatufunga huu.

Mhe. Naibu Spika, siku zote tunalalamika hapa watendaji kutokufuata sheria za fedha, maana yake na huyu itakua umempa jukumu la kusimamia sheria za fedha, lakini si mwajiriwa wa Serikali. Sasa sijui utakuja kumchukulia hatua vipi, maana yake huyu mtu ambaye huku kwenye hii kamati hakuna mwajiriwa wa Serikali pale zaidi ya Mwakilishi labda ndio mwajiriwa naweza kusema ambaye ndio Mwenyekiti. Lakini hawa wajumbe wengine, ndio maana ninapata wasi wasi na hii Kamati, kama hukutuwekea mtu wa fedha basi kuna masharti humu ni lazima uyapunguze, kwa sababu kumwambia tu mtu asimamie sheria ya fedha na matumizi haya ya fedha za Serikali ni pagumu, hatoweza kufanya hivyo kwa sababu hana hiyo taaluma. Lakini hata ule wajibu wa kumlazimisha wewe pia sijui kama unapatikana, Mwanasheria pia anaweza kutusaidia, sijui kama kutakua kuna uwezo wa kumshika kiasi hicho, maana hakuna kitu kitakachomlazimisha. Yeye anakwenda pale kama ni kujitolea sio mwajiriwa, lakini

unampa kazi azisimamie zile sheria za Serikali, kwa sababu zile fedha ni kweli ni fedha za Serikali zilizotoka lakini yule unaekwenda kumpa kuisimamia ile fedha si Serikali, naona hapa kidogo patakuwa pana tatizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiria nimezungumza mengi, wenzangu waliotangulia wamezungumza mengi sana, nilitaka kuongezea hayo. Lakini niende mbele kidogo nimalizie kwenye masharti mengineyo hapa kwenye kifungu cha 30, kwenye makosa na adhabu. Kifungu cha 30 kinasema, mtu yeyote atakayetumia vibaya, atakayesaidia au atakayesababisha mtu mwengine kutumia vibaya, atakayetumia fedha au mali za mfuko kinyume cha matakwa ya sheria hii basi atakua ametenda kosa. Mimi nakubali.

Kifungu cha pili kinasema, mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hiki, atalazimika kulipa faini ambayo sio chini ya shilingi 10,000/- na sio zaidi ya shilingi 20,000/- au kifungo kisichopungua miaka 5 au adhabu zote mbili faini na kifungo kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hii ni adhabu lakini ni kubwa mno. Ndio pale niliposema huu ni mtego anatuekea Mhe. Waziri atatumalizia watu wetu, hawa atawafunga wengi kwa sababu huku makosa yatatendeka kama hawa watu hawana taaluma ya hili jambo. Sasa na hii adhabu ukiitazama ni kubwa, tumepitisha sheria nyingi hapa naziona adhabu zake na bado tulikua tunaomba kuna adhabu kwa mfano, zile za wale wabakaji tulizipitisha hapa, tukawa tunazitaka ziongezwe. Tuliombwa hapa na Mhe. Waziri, kwamba kwa sasa tuanzie na hapo, wakati yale ndio makosa makubwa zaidi. Sheria za dawa za kulevya hapa tumeziona na juzi tulipitisha sheria ya rushwa, lakini eeh! Hii ilivyowekwa, hawa watendaji walivyoandaa huu mswada si wanakusudia kutufunga sisi wawakilishi hawa. Mhe. Naibu Spika, usicheke maana kila nikitizama naona yuko kama anatukomoa. Mimi ningeomba hii adhabu ipunguzwe kwa sababu makosa haya mengi yanaonekana yatakua ni makosa ya kifedha zaidi. Sasa hii adhabu iliyowekwa naomba kidogo ipunguzwe kidogo ni kubwa mno.

Mhe. Naibu Spika, mimi niungane na Mhe. Ismail Jussa Ladhu katika kupendekeza kwenye hiki kifungu cha 3 kwamba kiondoshwe kabisa. Mimi naunga mkono hoja yake pale kwamba kifungu hiki cha 3 katika kifungu cha 30 kiondoshwe kwa sababu imeshasemwa huko mwanzo, kwa hivyo inatosha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nisubiri ufafanuzi halafu nitakuja kutoa maelezo yangu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie mswada huu muhimu sana wa maendeleo ya nchi yetu. Nasema kwa mara ya mwanzo katika mkutano huu na mimi niungane na wenzangu wote kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Bububu, kutokana na kufiliwa na Mwakilishi Mhe. Salum Amour Mtondoo.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika Jimbo la Uzini, na hivi ninavyosema inawezekana yuko katika kutekeleza majukumu yake mengine huko. Lakini pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kumteua ndugu Yahya Khamis Hamad kuwa Katibu wetu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nianze kutoa pongezi za dhati kabisa kwenye ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwa Waziri wake, kwa kuleta mswada huu kwa wakati muafaka kabisa kwa maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, tuipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kuleta mswada huu hapa na tukaujadili na nina hakika Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu wataunga mkono mswada huu kwa sababu una maslahi yetu sisi. Sidhani kama atatokea Mwakilishi kuzuia au kusema kwamba mswada huu una matatizo yoyote, kwa sababu itakuwa ni jambo la ajabu kwamba utazuwia maendeleo ya jimboni kwako mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, natangulia kusema kwamba kwaniaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi, ambao nawashukuru sana wameshanichagua kwa vipindi vitatu mfululizo na *Inshaallah* bado najihisi nina nguvu, nina hakika na kipindi cha nne *Inshaallah* watanichagua. Kwa hivyo, nakubali kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Naibu Spika, tunapata funzo gani ndani ya uwamuzi huu ambao Serikali imetoa. Wananchi wetu sasa hivi wamebadilika sana, wananchi wetu sasa hivi wanaelewa na wanafahamu nini maana ya maendeleo. Kamati za maendeleo zipo katika majimbo yetu sasa hivi nyingi tu na zina viongozi mbali mbali na zinasimamiwa na watu

mbali mbali na sisi Wabunge na Wawakilishi tunazijua Kamati hizi. Ni imani yangu sasa uamuzi wa mswada huu unampeleka Mwakilishi moja kwa moja kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya maendeleo ya jimbo, kwa sababu yeye anakuwa ndio Mwenyekiti wa ile kamati yenyewe. Maana yake nini hapa. Hapa inatupa fursa maalum sisi Wawakilishi, Serikali imetusogeza karibu zaidi na ndilo jukumu letu. Nitashangaa kusikia kwamba kuna Mwakilishi au kuna Mbunge ambaye hana habari na Kamati zozote ambazo ziko kwenye jimbo lake, sidhani kama wapo kama hao. Kwa sababu Kamati hizo zinakuja kwetu sisi zinatueleza matatizo yao na maendeleo mbali mbali.

Kwa hivyo, mimi napongeza sana kwamba sasa hivi imewekwa kwenye sheria kabisa, sasa wananchi wakija kulalamika kwamba Mwakilishi hatumuoni au Mbunge hatumuoni basi hilo litakuwa ni jambo la ajabu, kwa sababu kuna mfuko maalum ambao wewe ndio Mwenyekiti, sasa pesa zipo Mwenyekiti huonekani basi itakuwa ni jambo la ajabu sana. Mimi nina hakika hili litatupa fursa maalum Waheshimiwa sote tutakuwa karibu na majimbo yetu kwa lengo la kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo tunapata funzo hapa ni kwamba tunaanza kuwapa nguvu wananchi wetu, yaani tunawawezesha wananchi wetu sasa hivi kuweza kusimamia maendeleo yao wenyewe kwenye kamati zao, na wao sasa ndio watakaoamua. Sio kwamba unatoka tu huko Mwakilishi una msaada wako, una pesa zako unakwenda kuamua mimi nataka mradi fulani hapana. Sasa hivi tunatakiwa tushirikiane na wananchi wetu kwenye kamati za maendeleo, tukae nao na tushirikiane nao. Sisi kama ni Wawakilishi madamu tumepewa uwezo wa kuchagua wajumbe wale, sheria inasema wazi Madiwani wawili, lakini na kule kwenye kamati ya maendeleo ya mfuko wa jimbo kwa upande wa jimbo mbunge vile vile naye nadhani kuna Madiwani kama hao, sifikirii kama utawachagua Madiwani wale wale, nina hakika kwamba utatafuta Madiwani wengine, ili kile mmoja apate nafasi ya kushiriki.

Vile vile kuna nafasi ya Masheha wawili, lakini pia wewe ndio unayechagua Katibu na mimi imani yangu kwamba utamchagua Katibu, kwa sababu hii ni Kamati ambayo inahitajia kusimamiwa vizuri kwa utaalamu mkubwa ambao ni *qualify* tutamuweka pale. Mtu mwenye busara nafasi hiyo umepewa wewe Mwakilishi kushirikiana na Kamati mkaweza kumchagua.

Kwa hivyo, mimi nadhani sasa hivi umefika wakati wa sisi viongozi kukaa na wananchi wetu tukajiamulia maendeleo yetu wenyewe. Katika hili nina hakika hatutofanya, lakini binadamu lazima tuseme, tuna utashi wetu wengine binadamu inawezekana. Mimi nikenda jimboni kwangu na mwengine akenda jimboni kwake, tunachotakiwa ni kwamba hii ni Kamati ya maendeleo ya jimbo.

Hatari iliyokuwepo usije ukachagua watu waliokuwepo karibu yako wewe tu, na mimi nawanasihi wenzangu kwamba na nina hakika watafanya hivyo, wala wasije wakasema kwa nini anatufahamisha kwani sisi hatujui. Nina hakika tunajua, lakini Kamati ya maendeleo ya jimbo na ndio maana zikatolewa humu kwenye mswada masuala ya dini na masuala ya siasa yakiwemo ili tusije tukajiingiza katika mtego kama huu.

Kwa hivyo, mimi nina hakika kabisa kwamba Kamati zetu hizi zitatusaidia. Fursa ambazo tumepata sio kidogo Mheshimiwa. Leo tumeanza na milioni 10. Lakini tutizame milioni 10 ambazo wewe Mwakilishi utapewa kwa ajili ya maendeleo ya jimbo lako na Mbunge huku kuna milioni tuseme 25, kwa mwaka mmoja jimbo linapata milioni 35, kwa miaka minne hii iliyobakia jimbo litakuwa na uwezo wa kupata karibu milioni 140. Mhe. Naibu Spika, hiyo ni hatua kubwa sana na tuzipongezeni sana Serikali zetu mbili. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuja na uamuzi huo, tunazipongeza sana kwa hatua hiyo nzuri.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wamezungumzia suala la matumizi ya pesa hizi pengine katika masuala ya dini. Tujiulize sasa hivi Mhe. Naibu Spika, hivi sasa pesa hizi hatujazitumia, lakini tunasaidia miradi mbali mbali ya kimaendeleo. Miradi ya maji tunasaidia, mradi wa umeme tunasaidia, mradi wa hospitali tunasaidia, mradi wa ujenzi wa madarasa ya skuli tunasaidia na miradi mingine ya kimaendeleo, pesa zile zinatoka kwenye mifuko yetu kama ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, sasa tuone hapa kwamba tumeshapunguziwa mzigo sasa zile pesa ambazo ulikua uzipeleke kwenye hospitali kidogo au kwenye maji sasa Serikali imekusaidia fungu lile. Sasa lile la ibada ni sadaka yako na tunaambiwa ukitoa sadaka mkono wa kulia basi mkono wa kushoto usisikie. Sasa pesa zile ukizitoa watu wote ndio wanazisikia hupati thawabu, tumeshahimizwa kwenye dini kwamba si vyema ukitoa sadaka ya kidini mkono wa kushoto ukatoa mkono wa kulia. Mimi nadhani tufike mahali iwe jambo lile ni sadaka, ulitoe mfukoni mwako na uendelee. Watu wanasaidia na tunaendelea kusaidia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla hapa alizungumza suala la mafunzo. Mimi nadhani sio vibaya, mafunzo ni kitu kizuri, lakini sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumepata mafunzo mbali mbali ya kusimamia miradi tumeletewa hapa, mafunzo ya kusimamia bajeti na mengine. Nadhani tuwe walimu wa kwanza sisi wenyewe Wawakilishi tutoe mafunzo kwenye Kamati zetu zile, nina hakika uwezo wa kuwasimamia na kutoa mafunzo tunayo, pale ambapo utahisi unahitajia msaada basi mimi nina hakika katika majimbo yetu kuna wataalamu mbali mbali, Wizarani kuna wataalamu mbali mbali na hata mkitaka msaada kutoka Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo au kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika basi tutakuja kusaidiana, lakini nina hakika uwezo wa kutoa mafunzo tunao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakusudia kusema kwamba hii ni hatua moja ya kutusaidia sisi Wawakilishi kupiga hatua kubwa zaidi sasa hivi. Tumeambiwa usimamizi tutasimamia sisi wenyewe, wala tusiogope kifungo na mambo mengine. Masuala haya Mhe. Waziri atakuja kutusaidia mimi sitaki kuzungumzia huko zitakapokua zinatumika fedha vibaya. Lakini pesa yoyote ya Serikali ni lazima itapitiwa na madamu itapitiwa basi ni kuhakikisha kwamba pesa hizi tunazisimamia vizuri. Mimi nina imani kwamba hakuna Mwakilishi hata mmoja ambaye atakuja kutumia pesa hizi kwa maslahi yake. Wawakilishi hawa watafurahi kwamba mwaka huu tumeanza na milioni 10 na mwakani *Inshaallah* tumeshapata fununu pengine itakuwa milioni 15, tutaendelea kidogo kidogo, lakini *Inshaallah* pesa hizi Mhe. Naibu Spika, zitatusaidia sana. Mimi namuombea Mhe. Rais wetu Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, afya njema *Inshaallah*. Lakini pia tujiombee na sisi wenyewe humu ndani Mwenyezi Mungu atupe nguvu na afya njema ili tuendelee kuwaongoza wenzetu tusaidiane *Inshaallah*, ili tupate maendeleo ya nchi yetu.
Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi nakushukuru tena na kwa kuthamini wakati wako sana, najua kuna dakika mbili tatu zimebakia, lakini nakuachia wewe Mhe. Naibu Spika, ili pengine una matangazo mawili au matatu. Mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru waliobahatika kuchangia katika kipindi chetu cha asubuhi. Tunategemea bado wachangiaji wataendelea katika kipindi cha jioni. Baada ya maelezo hayo mafupi, naahirisha kikao hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuendelea kuchangia mswada huu tunaoujadili hivi sasa kuhusu Maendeleo ya Jimbo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kwa kukaa na kutafakari na baada ya kuona kuwa, kweli Waheshimiwa Wawakilishi tunahangaika sana katika kuleta maendeleo kwenye majimbo yetu. Hivyo, kwa makusudi, serikali ikaamua kutekeleza mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi kwa leo sitokuwa na mengi ya kuchangia katika mswada huu, isipokuwa naomba ufafanuzi kwa baadhi ya mambo. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Jimbo imetolewa muongozo wake, na namna ya kukutana kadhalika. Lakini kuna sehemu moja kama kamati nyengine zilivyo sikuona.

Mhe.Mwenyekiti, wakati wote kamati inapofanya vikao huwa kunatokea mambo ambayo yanahitaji utaalamu. Kwa mfano, kwenye Mfuko wetu huu tunatakiwa tuidhinishe miradi pamoja na thamani ya kila mradi utakaoidhinishwa.

Kwa kweli kutathmini ni jambo ambalo linahitaji wataalamu, ikiwa ni maji basi wataalamu kutoka Wizara husika, ikiwa elimu ni hali kadhali. Sasa haikutiwa kuwa kamati inaweza kumualika mtu yeyote katika kikao chake japo kuwa atakuwa hana kura kwa ajili ya kusaidia kwa shughuli za kitaalamu.

Kwa hivyo, ninaomba Kamati ipewe uwezo katika vikao vyake iweze kuwaalika wataalamu pale wanapohisi inafaa, pamoja na kuwa wataalamu hao watakuwa hawapigi kura. Hilo ni moja.

Jengine imeelezwa katika Sheria hii kuwa kama itatokezea Mhe. Mwakilishi amefariki na ameacha miradi pale, kwa hivyo miradi ile ibakie vile vile bila ya kurekebishwa, yaani kufa kwake isisababishe miradi ile kupangwa vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya ya miradi hayajaanza leo, na yapo kwa muda mrefu sana, kweli tunajua kwenye majimbo yetu tunao Waheshimiwa Wabunge, na hawa nao wanapata fedha za kuendeleza shughuli zao za majimbo tena kuna miradi. Kwa mfano, wakati huu sisi hatujapata, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakitushirikisha kwenye vikao vyao na tumeiweka.
Sasa kama ikitokezea mradi aliouweka Mhe. Mwakilishi na ameondoka duniani, lakini mradi ule kumbe huko mwanzo ulikuwa umeshazungumzwa na Mhe. Mbunge akapata ufadhili wa kuendesha ule mradi, je si vyema pale pakaongezwa mradi mwengine, kwa sababu tayari ule mradi kwa njia nyengine umeshapata ufadhili. Hilo ni swali naomba nipatiwe jibu. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu haukutoa fursa ya kuchangia chochote kinachohusu siasa au dini. Kwa upande wa siasa Mhe. Mwenyekiti sina matatizo, lakini kwa upande wa dini naomba kutoa ushauri.

Mhe.Mwenyekiti, sote tuliomo humu ni Waislamu, yaani tumekuja duniani, tunapita na tunakwenda na huko tutakakokwenda ndio tutaishi milele. Tunajua kwamba Tanzania haina dini, lakini Watanzania wanazo dini, kwa sababu hiyo hata juzi mwenzetu alipofikwa na faradhi hapa, tulimleta katika Chombo hiki cha Kutunga Sheria cha Serikali na kumfanyia shughuli zote za kidini kama hali ilivyoturuhusu ikiwa pamoja na kumuombea dua.

Vile vile hata kwenye *Caucus* yetu, yaani *Briefing* tulieleza mambo ambayo hayakuwa ya Kiislamu yaliyojitokeza, kwa bahati mbaya ya yule mwenzetu na tukasema iwe ni mwisho.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninaloliomba ni kuwa Mfuko uruhusiwe kwa kusaidia maendeleo ya dini kama vile kujenga misikiti na kadhalika na sio kusoma maulidi na mengineyo watu wakachinja mbuzi, lakini iwe kujenga misikiti na kadhalika. Kwa maana hii itakuwa na sisi tumejiweka pazuri kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa huko mbele ya safari tunakokwenda pamoja na hao walioubuni Mfuko huu. *(Makofi)*

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa katika Mfuko kuwa wale watu ambao ni *signatories*, yaani watakaoweka saini katika kuweka na kutoa fedha imeambiwa ama Mwakilishi (a) Mwenyekiti au Katibu. Kwa kweli Mwenyekiti au Katibu maana yake ni mtu mmoja na mjumbe yeyote mwengine. Kwa maana hiyo, hapa Mwenyekiti umemuweka sawa na Katibu, kwa sababu ukisema huyu au yule, ina maana kwamba wote wako katika nguvu sawa.

Kwa hivyo, kwa kuweka sawa maelekezo na kusitokee kugongana, basi ni bora kuongezwe ikiwa Mwenyekiti hayupo, basi Katibu atachukua nafasi yake kuliko kusema Mwenyekiti au Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu apishie mbali pengine Katibu anayo mipango yake na kutia saini na Mwenyekiti yupo pale na wala asiambiwe, kwa sababu itakuwa ile sheria imemruhusu. Kwa hiyo, naomba pale pakae sawa na iwe ikiwa Mwenyekiti hayupo, basi Katibu ndio achukue nafasi yake. Hilo ni jengine.
Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la kuunda Kamati ya Utekelezaji, ambayo kwa mujibu wa mswada huu itaundwa na wananchi. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa vile Kamati hii ya Maendeleo ya Jimbo ndiyo inayohusika na kupokea miradi kutoka kwa wananchi, kuainisha miradi, kupiga kura wanaokubaliana na kadhalika.

Kwa hivyo, nadhani ni vyema kwa kuondoa matatizo, basi ndani ya Kamati hii ya Jimbo ingeundwa Kamati ndogo na ikawa ni Kamati ya Utekelezaji, Ufuatiliaji na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha jioni hii tukaweza kukutana katika Baraza letu hili tukufu.

Vile vile nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, ambae umenipa nafasi hii kuweza kusimama hapa jioni hii.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana pamoja na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kuuleta mswada huu wakati muafaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nimshukuru Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutuliza kilio cha Waheshimiwa Wawakilishi cha siku nyingi cha kuona wanajisikia wanyonge katika majimbo, wakati wenzao Waheshimiwa Wabunge wanapata Mfuko wa kuendeleza maendeleo, lakini wao walikuwa wamekosa. Kwa kweli hivi sasa wamefikiriwa kuanza kuupata Mfuko huu, yaani itakapopitishwa tu sheria hii basi na wao wataanza kujisikia wanazo nguvu fulani katika majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kwa kuletwa mswada huu nikiwa na mimi ni mwananchi ambaye ninalo jimbo langu tena ninaye mwakilishi wangu katika jimbo, ambapo fedha hizi zikipatikana, basi naamini wanawake wa jimbo lile nao wataweza kufaidika na maendeleo ambayo yatafikiwa katika mradi wowote tutakaoamua kuupanga, nadhani tunaweza kufikia mahala pazuri na sisi tukajisikia.

Kwa hivyo, ndio maana nikapata hamasa ya kuuchangia mswada huu, ili uweze kupita bila ya wasi wasi kwa kujua na sisi wanawake tutafaidika katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia mswada huu kwa kuwashauri Wawakilishi, ambao wanakusudiwa kupata fedha hizi na hatimaye kuweza kuchagua kamati ambayo itaweza kuchagua kamati ya kusimamia fedha na kuendesha miradi katika majimbo.

Ushauri wangu ni pale kamati inapochaguliwa, basi Wawakilishi waweze kuchagua watu makini ambao wanao uwezo na pia wanapenda maendeleo na wala wasiwe wenye uchu wa kupenda kula fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Vile vile naomba kutoa ushauri kwa Mhe. Waziri kwamba pale tu baada ya kuchaguliwa zile kamati, basi ni vyema kamati hizi angeweza kuzikusanya kwenye mikoa yao, kwa ajili ya kupatiwa mafunzo maalum yanayohusu uendeshaji wa miradi katika majimbo.

Kwa kweli tukizingatia hasa kwa wale watakaokuwa washika fedha, basi ni vyema kuweza kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara, ambayo yatakayowapa uelewa wa matumizi mazuri pamoja na uwekaji mzuri wa mahesabu.

Mhe.Mwenyekiti, nashukuru sana mswada huu umeweka uangalizi mzuri wa fedha. Kutokana na hali hii, hapa napata matumaini kwamba fedha hizi kwa uangalizi uliowekwa zinaweza kutumika vizuri na kuleta manufaa mazuri.
Kwa hivyo, nawaombea Wawakilishi wote wa majimbo wafanikiwe vizuri katika kuzitumia fedha hizi, ili tumpe Mhe. Rais matumaini mazuri na hatimaye apate hamasa kubwa na kutuongeza nyengine mara mbili zaidi kuliko ya hizi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nasema na sisi Wanawake wa Viti Maalum tunacho kilio cha maendeleo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti kwamba atupelekee salamu zetu hizi kwa Mhe. Rais kuwa wanawake na sisi tunao wivu wa maendeleo, ili na sisi tuweze kupatiwa *percentage* yoyote katika Mfuko huu. *(Kicheko/Makofi)*

Lengo ni kuwasimamia wanawake katika mikoa yetu, kwa sababu kama tunavyojua akina mama ni wadau wakubwa wa Serikali hii tena wanajituma sana, ili kuweza kuona familia zao zinaishi vizuri na wanamudu kuwasaidia akina baba majumbani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu ni hilo naomba na sisi akina mama tuangaliwe kwa jicho la huruma, kwa sababu bado akina mama tunayo majukumu makubwa, na kama utafanywa utafiti wa kina, basi utaona akina mama wanajituma sana na wapo karibu sana kwa ajili ya kuwasaidia watoto wao pale wanapopasi maskulini, ili waweze kuwasaidia fedha kwa ajili ya kuendelea na masomo na pale wanapofeli, ili waweze kuwanunulia mitihani. Kwa kweli suala hili likifanyiwa utafiti basi itaonekana akina mama wanajitahidi sana katika hili. Kwa hivyo, naomba na sisi tuweze kupatiwa miradi mizuri tena mikubwa, ambayo itaweza kuwaweka akina mama pahala pazuri na kuweza kufanya kazi zao vizuri, na hatimae wakawa na wao ni wakombozi wa familia na hata akina baba majumbani.

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi ya kusema kuhusu mswada huu, kwa sababu nahisi umekaa vizuri na wenzangu wamejitahidi kurekebisha mule mwa kurekebisha. Lakini naupongeza sana Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo utakapofikia, basi *Inshaallah* nawaombea dua Waheshimiwa Wawakilishi Mwenyezi Mungu awawezeshe kufanya vizuri kwa ajili ya kupata mafanikio kwa sote.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii angalau kueleza machache kuhusiana na hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai, hatimae kutupa nguvu na uwezo wa kuingia katika jengo hili la Kutunga Sheria. Kwa kweli hii ni hazina kubwa ambayo ametujaalia Mwenyezi Mungu kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru. Nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuitumia fursa hii katika hizi za mwisho na mimi kuweza kuingiza chochote kuhusiana na hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi kwa kuweza kufikiria kwa kutuletea mswada huu. Kwa kweli huu ni mswada muhimu sana kabisa, sio tu kwa ajili ya maendeleo, lakini hata katika kukijengea hadhi hiki chombo cha Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Chombo hiki, yaani Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni miongoni mwa Mabunge ya *Commonwealth*. Kwa hivyo, nashukuru kwamba kuletwa kwa mswada huu kwa kiasi kikubwa kutapunguza ile tofauti iliopo baina ya Baraza hili la Wawakilishi pamoja na Mabunge mengine ya Jumuia ya Madola. *(Makofi)*

Matarajio yangu ni kwamba mswada huu utasaidia sana katika kuleta maendeleo pamoja na kukidhi viwango vya *Commonwealth*.

Sambamba na hilo ni matarajio yangu kuwa Serikali yetu ya *GNU* pia haitaleta Mfuko huu tu katika kutuweka sawia kwenye Mabunge ya *Commonwealth,* lakini hata kwenye maduhuli mengine nadhani huenda ikafikiriwa kuwekwa sawa na Mabunge mengine ya Jumuia ya Madola.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli mswada huu umechelewa na ilikuwa uje kabla ya hapa, lakini nadhani kutokana na shughuli mbali mbali za Serikali imeamua kutuletea leo mswada huu na kwa vyovyote vile basi matarajio yangu ni kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa ujumla watauunga mkono mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko huu wa Maendeleo ya Jimbo mbali ya kuleta maendeleo kwenye majimbo yetu, pia utaleta uongozi mizania baina ya Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge. Kwa kweli kama tunavyofahamu katika majimbo ya Zanzibar kuna viongozi wawili, yaani kuna Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi kwenye jimbo moja.

Lakini jambo la kusikitisha katika kipindi hichi Waheshimiwa Wabunge wametupita sisi Waheshimiwa Wawakilishi kwa hatua kubwa sana, kwa sababu wao walikuwa wakitumia fedha zao za *CDF* na sisi walikuwa hawatushirikishi kwa lolote.

Kwa hivyo, matarajio yangu ni kwamba Mfuko huu wa *CDF* utaleta uongozi mizania katika majimbo na kuondoa ile tofauti iliopo baina ya Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge. *(Makofi)*

Mhe.Mwenyekiti, tofauti haitokuwa kubwa, lakini matarajio yangu ni kuwa kwa sababu wenzetu mfuko wao umetanuka kidogo, basi matarajio yangu kwamba hapo baadae Serikali inaweza kuongeza kiwango, kwa sababu shilingi milioni 10 ukilinganisha na za Waheshimiwa Wabunge ni kidogo mno. Kutokana na hali hiyo, nadhani Serikali italiona hili na hatimae wanaweza kuongeza, kwa ajili ya kutuweka sawa katika majimbo.

Mhe.Mwenyekiti, nikiangalia Sehemu ya Pili ya Mswada huu kuna Vyanzo vya Fedha, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 4 (a) na (b) kuhusu Vyanzo vya Fedha kinaeleza hivi:-

“4. Mfuko utawekwa:-

(a) Jumla ya fedha zilizotengwa katika Bajeti ya Serikali kwa madhumuni ya maendeleo ya Majimbo;
(b) Fedha nyengine yoyote itakayokusanywa au kupokelewa kutoka katika vyanzo vyenginevyo".

Mhe. Mwenyekiti, nadhani mfuko huu zaidi chanzo kikubwa ni Bajeti ya Serikali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi aniambie vyanzo vyengine ni kutoka pale jimboni au wapi, kwa sababu sidhani kama mfuko huu unaweza kuendesha biashara kwa ajili ya kutoa mapato sehemu nyengine. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aje aniweke sawa hapo.

Mfuko huu pamoja na kuleta maendeleo, lakini utasaidia zaidi ile dhamira ya Serikali ya kupunguza umasikini katika majimbo yetu. Mhe. Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza ni kwamba hali ya umasikini imetanda, uwezo wa Waheshimiwa Wawakilishi ni mdogo. Lakini kuwepo kwa mfuko huu naamini kwamba utatusaidia sana kwenye majimbo yetu katika suala la kuongeza kipato na kupunguza umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Sehemu ya Nne ya Mswada huu kifungu cha 12 kuhusu suala la Uidhinishaji wa Miradi katika Kamati, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 12(1) na (3) Uidhinishaji wa Miradi katika Kamati kinaeleza hivi:-

"(1) Kamati itapendekeza miradi kabla ya mwisho wa mwezi wa Disemba wa kila mwaka.

(3) MKurugenzi ataweza kurudisha miradi kwa Kamati pale ambapo itabainika vigezo havikuzingatiwa, ili Kamati iifanyie kazi kabla ya kuiwasilisha tena kwa Mkurugenzi".

Mhe. Mwenyekiti, huyu Mkurugenzi amepewa kazi kubwa sana hapa, na kwa kweli nahofia kwamba mamlaka aliyopewa Mkurugenzi hapa inaweza kuidhalilisha Kamati pamoja na Mwakilishi ambaye ni Mwenyekiti wa huu mfuko.

Kwa hiyo, Kamati ndio inayokaa katika jimbo akiwemo Mhe. Mwakilishi na ndio inayojua changamoto za maendeleo katika jimbo. Sasa leo Kamati tayari imeshapendekeza miradi, na Mkurugenzi ambae yupo Makao Makuu Unguja Mjini hapa yeye ndie ajue zaidi kuliko ile Kamati ambayo ina Mwakilishi, Madiwani pamoja na Masheha, kwamba yeye atakuwa ni bora zaidi.
Mhe. Mwenyekiti, nadhani kipengele hiki kitolewe na badala yake Mkurugenzi afuatilie tu matumizi mazuri ya fedha hizi, lakini pale ambapo Kamati imeshapendekeza, basi asipewe mamlaka ya kutengua maamuzi ya kikao. Kwa maana hiyo, bila ya shaka miradi hii imepitishwa katika vikao, yaani vikao vimeamua chini ya uongozi wa Mhe. Mwakilishi ambae ni Mwenyekiti, wapo Masheha pale pamoja na Madiwani, yaani wameamua kabisa kwamba miradi yetu ni hii, sasa leo anakuja kutengua maamuzi ya kikao.

Mhe.Mwenyekiti, nafikiri katika hili kipengele hiki hakifai na kiondoshwe kabisa, ili kusudi tusiingize ukiritimba katika Mfuko huu.

Mhe.Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikiria jambo la maana kabisa na mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Vile vile ili kujiweka sawa baina ya Baraza letu hili la Wawakilishi na Mabunge mengine ya Jumuia ya Madola, basi waangalie pia katika maduhuli mengine.

Mhe.Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia japo kidogo kwa sababu suala hili na mimi limenigusa. Kwanza kama walivyotangulia wenzangu tokea kuanza kwa kikao hiki cha Baraza niseme natoa salamu zangu za rambirambi kwa wazee pamoja na ndugu wa marehemu aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu Mhe. Salum Amour Mtondoo. Vile vile nimpongeze Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kwa kuapishwa rasmi kuwa Mjumbe wa Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe.Mwenyekiti, kama walivyotangulia wenzangu ni kwamba nitoe shukurani zangu za dhati kwa waziri husika kwa kutuletea mswada huu, ambao kwetu sisi itakuwa ni faraja kubwa kwa kuja kwa mswada huu. Kwa kweli sisi kama ni viongozi wa majimbo, na tunawakilisha majimbo, basi kuna changamoto nyingi ambazo zilikuwa zinatukabili na kwa sababu kulikuwa hakuna mfuko huu, ilikuwa changamoto hizo tunazikabili kwa kutoa fedha mifukoni mwetu. Kwa hivyo, leo hii ni faraja kwetu. Sasa kwa vile ni fedha na zinatakiwa zitumike kwa utaratibu ambao unafaa, basi lazima tuwe makini na waadilifu, ili tuweze kuzitumia fedha hizi kwa kufuata yale masharti pamoja na kanuni za fedha ambazo zipo katika matumizi.

Mhe.Mwenyekiti, niseme kwamba kwa kuwa tumepewa fedha hizi, basi ni lazima tukubali yale masharti ambayo yamewekwa kwenye mfuko huu, kwa sababu baadae nina hakika pesa hizi zitakuja kufanyiwa ukaguzi. Kwa hivyo si vizuri kuzitumia bila ya kufuata zile taratibu na sheria za fedha.
Mhe.Mwenyekiti, sehemu ya tano inasema utekelezaji wa miradi, kutakuwa na kamati ya utekelezaji wa miradi chini ya sheria hii, sawa sawa mimi nakubaliana nayo, na ni lazima tufuate utekelezaji wa mradi kama ulivyo katika sheria hii, vile vile kwa sababu kamati itakuwa dhamana ya matumizi yote ya malipo yatakayofanywa.

Mimi vile vile naunga mkono kifungu hiki kwamba, kamati iwe dhamana wa matumizi, kwa kweli mimi mwenyewe nasema nitatekeleza yote yale kwa sababu najua mambo ya hesabu mimi nilikuwa ni mhasibu, kwa hivyo zile sheria ambazo zitakuwa zinaambatana na mradi huu basi naahidi na wenzangu vile vile.Vile vile, wenzangu wamesema hapa kina mama na wao, kwa sababu nisijisemee mimi peke yangu kama alivyosema Mhe. Panya kwa hivyo na mimi naunga mkono kama kikipatikana na wao angalau kidogo wagaiwe ili waweze kufarijika, baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana ingawaje ulikuwa umeshafika ukingoni lakini niliona ishara tu, kwa hivyo naunga mkono hoja hii mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Amani. *(Makofi)*

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti naomba kuchukua fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kufanya majumuisho, lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote wa baraza hili tukufu, kwa michango mizuri waliyoitoa, nataka niwahakikishie waheshimiwa wajumbe kwamba, michango yao kwetu ilikuwa ni dira ya kuzidi kufanya vizuri katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Mhe.Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu niwataje waheshimiwa ambao walichangia mswada huu, jumla ya waheshimiwa waliochangia walikuwa kumi na nane (18), waheshimiwa kumi na nne (14) walichangia moja kwa moja, na waheshimiwa (4) walichangia kwa maandishi. Naomba niwataje wale waliochangia moja kwa moja.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wakuu wa Kitaifa.
2. Mhe. Moh'd Haji Khalid
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
4. Mhe. Rashid Seif Suleiman
5. Mhe. Hija Hassan Hija
6. Mhe. Omar Ali Shehe
7. Mhe. Moh'd Mbwana Hamad
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
10. Mhe. Mbarouk Wadi Mtando
11. Mhe. Haroun Ali Suleiman
12. Mhe. Salim Hamad
13. Mhe. Panya Ali Abdalla
14. Mhe. Saleh Nassor

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1 Mhe. Nassor Salim Ali
2 Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
3 Mhe. Abdi Mossi Kombo
4 Bikame Yussuf Hamad

Mhe.Mwenyekiti na waheshimiwa wajumbe, napenda tena kutoa shukurani zetu za dhati kabisa kwa wale wote waliochangia, kama nilivyosema waheshimiwa wajumbe wengi walitupa ushauri, nataka niwahakikishie kwamba ushauri tumeupokea na tunakwenda kuufanyia kazi.

Mhe.Mwenyekiti, madhumuni ya mfuko wa jimbo hasa hasa yanalenga katika kuunga mkono jitihada za wananchi za kuwaletea maendeleo yao katika majimbo yao, vile vile kutoa uwiano wa kimajimbo ili majimbo yaweze kwenda sambamba kimaendeleo, lakini pia ni kusaidia jitihada za Mheshimiwa Muwakilishi mwenyewe katika kusaidia wananchi wake, tunaelewa kwamba wananchi huwa wanamtegemea sana Mhe. Muwakilishi, leo hivi asubuhi kama mtakumbuka Mhe. Khalid alieleza kwamba muwakilishi ni kama waziri wa wizara zote katika jimbo lake. Msingi wake anaelezea kwamba kila sekta katika jimbo inamtumainia muwakilishi kuisaidia, na kusaidia wananchi wake, huo ndio ukweli wenyewe ulivyo, hii inatokana na hali halisi ya hali yetu ya uchumi, hali halisi ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, mimi kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza sana sana waheshimiwa wawakilishi kwa kazi kubwa wanazofanya katika majimbo yao ya kuleta maendeleo.

Mhe.Mwenyekiti, lengo letu hasa katika jambo hili kama walivyosema wawakilishi wengi, ni kuongeza fedha hizi kadiri ya uwezo wa serikali utakavyowezekana ili kila mwaka tuweze kuongeza fedha hizi za maendeleo ya jimbo, na hii hasa ndio dhamira ya serikali, lakini itategemea sana na matokeo ambayo wananchi kwa kushirikiana na muwakilishi wao namna ambavyo miradi hii itakavyokuwa endelevu, itakavyotekelezwa na suala zima la kusimamia vizuri fedha hizo ambazo zinatolewa, kama fedha hizo zitasimamiwa vizuri, utekelezaji utakuwa mzuri, na hapana shaka yoyote kuwa utavutia serikali kuongeza fedha hizo katika majimbo yetu.Kama taarifa ilivyotoka kwamba,Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo alielezea hapa kwamba, katika mwaka unaokuja wa fedha basi tutaondoka kwenye kiwango cha milioni kumi na tutaelekea kwenye kiwango cha milioni kumi na tano, tuombe dua mambo yaende vizuri, na ahadi hiyo itekelezwe kama ambavyo imeahidiwa. Lakini jambo la msingi hapa, ni kujenga mashirikiano mazuri katika kuyasimamia hayo mambo yetu huko majimboni ili yatoe matunda mazuri.

Mhe.Mwenyekiti, kuhusu suala la matumizi kusimamiwa vizuri, sheria ile ya fedha za umma ndiyo ambayo itatoa muongozo wa matumizi ya fedha hizi katika majimbo, kwa hivyo mimi sina shaka yoyote kama utaratibu utafuatwa vizuri, hatuna haja ya kuwa na wasi wasi kwa jambo hili, mambo yatatekelezwa vizuri kwa sababu mifano ipo, kuna miradi mingi ambayo imetekelezwa na haikuzua matatizo yoyote, wala wananchi hawakupata matatizo yoyote. Cha msingi hapa ni kuwa na nia njema kwamba nia yetu ni kutekeleza miradi hii kwa maendeleo na manufaa ya watu wetu.

Ile dhana ya kukosekana kwa ujuzi kwa wananchi wetu, jambo hili litashughulikiwa kwanza kwa kutoa mafunzo kwa wana kamati hawa, lakini pia sekta husika zitaendelea kusaidia na kushirikiana na wana kamati na wananchi katika majimbo yao, ili utekelezaji uwe mzuri na usitoe matatizo ya aina yoyote, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais itaendelea kuratibu jambo hili, kwa kushirikiana na majimbo na viongozi wa majimbo, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaelewa taratibu zilizopo na taratibu za kisheria, ili kuepuka matatizo ambayo yangeweza kutokea.

Kuna suala lilizungumzwa sana na waheshimiwa wajumbe hapa, kuhusu kwamba kuna kamati nyingi, Mhe. Mwenyekiti na waheshimiwa wajumbe, kamati sio nyingi, kamati zilizopo hapa ni mbili tu, kwa maana ya kamati kubwa ambayo ni ile kamati ya maendeleo ya jimbo, ile kamati ya matumizi moja katika mamlaka ya ile kamati ya maendeleo ya jimbo ndio itakuwa pia kamati ya matumizi, kwa hivyo kamati ya matumizi ni ile ile kamati ya maendeleo ya jimbo, ni moja tu katika kazi yake.

Kamati ya utekelezaji, hii waheshimiwa wajumbe ninayo mifano yake sana, kwa sababu katika majimbo yetu mbali mbali, nyote mnaelewa kwamba kwenye ile miradi wananchi wenyewe hujitokeza kuisimamia ile miradi ili itekelezwe vizuri, kwa mfano katika jimbo la Mji Mkongwe kuna mradi wa skuli eneo la Shangani, kwa hivyo wananchi wa Shangani wenyewe ndio wanaojikusanya, wakashirikiana na kamati yao ya Maendeleo, kusimamia ule utekelezaji uende vizuri, si kwamba kamati hii itakuwa imetokana na kamati ile kuu ya jimbo, lakini Kamati kuu ya Jimbo inaweza kutoa maelekezo, ni wale wananchi wenyewe kwenye maeneo yao unapoanza mradi namna wanavyousimamia, ili utekelezaji uende vizuri na kuwepo na ushirikiano wa kutosha.

Kuhusu marekebisho mbali mbali yaliyofanywa na kamati yetu, kwanza nataka kusema marekebisho yale sisi tumeyapokea, na ni sehemu ya mswada huu, tayari yalikwisha gaiwa bahati nzuri au mbaya, baadhi ya waheshimiwa walikuwa hawakuyapitia vizuri yale marekebisho na matokeo yake wakarekebisha yale ambayo yamesharekebishwa. Kwa hivyo, ile kamati ilifanya kazi nzuri kufanya marekebisho makubwa, na naamini itatusaidia sana, hata kwenye mswada ule kwenye kamati, utaona sehemu nyingi zinazungumzia Mkurugenzi, sasa yale maeneo ambayo yamewekwa Mkurugenzi mengi yatakuwa hayapo, isipokuwa kwenye kile kifungu cha namba sita tu ndio Mkurugenzi anabakia, lakini sehemu nyengine zote anabakia Katibu Mkuu, na hii inatokana na kwamba itaenda sambamba na ile sheria ya matumizi ya fedha za umma, ili katibu Mkuu awe na haki ya kusaidia katika harakati nzima za kuleta maendeleo ya jimbo kwa wananchi wetu.

Kuhusu adhabu ni kweli adhabu ni kubwa, na kwenye hili tutashirikiana basi na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ili tutizame namna gani ya sheria nyengine ambazo zenye makosa yanayolingana na haya, ili tuweze kuweka adhabu inayolingana na kosa lenyewe, tusitoe adhabu kubwa ambayo hailingani na makosa yenyewe. Mimi nakubaliana kabisa, na ushauri tunauchukua waheshimiwa wajumbe na tutaufanyia kazi, ili adhabu yenyewe ilingane basi na hali halisi ya kosa lilivyo.

Kuhusu fedha za uendeshaji wa miradi unaratibiwa vipi au unasimamiwa na nani, zile fedha ambazo zitatengwa kwa ajili ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa shughuli za uendeshaji na sana zitahusu mambo ya *stationary* mambo ya usimamiaji na mambo mengine, fedha hizi zitasimamiwa na sheria iliyopo sasa ya fedha za umma kwa sababu itakuwa ni sehemu ya bajeti ya serikali kwa maana hiyo zitachunguzwa kwa utaratibu wa kawaida kama taratibu zinavyofanyika katika sekta nyengine, au kwenye idara nyengine. Kwa hivyo uhakika wa kwamba, fedha hizi hazitotumika vyenginevyo utabakia pale pale, vyenginevyo utakwenda kinyume na sheria, na fungu lake litakuwa linaingizwa na kila mmoja atakuwa analifahamu.

Mhe.Mwenyekiti na waheshimiwa wajumbe, suala moja kubwa limejitokeza hapa kuhusu mfuko kuruhusiwa kusaidia mambo ya dini, jambo hili Mhe. Haroun Ali Suleiman alilitolea ufafanuzi sana na ufafanuzi wake umekuwa mzuri, lakini naamini waheshimiwa wajumbe, jambo hili tukilichukulia kwa misingi mizuri na kulisimamia vizuri litakuwa haliwezi kutuletea matatizo. Lakini kama tukilikosea namna ya kulisimamia linaweza kutuletea matatizo, kwa sababu ni kweli wananchi wetu wana dini zao, lakini serikali yetu haina dini, kwa hivyo jambo hili nafikiri mutuachie tuzidi kutafakari tuone namna gani tunaweza kulifanyia kazi vizuri ili lisilete matatizo katika utekelezaji.

Mhe.Mwenyekiti baada ya maelezo haya ya jumla, ningeomba sasa nijibu hoja moja moja kutokana na zilivyochangiwa na Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nianze na Mwenyekiti Mhe. Hamza Hassan Juma yeye alitaka tuone mafanikio yanayotokana na mfuko wa jimbo, akatutolea mfano mzuri wa matukio yaliyotokea Kenya, ushauri huo Mwenyekiti tunaupokea na naamini tutajifunza zaidi kupitia kwa wenzetu walioko Kenya.

Lakini kuhusu serikali kuongeza fedha katika mfuko wa jimbo, nia ni hiyo hiyo na maelezo yametolewa.

Kuhusu kuweka kumbukumbu vizuri za matumizi hatua hizo zitachukuliwa ili mambo yaende vizuri.

Kwa upande wa Mhe. Mohammed Haji Khalid yeye alitaka pia na wenzetu wa viti maalum wanawake, nao watizamwe mfuko wao, jambo hili linategemea sana na uwezo wa nchi kifedha na kiuchumi. Ushauri acha tuuchukue na tuufanyie kazi tutizame hali itakavyoruhusu tuweze kulishughulikia jambo hilo, lakini kwa sasa hali yetu ya uchumi kwenye jambo hili bado ni ngumu, pale hali ikiwa nzuri tutalifanyia kazi vizuri, lakini hasa lengo la sheria hii ni kusaidia maendeleo katika jimbo.

Mhe.Hemed Suleiman Khamis yeye alitaka tuweke vipaumbele katika miradi, ushauri wake ni mzuri, kuongeza fedha ni ushauri mzuri na ufafanuzi umetolewa.

Mhe.Rashid Seif Suleiman yeye alitaka kujua kuhusu kamati tekelezaji, naamini ufafanuzi wangu utakuwa umekidhi haja kwake, vile vile alitaka kujua kamati ya manunuzi, ufafanuzi nafikiri utakuwa umekidhi haja yake.

Mhe.Hija Hassan Hija yeye mambo mengi aliyazungumzia, pia alizungumzia kuhusu ujenzi wa Ofisi za Jimbo kwa waheshimiwa Wawakilishi, huu ni ushauri mzuri tunaupokea lakini itategemea pia na hali ya uwezo wa nchi kadiri

ya fedha zitakapopatikana ndio tutakapoweza kufanya mipango hiyo, wazo hili lipo, lakini tatizo ni hali halisi ya uchumi wetu, kadiri fedha zitakapopatikana basi tutaweza kushughulikia jambo hilo.

Vile vile alizungumzia kuhusu fedha tutapata wapi kuweza kufanyia uchambuzi wa miradi, kwa maana alikuwa hapendelei zitokane na hizi pesa kidogo, ambazo zinatengwa kwa ajili ya jimbo, sisi nia yetu hasa ya kuweka jambo hili tunajua kabisa kuwa fedha hizi kidogo huwezi kutoa fedha hizo kufanyia uchambuzi, ndio maana tukataka sana sekta husika katika miradi itakayoandaliwa ziweze kusaidia katika kufanya uchambuzi wa miradi mbali mbali. Lakini hili tunaliweka kama akiba kwa siku za mbele, ambapo pale serikali itakapokuwa na uwezo mzuri na kuweka fedha nyingi katika majimbo, itabidi mambo haya ya kutafuta *consultant* na mengine yafanyike, kwa hivyo kwa sasa ni hakika kwamba fedha hizi ambazo zipo haziwezi kusaidia kwenye shughuli hii, lakini huko mbele inawezekana pakatokea mahitaji tukaweza kuzitumia, lakini pia ushauri wowote tutapokea waheshimiwa kama kufanyike marekebisho yoyote kwenye jambo hili.

Nafikiri kuhusu fedha za utaratibu wa uendeshaji nimezitolea ufafanuzi wa kutosha, kuhusu adhabu nafikiri vile vile nimelitolea ufafanuzi.

Mhe. Omar Ali Shehe alisema matumizi yatumiwe vizuri, ushauri naupokea na tutaufanyia kazi vizuri.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad ushauri wake pia na yeye tunaupokea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu yeye kwa kweli alitoa ushauri mwingi katika vifungu mbali mbali, nikianza na kifungu namba 6C yeye alitaka ule muda wa ripoti badala ya miezi mitatu uwe miezi sita, ushauri sio mbaya, lakini tatizo liliopo mazoea na utaratibu wetu katika serikali hivi sasa kila aina ya utekelezaji una ripoti ya miezi mitatu mitatu, kwa hivyo nafikiri bado tuendelee kutumia uzoefu huo ambao umetusaidia sana, ambao wa ripoti ya miezi mitatu mitatu.

Kuhusu kutatua migogoro, hili waheshimiwa wajumbe sisi hatuna matatizo nalo kama mkiona kipengele hiki tukiondoe, kwetu ni sawa tu hakina tatizo, sisi tuliweka kwa nia njema kabisa kwamba inapotokea migogoro ambayo tutaihusisha kidogo na upande wa serikali kusaidia kutatua, lakini kama waheshimiwa mtaona kipengele hiki tukitoe hilo tunalipokea na hatuna tatizo nalo.

Kuhusu kifungu namba nane kuwasilisha ripoti barazani, tokea hapo mwanzo kwa mujibu wa utaratibu ule, ripoti lazima inatakiwa iwasilishwe barazani.

Kuhusu kifungu namba 9b kamati ya maendeleo ni kubwa, tunaona pale tufanye marekebisho, labda tuseme isiwe zaidi ya madiwani wawili, kwa wale waheshimiwa katika majimbo yao watakaopenda kufanya hivyo basi watafanya ili tumalize hili tatizo.

Kuhusu kifungu namba 9(6) marekebisho tunayapokea kama alivyoshauri Mhe. Ismail Jussa Ladhu na kile kifungu cha 10(b) tayari ufafanuzi umeshatolewa kwenye marekebisho ya kamati.

Kuhusu kifungu cha 10 (d) ushauri tumeupokea maana ile inahusu kutekeleza kazi nyengine yoyote inayohusiana na mfuko wa maendeleo ya jimbo, kwa hivyo ile ni sahihi kabisa.

Kuhusu kifungu cha 11(2) tumepokea ushauri wake na tayari kilishafanyiwa marekebisho kama inavyoelekezwa katika marekebisho yanayofanywa na kamati, ni kama yale ambayo Mheshimiwa umetoa ushauri.

Kuhusu kifungu cha 14(2) kuhusu masahihisho ya marekebisho ya makosa ili waziri aweze kufanya marekebisho wakati yanapotokea masahihisho ya makosa, kwa hivyo nafikiri jambo hilo sio baya kama ambavyo ushauri tunaupokea.

Kifungu cha 15 kwa sababu tayari kuna mabadiliko kutoka kwa Mkurugenzi na sasa kinasomeka kama Katibu Mkuu naamini tumuachie katibu mkuu na timu yake kuweka vile vigezo badala ya waziri kama wao ni wataalamu nafikiri itakuwa ni busara zaidi.

Kifungu cha 16(3) tayari nafikiri tumetoa ufafanuzi kuhusu uchambuzi.

Kifungu cha 16(4) kuhusu shughuli za dini, hiki tutaendelea kupokea ushauri, mimi nadhani mawazo yangu kwamba tutumie busara zaidi na Mhe. Haroun Ali Suleiman alilitolea ufafanuzi zaidi.

Kifungu cha 24(1) ushauri tumeupokea na kifungu hiki kinaondoka.

Kifungu cha 26(2) hapa katibu ndio atasimamia pale patakapotokezea haja katibu mkuu.

Kifungu cha 30(3) kifungu hichi tayari kishaondolewa na kamati katika marekebisho yaliyofanywa na kamati.

Kwa upande wa Mhe.Abdalla Juma Abdalla suala la mafunzo litapewa kipaumbele, suala la uendeshaji wa mfuko tayari nimelitolea ufafanuzi.

Kuhusu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kwanza hili la katibu mkuu kwamba asikatae miradi, ukweli ni kwamba nia sio Katibu Mkuu kukataa miradi, nia pale ni katibu mkuu kusaidia marekebisho ili mradi ukidhi matakwa ya kisheria, hawezi kukataa ule mradi ambao unaletwa na maamuzi ya kamati yale ya jimbo na matokeo yake atasaidia tu pale ambapo pamewekwa mradi na hapakudhi yale matakwa ya kisheria, basi atafanya marekebisho aurudishe kule kwa ushauri zaidi lakini hawezi kukataa miradi ambayo tayari imepitishwa na wananchi katika majimbo yao chini ya muwakilishi wao.
Kuhusu fedha kutumika kwa mambo ya dini, hili bado linahitaji ushauri zaidi nafikiri mutupe muda kama nilivyoomba.

Kuhusu Mwenyekiti na Muwakilishi kusaini katika wale wanaotia saini za benki, hapa hizi fedha madhumuni yake hasa makubwa ni kusaidia Mheshimiwa Muwakilishi aweze kusaidia juhudi za maendeleo ya wananchi katika jimbo lake, kwa hivyo mlengwa hapa ni Mheshimiwa Muwakilishi mwenyewe. Kwa hivyo kwa njia moja au nyengine, sisi tunaona ni vyema Mhe. Muwakilishi bado saini yake iwepo kwenye kutoa fedha, kwa sababu atakuwa anazisimamia vizuri zaidi fedha hizi kuliko mtu mwengine yoyote.

Kwa hivyo mimi ninachoomba waheshimiwa, mambo haya tusiyatilie wasi wasi sana, la msingi hapa ni kufuata taratibu, na hapa wanaotakiwa kutia saini wasipungue watu wawili, ndio maana tukashauri wawepo watu watatu, wakati mwengine kama mmoja hayupo wale wawili watakaokuwepo waweze kusaini na fedha zitoke. Nia ni kuhakikisha kwamba utaratibu unakwenda vizuri zaidi.

Kuhusu marejesho kwamba wana kamati na wananchi hawana utaalamu wa kutosha, nafikiri nimeelezea kwamba utaalamu utatolewa, na sisi tuko tayari kushirikiana na wana kamati wetu na wananchi ili suala lifanyike vizuri.

Kuhusu fedha zisichanganywe kwenye akaunti ile ambayo itafunguliwa maalumu kwa ajili ya zile fedha ambazo zinatolewa na serikali, kwa hivyo jambo hili ni kwamba, huu ni utaratibu wa kawaida wa mahesabu kwamba fedha zile ziwe na hesabu yake maalumu, lakini wahisani hawakatazwi kuchangia miradi ile ya maendeleo katika majimbo yao isipokuwa kwenye akaunti ile hatutoweza kuchanganya fedha zile, ile itakuwa ni maalumu kwa ajili ya fedha zile zinazotoka mfuko mkuu na ziingie pale na zitumike kwa shughuli iliyopangwa. Lakini wahisani wanaruhusiwa kabisa kuchangia na mnaweza kuwa na akaunti nyengine lakini wahisani ni jambo ambalo linatakiwa sana kufanyika, tunawaomba waheshimiwa Wawakilishi jitihada hizo muzifanye ili watokee wahisani wengi katika kusaidia mambo mbali mbali ya maendeleo katika majimbo yetu.

Kuhusu suala la *CAG* kufuatilia utaratibu ule, nataka niwahakikishie waheshimiwa wajumbe na waheshimiwa wananchi, *CAG* madhali kuna fedha za umma pale lazima atafuatilia utaratibu huo, na hatuna namna nyengine yoyote ya kuepuka, kwa sababu ndio utaratibu halali ambao utahakikisha kuwa matumizi yetu yanakwenda vizuri na kwa kufuata taratibu zilizowekwa. Ninachokiomba mimi, ni kuhakikisha kwamba matumizi yetu yanakwenda vizuri na kwa taratibu zilizowekwa. Mhe.Haroun Ali Suleiman mimi nakushukuru sana kwa ufafanuzi mzuri, maelekezo mazuri, ushauri wako tunaupokea sana sana. Mhe. Salum Abdalla Hamad kuhusu uwezo wa kumualika mtu mwengine, huo ni uwezo wenu na maamuzi yenu mnaweza kumualika mtu ambae mnamuona anafaa aje awasaidie ushauri na ndio mambo ya miradi iweze kufanikiwa vizuri, hamna haja kuwa lazima mshikilie mradi ule kwa sababu tu aliouanzisha mwanzo kuwa hayupo tena. Mnayo haki ya kuanzisha mradi mwengine.

Hili sioni kama ni tatizo. Lakini kama nilivyokwisha eleza kwamba ni vizuri sana kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuwa nao ni sehemu ya saini hizo.

Mhe. Panya Ali Abdalla, ushauri tunaupokea, tutaufanyia kazi na nakupongeza na salamu zako tutazifikisha kunakohusika kama unavyotaka zifikishwe.
Mhe. Saleh Nassor ulielezea kuhusu kuongezewa fedha za mfuko, ushauri tunaupokea na unaendelea kufanyiwa kazi. Hivi vyanzo vyengine vya fedha ni vile kutoka kwa wahisani, wafadhili na wengineo.

Kwa hivyo hatutaki tuvikatae na tunawaomba waheshimiwa muendeleze jitihada hizo. Miradi haitofutwa kama nilivyosema kwamba, Katibu Mkuu yeye atashauri tu, zaidi ili mufikie vile vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria. Mhe. Fatma Mbarouk na wewe tunaupokea ushauri wako na tunakushukuru sana. Baada ya hayo Waheshimiwa, naomba niwashukuru sana Wawakilishi wote kwa michango yao na naamini itasaidia kuwa na sheria nzuri. Ahsante sana naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tunaomba utoe hoja sio kuwasilisha tu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo
Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kupitia Mswada kifungu baada ya kifungu.

Naomba kutoa hoja.

(*Hoja ilitolewa na kukubaliwa)*

Kamati ya Baraza Zima

Sehemu ya Kwanza - Utangulizi

Kifungu cha 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika
Kifungu cha 2 Ufafanuzi Pamoja na Marekebisho Yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Pili – Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar

Kifungu cha 3 Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 4 Vyanzo vya Fedha Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 5 Mgawanyo wa Fedha.
Kifungu cha 6 Kazi za Mkurugenzi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 7 Fedha Zitatunzwa na Mfuko Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 8 Mgawanyo wa Fedha Pamoja na Marekebisho yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Tatu – Kamati ya Maendeleo ya Jimbo

Kifungu cha 9	Kuanzishwa Muundo wa Kamati za Maendeleo ya Jimbo Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 10	Kazi za Kamati Pamoja na Marekebisho Yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza
Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Nne - Kukamilisha Mapendekezo ya Mradi ya Jimbo.

Kifungu cha 11	Mapendekezo ya Miradi ya Jimbo.
Kifungu cha 12	Uidhinishaji wa Miradi Katika Kamati Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 13	Uwasilishaji wa Fomu Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 14	Fomu za Maendeleo ya Mradi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 15	Sifa za Maelezo ya Mradi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 16	Miradi ya Jamii……..

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri, na kwa kukubali hoja nyingi za Wajumbe. Lakini kama alivyokubali hoja zetu ambazo alizoziona zina mantiki, naomba vile vile katika kifungu hichi cha 16 kifungu kidogo cha 4 ambacho nilikichangia wakati natoa mchango wangu kama walivyochangia wajumbe wengine, akubali vile vile kwamba ile *restriction* iliyokuwepo kwa kutumika fedha hizi katika misaada au miradi ya kidini pia akikubali.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini Mhe. Waziri na hoja zake, lakini nilivyokuwa nikichangia nilisema kwamba nchi yetu pamoja na kwamba unaweza ukasema ni *Secular*, lakini kutokana na *tradition* yake tuna mfumo maalumu wa kuendesha mambo yetu.

Ndio maana hata katiba yetu inatambua baadhi ya mambo ya Kiislamu, lakini haitambui baadhi ya mambo ya dini nyengine. Hili si jambo la ajabu Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika mchango wangu.

Katika nchi kama ya Uingereza pamoja na kwamba inaheshimu dini zote lakini Madhehebu ya Anglican ya Kikristo ndiyo yanayotambulikana kama vile ndio madhehebu ambayo ni rasmi. Na hapa kweli Rais hachagui Askofu Mkuu lakini anachagua Kadhi Mkuu, Mufti, kwa sababu ya misingi ya nchi yetu. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nasema wala hapakuwa na hofu iliyokuwepo kwamba ukiondosha hichi maana yake umetaja dini fulani. Lakini lile zuio tu la kwamba tusiweze ku- *support* miradi ya kidini ambayo nayo pia naweza nikasema ni ya maendeleo ya Jimbo.

Mimi bado sikubaliani nayo maelezo hayo na naomba Mhe. Mwenyekiti, Waziri atukubalie kwamba kifungu hichi kiishie pale kwa shughuli za kisiasa na yale maneno “na ya kidini” yaondoke. Halafu aiachie kamati, kwa sababu maamuzi haya haamui Mwakilishi kama Mwenyekiti. Itakuwa ni Kamati, itapima wenyewe maombi itakayoyapata na yakionekana yana msingi yanaweza kusaidiwa kama yanavyosaidiwa maeneo mengine. Namuomba sana Mhe. Waziri, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo mafupi na sio maelezo hasa, ni kusema kwamba nakubaliana na hoja ya Mhe. Jussa na hapa sasa basi, neno “ na ya kidini” litoke libakie mpaka hapo “za kisiasa”.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri na kwa sifa hizi za serikali, tutaendelea kushirikiana nayo milele. Naomba tuendelee, ahsante.

Kifungu cha 16	Miradi ya Jamii Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 17	Fomu Maalum Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 18	Zawadi Binafsi Haitoruhusiwa.
Kifungu cha 19	Uchangiaji wa Miradi utaruhusiwa Pamoja na Marekebisho Yake

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza
Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Tano – Utekelezaji wa Miradi.

Kifungu cha 20 Utekelezaji wa Ufuatiliaji wa Miradi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 21 Malipo na Manunuzi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 22 Miradi iliyopo na Yenye Kuendelea.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Sita – Fedha na Uendeshaji

Kifungu cha 23 *Account* ya Kamati Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 24 Kumbukumbu za Maingizo na Malipo.
Kifungu cha 25 Ukaguzi na Uhasibu.
Kifungu cha 26 Kumbukumbu za Malipo Pamoja na Marekebisho Yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Saba – Masharti Mengineyo.

Kifungu cha 27 Gharama za Uendeshaji wa Mfuko.
Kifungu cha 28 Kanuni Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 29 Nyongeza ya Miradi Mengine Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 30 …

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, niruhusu kwa mara nyengine tena nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuyakubali kimsingi mapendekezo ya wajumbe wa Baraza kukifanyia marekebisho kifungu kidogo cha 2. Kwa hivyo tumeshakubaliana lakini tu alipokuwa akifanya majumuisho alisema kwamba baadaye watakaa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kufanya marekebisho. Sasa kiutaratibu Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Baraza la Kutunga Sheria ni lazima tu- *specify* hivi sasa kwamba adhabu zinakuwaje.

Ni lazima nikiri, tulishauriana na wenzangu tukaona kwamba tupendekeze kwamba adhabu hii ikubaliwe na baraza kwamba tui- *specify* iwe kwa faini ambayo haitozidi milioni tatu au kifungo ambacho hakizidi mwaka mmoja au zote mbili. Namuomba Mhe. Waziri alikubali hili basi iwe ndio adhabu tunayoipendekeza. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na pia naomba nimshukuru Mhe. Jussa kwa ushauri alioutoa, nakubaliana na hoja hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. Ahsante sana.

Kifungu cha 30 Makosa na Adhabu Pamoja na Marekebisho Yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya Mabadiliko Yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imepitia Mswada wangu kifungu baada ya kifungu na marekebisho yake na kuukubali. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo
Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar Mwaka 2012 usomwe kwa mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kumaliza kazi hii nzito ambayo tulikuwa tunayo tokea asubuhi hii ya leo hadi wakati huu. Baada ya hapo nichukue fursa hii kuwatangazieni rasmi kwamba baada ya shughuli hii tunaakhirisha shughuli za Baraza hadi kesho asubuhi saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:15 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 30/03/2012 saa 3:00 asubuhi)